**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Nane – Tarehe 23 Juni, 2006**

*(Ulianza Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

***D U A***

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Shirika la Makumbusho ya Taifa kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2005 *(The Annual Report and Audited Accounts of the National Museum of Tanzania for the year ended 30th June, 2005)*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Taasisi ya Utafiti ya Wanyamapori Tanzania kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2005 *(The Annual Report and Audited Accounts of the Tanzania Wildlife Research Institute for the year ended 30th June, 2005).*

Taarifa ya Mwaka ya Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania kwa Mwaka 2004/2005 pamoja na Hesabu zilizokaguliwa kwa Mwaka 2003/2004 *(The Annual Report of the Tanzania Forestry Research Institute for the year 2004/2005 and Audited Accounts for the year 2003/2004).*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Katibu kwa *agenda* inayofuata naomba niwatambulishe wageni mbalimbali walioko sehemu za *gallery*, kwenye *Speakers Gallery* tunao Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, Mheshimiwa Sepetu na Mheshimiwa Nangali. Pia wageni wengine upande huu wa kulia ni Viongozi wa Chama cha Mapinduzi wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Kusini Unguja wako tisa. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tatu tunao wageni wawili Mwenyekiti wa UWT Iringa na Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana Iringa wamekaa kulia nao pia. Ahsante sana. (*Makofi*)

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 68

### Barabara ya Shekilango

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Kwa kuwa Barabara ya Shekilango – Sinza ni mbovu kwa kipindi kirefu sasa na kwa kuwa Serikali ilikiri kwamba, imetoa kiasi cha shilingi milioni 700 kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo, lakini zikatumiwa visivyo na Manispaa ya Kinondoni.

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kwa watendaji waliohusika na ubadhirifu huo ili iwe fundisho kwa wengine?

(b) Baada ya kutoa muda wa wiki tatu zilizotolewa kwa wahusika kurudisha fedha hizo. Je, ni kiasi gani cha fedha kimesharudishwa?

(c) Kwa kuwa sio wakazi wa Sinza waliofanya ubadhirifu huo. Je, Serikali ina mpango gani na kuendelea na ukarabati wa barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee, Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara ya Shekilango yenye urefu wa kilomita 3.8 ilifanyiwa ukarabati mkubwa mnamo mwaka 1991 chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia na kujengwa kwa kiwango cha lami. Hata hivyo ujenzi huo haukuhusisha ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua na badala yake ilichimbwa tu na kuachwa bila ya kujengwa. Aidha kati ya mwaka 2002 hadi mwaka 2005 barabara hii imekuwa ikifanyiwa matengenezo ya dharura yenye jumla ya shilingi 95 milioni, ambayo matengenezo hayo yalihusisha kuziba mashimo ya viraka vya lami na kufukua mifereji ya maji ya mvua.

Mheshimiwa Spika, baada ya kujitokeza kwa uchakavu mkubwa katika barabara hiyo, upembuzi yakinifu wa kwanza ulifanyika na kuandaa gharama halisi ya ukarabati wa barabara hiyo, kwa kiwango cha lami cha kiasi cha shilingi billion 1.5. Katika mwaka

wa fedha 2004/2005, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi milioni 760 toka Mfuko wa barabara kufanyia matengenezo madogo madogo ya barabara hiyo. Baadaye iliamuliwa ufanyike upembuzi yakinifu kwa barabara nzima ikihusisha mifereji. Aidha usanifu ulifanyika upya mwaka Januari 2006 na gharama halisi ilionekana kwamba ni Sh. 2.3 bilioni. Hivyo hakuna ubadhilifu uliofanyika na fedha hiyo hazikutumika kwa makusudi mengine.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu (a) hapo juu shs. 760 milioni zilizotolewa na Serikali hazikutumika kwa kwa makusudi mengine bali zilihifadhiwa benki. Hivyo hapakuwa na fedha yoyote ya kurejeshwa.

(c) Mheshimiwa Spika, hivi sasa, Serikali imeamua kuitengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami na kutengeneza mifereji ya maji. Baada ya usanifu kufanyika gharama kuonekana kwamba ni sh. bilioni 2,095,420,000/= zabuni ilitangazwa tarehe 23/2/2006 na kufunguliwa tarehe 28/03/2006. Uchambuzi wa kitaalum ulifanyika na kumalizika tarehe 26/04/2006. Uteuzi wa Mkandarasi ulifanyika tarehe 11/05/2006. Muda wa ujenzi utachukua wiki 32 tangu siku ya kusainiwa kwa mkataba huo na ukarabati wa barabara hiyo unategemewa kukamilika mwezi Januari mwaka 2007. Kazi za ujenzi inaendelea na gharama za ujenzi zimechangiwa kama ifuatavyo; Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imekwishatoa shilingi milioni 760 na shs. 900,000,000/= zimetengwa kwa mwaka huu wa 2006/2007. Aidha fedha zilizobakia ambazo ni shilingi shs. 435,420,000/= zitachangwa na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba Serikali ilichukua maamuzi ya haraka pasipo kuangalia utabiri wa hali ya hewa hali iliyopelekea barabara hiyo kuwa mbaya sana sasa hivi:-

(a) Je, Serikali ilishafanya tathmini mpya kuangalia gharama zitakuwa kiasi gani na kama imefanya ni shilingi ngapi?

(b)Hali inaonesha kwamba barabara hiyo itachukua muda mrefu kutengeneza kuliko ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuzishughulikia barabara za ndani *especially* Shekilango kwenda Kijitonyama na Kijitonyama kwenda Mwananyamala ili kurahisishia wasafiri wanaelekea Mjini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu umebaini kwamba gharama halisi ya kutengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami pamoja na mireji ni shilingi bilioni 2.3 na milioni shilingi 760 zimekwishatolewa na Serikali. Sasa hivi ukarabati umeshaanza na unaendelea na tahadhari hiyo imechukuliwa kwamba ikitengenezwa hiyo barabara haitakuwa na matatizo tena kama ilivyokuwa hapo mwanzoni.

Kuhusu swali la pili ni kwamba Serikali itaziangalia hizo barabara ili kuhakikisha kwamba usafiri unakuwa rahisi katika barabara zinazounganisha barabara ya Shekilango. (*Makofi*)

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuweka hela benki wakati inatakiwa kufanya kazi ni kuongeza gharama baada ya muda mrefu kupita na kwa kuwa kufanya hivyo na kutokutengeneza barabara ni uzembe. Je, Waziri anakubali kwamba waliohusika wamefanya uzembe wakati wananchi wanakosa barabara hela inakaa benki na wanastahili kuchukuliwa hatua?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, hakukuwa na uzembe wowote ambao tunaweza tukasema ulijitokeza katika zoezi hili la kujenga barabara ya Shekilango. Kilichotokea ni kwamba shilingi 760 ambazo zilitengwa kwa mara ya kwanza na ninyi nadhani mta-*appreciate* jambo hili zisingeweza kutengeneza barabara ile na kuonyesha *impact* ya namna yoyote ile wakati gharama halisi ni shilingi bilioni 2,300,000,000. Busara ilivyotumika ilikuwa ni kuendelea kuzungumza na Serikali kwa maana ya ofisi yetu kuona kama tunaweza tukapata fedha za ziada ili angalau barabara ile itakapoanza kutengenezwa itengenezwe kwa kiwango ambacho kitawaridhisha Watanzania na ndio maana tumelazimika kuweka sasa fedha hizi zote katika bajeti ya mwaka huu ili mkishazipitisha tunahakika barabara ile itakamilika vizuri sana. Lakini kwa upande mwingine naomba niongezee tu kusema kwamba kuweka fedha benki ni utaratibu wa kawaida wa Kiserikali. Kama kuna gharama ni gharama ni gharama za kawaida ambazo zinaendana na shughuli za kawaida za kibenki, ili mradi nia ilikuwa nzuri yote hayo tunayakubali. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita mwuliza swali kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, nilitaka nitangaze kwa wale ambao pengine walikuwa hawajaelewa hali kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye huwa hakosekani kabisa humu ukumbini hasa kipindi cha maswali yupo Dar es Salaam kikazi kwa mapokezi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya China. Kwa sasa hadi hapo atakaporejea Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali humu Bungeni ni Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib. (*Makofi*)

Na. 69

**Kuboresha Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:

Kwa kuwa, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, katika miaka ya nyuma ilikuwa ikishughulikia majukumu yake kwa vitendo huko vijijini kama vile Elimu ya Afya, Elimu ya Watu Wazima n.k na kwa kuwa, sababu hiyo Wizara ilikuwa na hadhi kubwa na ilikuwa na vitendea kazi kama vile usafiri wa kuwafikia walengwa hao, tofauti na ilivyo sasa ambapo kazi nyingi za Wizara hii zimebaki kwenye madawati/ maofisini tu.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuiboresha Wizara hii irudi katika hadhi yake ilivyokuwa zamani kwa kuiongezea bajeti na kurudisha yale mambo ya msingi yaliyokuwa yakifanywa wakati huo kwa lengo la kufikisha huduma zao kwa wananchi huko vijijini?

(b) Je, Serikali haioni kwamba ipo haja sasa ya kuwawezesha watumishi wa ngazi ya Kata na Wilaya, katika Wizara hiyo kwa kuwapatia vitendea kazi kama usafiri ili waweze kutoa huduma zao kwa walengwa?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa inaajiri watumishi kwenye Wizara hii kulingana na taaluma zinazoendana na majukumu yaliyo chini ya Wizara hiyo ili utendaji wa kazi uwe wa kitaalam na wa mafanikio mazuri kuliko ilivyo sasa ambapo kuna mchanganyiko wa watumishi?

**NAIBU WAZIRI MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge Viti Maalum, lenye vipengele (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Diana Chilolo, kwa kuwa mmoja wa Wabunge watetezi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. (*Makofi*)

(a) Ni kweli kabisa kama alivyobainisha Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, kuwa Wizara hii ina majukumu makubwa katika kuhamasisha na kuchochea maendeleo ya jamii kwa ujumla, lakini pia ina jukumu la kushughulikia masuala ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake, Maendeleo ya Familia, Maendeleo ya Watoto pamoja na kusajili na kuratibu Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Kwa ujumla wake shughuli hizi ni nyingi na kwa umoja waje zina mchango mkubwa sana katika kujenga misingi ya kufikia azma ya maisha bora ka Kila Mtanzania. Serikali kwa kutambua hili imeweza kuongeza Bajeti ya Wizara hii, kutoka mgao wa Shilingi Bilioni 6.1 mwaka 2003/2004 hadi kufikia shilingi bilioni 8.4 mwaka 2005/2006. Wizara kwa upande wake imeshakamilisha zoezi la kuandaa Mpangowa Kimkakati wa Wizara (*Strategic Planning*) inayoonyesha Dira, Malengo na Mikakati ya muda mrefu na mfupi. Mpango huu umekwisha kamilika na unaweka misingi mizuri ya kuwezesha Wizara hii kuongezewa Bajeti yake ili kuwa na ufanisi zaidi.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kuwa Watumishi wengi kuanzia wakufunzi katika vyuo vyetu vya Maendeleo ya Jamii na Wananchi, pamoja na Wataalam wa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri na Kata, hawana vitendea kazi kama vile magari, pikipiki, baiskeli na vifaa vingine, hata hivyo kwa kuwa sasa Wizara imekamilisha Mpango wake wa kimkakati, na kutokana na ahadi ya nyongeza ya Bajeti ya Wizara hii katika mwaka ujao wa fedha, mambo mengi aliyoshauri Mheshimiwa Diana Chilolo yatazingatiwa.

(c) Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa Wizara inaajiri wataalam kulingana na taaluma zinazoendana na majukumu yake, Wizara inaendelea na mpango wa kuziba mapengo kutokana na upungufu wa watumishi wataalam katika idara zake mbalimbali kwa kujaza nafasi hizo chache, kutokana na ufinyu wa bajeti, lakini mwaka

ujao wa fedha tutakuwa na ajira nyingi zaidi ili kupata watalaam wenye upeo wa kwenda na ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. (*Makofi*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Pamoja na majibu mazuri napenda kumuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa bajeti zilizopita Serikali ilijihusisha kidogo sana katika kuhudumia vituo vya watoto waliokuwa wanaishi kwenye mazingira magumu ambavyo vingi vimetelekezwa na wahisani. Je, kupitia bajeti hii Serikali itakuwa imekita kwa asilimia 100 kuhudumia vituo hivyo?

(b) Kwa kuwa wako akina mama wajane wengi nchini ambao wamekosa haki zao za msingi wanapofuatilia mirathi kwa kushindwa kujua sheria. Je, kupitia bajeti hii, Serikali itakuwa imeandaa fungu la kuwasaidia akina mama hawa kuweza kufuatilia mirathi yao kisheria? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Diana Chilolo kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kama ilivyoahidi kupitia Wizara yetu kwamba tunatengeneza Mpango wa Hifadhi ya Jamii, ambao utahusisha watoto wanaoishi katika mazingira magumu Wizara yetu kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, tuko katika hatua ya kubainisha watoto wanaoishi katika mazingira magumu ili basi tuweze tukawa na mkakati mzuri wa kuweza kutoa huduma na kuwasaidia watoto hawa yatima na wale walioko katika mazingira magumu.

(b) Kuhusu msaada wa kisheria ni kweli kabisa kama alivyobainisha Mheshimiwa Mbunge, akina mama wengi wanapata shida sana ya kudai mirathi hasa kwa wale wajane. Lakini hata wale walioko katika ndoa wanapata matatizo makubwa sana kwa kuweza kupata matunzo kwa watoto. Wizara yetu iko katika hatua ya kuweza kuainisha na kuweza kupata fungu na kuweza kupitia bajeti itakayokuja kwa sababu wote tunajua kwamba sungura huyu wa safari hii ni mdogo na amekonda kutokana na ukame. Lakini inshala mwaka ujao tutakuwa na fungu kwa ajili ya msaada wa kisheria kama inavyoainishwa katika MKUKUTA. (*Makofi*)

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto nitegemezi kubwa sana ya kutoa elimu katika vikundi vya akina mama huko vijijini. Katika utaratibu wa nyuma tulikuwa na Maafisa Maendeleo katika Kata zetu na Bahati mbaya wale maafisa maendeleo wa kata walikuwa wanalipwa na Halmashauri ambazo hazina fedha. Je, Sasa Wizara hii haioni umuhimu ili walengwa wanawake wa vijijini kufikiwa elimu ya kutosha au Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Kata wakalipwa na Wizara?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nyawazwa kama ifuatavyo:-

Ni kweli Serikali hapo zamani imekuwa ikiwahudumia na kuwalipa mishahara Maafisa Maendeleo, katika maeneo yetu na walifanya kazi nzuri sana katika kubadilisha maisha ya wananchi. Serikali imeliona hilo na hivi sasa Wizara yetu imepewa jukumu la kuwashughulikia hawa Maafisa Maendeleo katika kata moja kwa moja. Hivi sasa tunaendesha semina na warsha mbali ya kuwahamasisha wajibu wao kikamilifu. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita muuliza swali kwa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, leo tuna baraka ya wageni wengi na ni heshima kuwatambua. Kwanza naomba nimtambue kwenye *Speakers Gallery* Mheshimiwa Asha Abdallah Juma Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto Zanzibar. (*Makofi*)

Pili, tuna ujumbe kutoka Canada, *Doll House University* unaongozwa na Profesa David Weller ambao ni wageni wa Wizara ya Mipango, kutoka Canada wanashirikiana na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezesheji, kuhusu maendeleo ya sekta binafsi hasa wale wananchi wa kawaida wanaojishughulisha kutafuta riziki yao, ndiyo uwezeshaji wenyewe huo. Tunashukuru sana kuwa na wageni hao. (*Makofi*)

Tatu kutoka Kisarawe tunao Waheshimiwa Madiwani wa Kamati ya Fedha wa Halmashauri ya Kisarawe Mheshimiwa Janguo, hakututamkia majina, lakini ni wale pale upande wa kulia. Huo ndiyo mwisho wa wageni kwa sasa.

Na. 70

**Biashara ya Chuma Chakavu**

**MHE. MOHAMED S. SINANI** aliuliza:-

Kwa kuwa biashara ya chuma chakavu inashamiri hapa nchini na kwa kuwa tunashuhudia wizi wa nyaya za umeme, vifuniko vya chemba ya mifereji ya maji ya mvua vilivyopo katika barabara hasa Dar es Salaam:-

Je, kwa nini Serikali isipige marufuku biashara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini, ningependa kuanza kutoa maelezo yafuatayo:-

Ni kweli kwamba biashara ya chuma chakavu imeshamiri hapa nchini. Hii inatokana na kukuwa kwa uelewa wa wananchi kuwa chuma chakavu kinaweza kuuzwa ndani na nje yanchi kwa faida. Hali hii imeleta mgongano wa kati ya wenye viwanda

vinavyoyeyusha chuma na wasafirishaji wa chuma nje ya nchi mpaka kuilazimu Serikali kuchukua hatua mbalimbali za kusimamia biashara hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua migongano inayotokana na mahitaji ya chuma chakavu ndani na nje ya nchi ililazimika kuitisha vikao mbalimbali vya wadau. Vikao hivi vilibainisha namna nzuri ya kuendesha biashara ya chuma chakavu. Aidha, Serikali imefanya utafiti wa kina ili kubaini masuala mbalimbali yanayohusiana na biashara hii. Tunatarajia kutumia matokeo ya utafiti wetu na maoni ya wadau wa ndani katika kuandaa utaratibu wa kudumu wa kusimamia biashara ya chuma chakavu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, wizi wa nyaya za umeme na mifuniko ya mifereji ya maji machafu ni makosa ya jinai kwa wanaouza na wanaonunua vifaa hivyo. Serikali itaendelea kushirikiana na vyombo vya dola ili kudhibiti wizi huo ili hatimaye kuukomesha kabisa. Aidha tunawaomba washirikiane na vyombo vya dola katika kukomesha biashara hii haramu ya vyuma chakavu. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED SAID SINANI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri lakini nina swali moja.

Je, Serikali imejiandaa vipi kukabiliana na gharama za kurudishia tena vifuniko vya maji machafu ambavyo ni lazima vifunikwe haraka kwa sababu vinahatarisha maisha ya watu?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, malipo yote yanayotakiwa kufanyika mpaka tathimini ifanyike. Kwa sasa hivi tathimini haijafanyika na upembuzi yakinifu wa hasara haujafanyika pamoja na fedha zinazotakiwa ili Serikali iweze kujiandaa kukamilisha kurudisha mifuniko hiyo. (*Makofi*)

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa chuma chakavu na vyuma vingine inaonekana vinahitajika sana katika nchi yetu na kwa kuwa katika Wilaya ya Ludewa Mkoa wa Iringa, tunao Mlima wa Chuma yaani Liganga na kwa kuwa Serikali imeelezea katika Ilani kwamba itashughulikia, ningependa kujua Serikali ina kauli gani juu ya mlima huu wa chuma yaani Liganga? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO):** Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango kabambe wa kuendeleza uchimbaji wa chuma cha Liganga kama moja ya miradi mikubwa chini ya utaratibu wa *Mtwara Development Corridor*. Katika mpango huu iko miradi mikubwa yaani *ENCA projects* miwili, moja ni huu wa wa Chuma cha Liganga na wa pili ni wa mkaa wa mawe wa mchuchuma. Kwa hiyo, kama kweli ilivyoandikwa kwenye ilani matarajio yangu ya kwamba katika mpango utakaoanza mwaka 2007/2008 suala la uchimbaji wa makaa ya mawe ya mchuchuma na chuma cha Linganga utawekwa katika mpango. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) Na (b) napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika mchakato wa kuondoa kero katika mfumo wa biashara nchini na ili kuinua sekta ya biashara ndogo na za kati, pamoja na sekta isiyo ramsi kuingia kwenye mfumo wa uchumi rasmi, Serikali imefanya mabadiliko kadhaa katika mfumo na taratibu za utoaji wa leseni za biashara nchini. Mabadiliko haya ambayo yanaratibiwa na kitengo cha kanuni bora *(Better Regulation Unit)* na Wizara yangu chini ya Programu ya Kuimarisha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA/BEST), bado yanaendelea ili kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa shindani katika soko ili tuweze kukuza uchumi wetu.

Baada ya maelezo hayo, naomba sasa nimjibu Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimikwa Spika, Serikali imefanya mabadiliko kadhaa katika mfumo na taratibu za utoaji wa leseni za biashara nchini kwa mujibu wa Sheria Na. 25 ya 1972.

Marekebisho hayo yalihusu ada za leseni za biashara ambapo biashara zenye mauzo yasiyofikia shilingi milioni 20 kwa mwaka hazitozwi ada. Aidha, kwa mauzo yanayofikia shilingi milioni 20 kwa mwaka ada ni shilingi 20,000/= tu.

Mheshimiwa Spika, Sheria Na. 28 ya Vileo ya mwaka 1968 haihusiki na mabadiliko haya. Kwa hiyo, ada za leseni za vileo zinatozwa na Halmashauri mbalimbali nchini kwa bidhaa za vileo zenye mauzo chini ya shilingi milioni 20.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubali kuwepo kwa mgongano wa baadhi ya Sheria zinazosimamia biashara mbalimbali nchini, ili kuondoa migogoro hiyo, Wizara yangu imekwishaanza kazi ya kuainisha na kuchambua sheria mbalimbali zenye migongano kwa lengo la kuziondoa ama kuzirekebisha. Kazi hii inafanyika kwa kushirikisha wadau mbalimbali zikiwemo Wizara, Idara na Jumuiya za wafanyabiashara.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa. Hata hivyo, naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Sheria nyingi za Halmashauri, Sheria ndogo ndogo zilipitishwa kabla ya mabadiliko haya ya sheria hii ya Kodi ya Mapato na kwa sababu hiyo yamechangia sana kuleta mgongano katika utekelezaji wa sheria mama. Je, ni lini kazi hiyo ya uainishaji wa Sheria hizo utakamilika ili kuondoa matatizo haya yanayojitokeza?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Sheria zinazotungwa na Bunge ni sheria mama na si vema sheria hizi zikatenguliwa na Sheria ndogo ndogo za Halmashauri. Je, kuna utaratibu gani wa kuhakikisha jambo hili halitokei hapo baadaye?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, lipo Shirika moja linaitwa *BANOC* ambalo limeshirikiana na *Law Firm* ya Tanzania na limefanya utafiti likagundua kwamba kuna sheria 63 ambazo zinaingiliana katika biashara. Zinaingiliana katika kupata leseni za biashara. Shirika hili linasaidiana na *Better Regulation* pamoja na *Best* au MKUMBITA katika kuzitambua na kuzirekebisha hizo Sheria.

Kwa mfano, Sheria ya 18 ya mwaka 1975 inasema kwamba mfanya biashara anayetoka nje hawezi akafanya biashara hapa nchini au akapata leseni hapa nchini kama hana *residence permit* kibali cha kukaa hapa nchini. Lakini Sheria ya mwaka 1972 Na. 25 inasema kwamba mtu hawezi akapata leseni kama hana *residence permit* kwa hiyo kuna migongano ya sheria. Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba sasa hivi tunafanya kazi ya kuzitambua kwanza halafu baadaye tunafanya ile shughuli ya kuzibadilisha, ili ziweze kuwa *hamonized* sheria moja isiponze sheria nyingine. Kwa hiyo, kazi hiyo inafanyika sasa hivi.

La pili, hilo tutalizingatia Mheshimiwa Mbunge.

Na. 72

**Upatikanaji wa Vyeti vya Kuzaliwa**

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY** aliuliza:-

Kwa kuwa utaratibu wa kupata vyeti vya kuzaliwa *Birth Certificate* una usumbufu mkubwa hivi sasa:-

Je, Serikali haioni haja ya kuandaa utaratibu wa kupata vyeti hivyo katika zahanati ambazo watoto hao wanazaliwa?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, kama ifuatavyo:-

Utaratibu wa usajili na utoaji wa vyetu vya kuzaliwa umeelekezwa chini ya Sheria ya Uandikishaji Vizazi na Vifo, *(The Births and Deaths Registration Act, Cap. 108).* Kwa mujibu wa sheria hii, usajili na utoaji wa vyeti unafanyika katika ngazi mbili ambazo ni Makao Makuu ya Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu na vile vile, Wilayani alipo Msajili wa Vizazi na Vifo. Msajili wa Vizazi na Vifo wa Wilaya ndiye mwenye

dhamana ya kusajili vizazi na vifo vinatokea katika Wilaya yake. Wanaposajili hutoa vyeti pale pale.

Kwa kuzingatia umbali kutoka Makao Makuu ya Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu na vile vile Makao Makuu ya Wilaya na maeneo ya Miji midogo, tarafa na vijiji wanapoishi wananchi wengi, ni kweli kwamba upo usumbufu wanaoupata wananchi katika kupata vyeti hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua usumbufu huo, Serikali imechukua hatua mbalimbali ili kusogeza huduma ya Usajili wa vizazi na vifo karibu na maeneo wanayoishi wananchi. Kwa sasa, vizazi na vifo vinavyotokea nyumbani, vinasajiliwa katika zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali na Ofisi za Watendaji wa Kata. Hata hivyo, vyeti havitolewi pale pale, badala yake, wahusika sharti wafuate vyeti Makao Makuu ya Wilaya kwa kuwa ndipo alipo Msajili wa vizazi na vifo wa Wilaya. Hatua nyingine ni kufanya marekebisho ya sheria ya Uandikishaji vizazi na vifo ili uandikishaji wa mtoto wa miaka 10 na zaidi sasa ufanyike kwa wepesi bila kuathiri usalama wa nyaraka hizo.

Mheshimiwa Spika, siku zote lengo la Serikali ni kuwaondolea kero wananchi kwa kuwapatia huduma muhimu. Moja ya mikakati ya Ofisi ya Kabidhi Wasii ni kurahisha zaidi huduma za Usajili wa Vizazi na Vifo na upatikanaji wav yeti hivyo kwa kuanzisha huduma maalumu ya *Mobile Service* ambayo itawafikia wananchi hadi mlangoni. Mkakati huu utaanza kutekelezwa hivi karibuni hasa baada ya Ofisi ya Kabidhi Wasii kuwa Wakala wa Serikali pamoja na hatua hii Serikali inafanya utafiti sasa kuhusu uwezekano wa kuwapatia Makatibu Watendaji wa Tarafa na Watendaji wa Kata mamlaka ya kusajili na kutoa vyeti.

Mara baada ya utafiti huu kukamilika Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Uandikishaji wa Vizazi na Vifo utawasilishwa katika Bunge lako Tukufu na ni matumaini yangu kuwa hatua hizo zitaondoa usumbufu kuhusu upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa.

**MHE. AZIZA S. ALlY:** Nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Kwa kuwa Serikali imeshaona kuwa kuna usumbufu mkubwa wa wananchi kuweza kupata vyeti vyao vya kuzaliwa na Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri na kusema Sheria hiyo italetwa hapa Bungeni ili tuweze kuibadilisha. Je, anaeleza nini wale wananchi ambao bado hawajapata vyeti vyao vya kuzaliwa mpaka hivi sasa na kwa kuwa kuna utaratibu wa kuandaa vyeti vya uraia, haoni kuwa utakuwa ni usumbufu mkubwa ili kuweza kuandaa vyeti vya uraia wakati wananchi wengi hawana tayari vyeti vyao vya kuzaliwa?

Pili, kutakuwa na utaratibu gani wa kuweza kuwapatia wale wananchi ambao wako vijijini kabisa ambao hata hivi vyeti hawavifahamu kabisa vyeti vya kuzaliwa hususan wale wananchi wa Urambo, Nzega, Sikonge, Uyui, Igunga na Tabora Mjini?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa umakini wake wa kufuatilia mambo haya hasa yanayowagusa wananchi wa vijijini kule Urambo na kwingineko.

Pili, napenda nimhakikishie kwamba utaratibu uliowekwa hivi sasa ni wananchi kuvifuata vyeti hivi katika Wilaya. Lakini tunasema mipango yetu ni kuhakikisha kwamba tunawafikia hata wale wa Urambo mlangoni pao tukisha-*establish Mobile Service*. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge tushirikiane pamoja na tusubiri kidogo tu tutafika Urambo na *mobile service* yetu tutawaandikisha ndugu wa pele.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**: Mheshimiwa Spika, naomba kupitia Bunge lako Tukufu kuwakumbusha wazazi na wananchi kwa ujumla umuhimu wa kuwachukulia watoto wao vyeti kwa sababu bila vyeti hivyo watakuwa wananyima haki zao nyingi sana. Na kwa upande wa Serikali tutaangalia mapema namna ya kurekebisha Sheria lakini nina hakika sasa Ofisi ya Kabidhi Wasii baada ya kuwa Wakala wa Serikali mambo yatakuwa yanaenda kwa kasi mpya.

Na. 73

**Sheria ya *Affiliation***

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, miaka ya nyuma Bunge lilipitisha sheria inayoitwa *Affiliation Ordinance* ambayo inatamka mwanaume anayempa mamba mwanamke ambaye si mkewe, na hasa mwanafunzi ana ulazima wa kumtunza mtoto na mama yake:-

(a) Je, Sheria hiyo ingali inatumika?

(b) Je, mpaka sasa ni ni wastani wa wanaume wangapi wamehukumiwa chini ya sheria hiyo?

(c) Je, Serikali imeona matatizo gani katika utekelezaji wa sheria hii mabayo yanaweza kurekebishwa na Bunge?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA N A SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Viti Maalum, napenda kutoa maelezo ya ujumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sheria ya ushirikishaji katika matunzo *(The Affiliation Act, Cap. 278)* ilitungwa mwaka 1949, ili kuwawezesha wanawake kudai matunzo wakati wa ujauzito na matunzo ya watoto. Kwa mara ya mwisho Sheria hii ilifanyiwa marekebisho mwaka 1964 kupitia Sheria Na. 4 ya mwaka huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Wanawake, Jinsia na Watoto imeona matatizo kadhaa katika sheria hii. Kutokana na matatizo hayo, Serikali iliunda Kamati Maalum ya wataalam ili kuipitia. Kamati imeshatoa mapendekezo Serikalini kwa ajili ya kuyafanyia kazi. Mchakato wa

kuyafanyia kazi mapendekezo hayo utakapokamilika, Serikali itaandaa Muswada wa Sheria ya Watoto na kuuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu. Sheria hiyo itaweka masharti kadhaa ikiwa ni pamoja na haki, ushirikishaji katika matunzo na uasili wa watoto.

Mheshimiwa Spika, baaada ya maelezo hayo ya jumla sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Mchemba, kama ifuatavyo:-

(a) Sheria ya ushirikishaji katika matunzo bado inatumika hapa nchini.

(b) Si rahisi kufahamu ni wastani wa wanaume wangapi wamehukumiwa chini ya sheria hii. Kumbukumbu na takwimu za mashauri yanayoamuliwa Mahakamani haziwekwi katika misingi ya sheria moja moja. Kinachoonyeshwa katika kumbukumbu hizo ni mashauri mangapi yamefunguliwa na mangapi yameamuliwa.

(c) Tatizo kubwa ambalo Serikali imeliona katika utekelezaji wa sheria hii ni kiwango kidogo cha sh.100/= kwa mwezi kilichowekwa na sheria hii. Wanawake wengi hawahamasiki kuanzisha madai chini ya sheria hii kwa sababu kiwango hiki cha fedha hakitoshi kwa matunzo ya mtoto au mama mjazito.

Mheshimiwa Spika, matatizo haya yatakwisha pale Serikali itakapowasilisha katika Bunge lako tukufu, Muswada wa Sheria ya Watoto ambao utaweka masharti kama nilivyokwishaeleza na pia Sheria ya Sheria inayoitwa *Currency Points* ambayo itaweka utaratibu endelevu wa kubadili viwango vya adhabu ya faini na malipo mengine kulingana na mabadiliko ya thamani ya fedha yetu.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa wasichana hupewa mimba na kwa kuwa wanaume wengi hukataa kuwalea hawa wasichana, yaani kulea hao watoto. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuleta Sheria hiyo haraka sana ili kukidhi haja hii, Sheria hiyo haraka sana ili iweze kukidhi haja hii na kuepukana na tabia ya wasichana kutupa watoto hovyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**: Mheshimiwa Spika, Serikali kama nilivyokwishaeleza katika jibu langu la msingi imeandika *White Paper* kuhusu sheria hii ya watoto na mara tutakapopata matokeo ya *White Paper* tutaleta Muswada hapa Bungeni ambao utawabana hao ambao Mheshimiwa Mbunge anasema wanakimbia majukumu yao ya kutunza watoto waliowazaa wenyewe. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sheria hii ndiyo imesababisha watoto wengi kuzagaa mitaani kwa vile shilingi 100 hazimtoshi mama kumtunza huyo mtoto. Haingekuwa sasa vizuri kwa Serikali kabla haijaleta Sheria hii sasa kufidia matunzo ya hawa watoto mpaka hii Sheria mpya itakapoletwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**: Mheshimiwa Spika, sio busara kwa sasa kuanza kufidia kitu ambacho bado hakijadaiwa. Hizi ni kesi za madai. Sasa sijui tunamfidia nani, tunamfidia kiasi gani. Nafikiri kwa sasa si busara kwa Serikali hata kulifikiria jambo hilo. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**: Mheshimiwa Spika, naomba kuongezea juu ya majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria. Shilingi 100 haitoshi katika malezi ya watoto na haitoshi hata kununua maziwa ya siku moja.

Kwa hivyo, Serikali inatambua umuhimu wa kuleta marekebisho ya Sheria hii pamoja na ile ya kufanya faini ziwe zinaongezeka kadri wakati unavyopita.

Mheshimiwa Spika, lakini wazazi wawajibike bila hata sheria kwa sababu ninajua wengi ambao wanatambua wajibu wa kulea watoto wao. Kwa hiyo, naomba wakati tukiirekebisha hii sheria wote ambao wanajua kwamba wana watoto nje ya ndoa wawajike kwa sababu hakuna mtoto anayezaliwa bila baba na mama. (*Makofi)*

**MHE. YAHYA KASSIM MUSSA:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, muda mrefu sana kuhusiana na swali hili nasimama. Kwa kuwa sheria hii mara nyingi inawaandama watoto wa kiume na kwa kuwa mtoto wakati anatiwa mimba wamekubaliana ya mtoto wa kike na kiume. Je huoni kwamba sasa umefika wakati muafaka kubadilisha sheria hawa wote kuwa na makosa na kuhukumiwa sawasawa? *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kama ilivyo na mvuto basi na Serikali inaona wajibu kwa kweli wa kuleta sheria haraka sana kwa mabadiliko yanayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, suala lililo mbele yetu ni kumwonea mmoja ya wazazi kuangalia watoto na mwingine kutowajika ndiyo swali ambalo liko mbele yetu. Na mimi nasisitiza wajibu wa wazazi wote wawili kuona umuhimu wa kulea watoto kwa namna ambayo inategemewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza si maadii ya kitaifa kufanya hivyo. Lakini inapotokea si kosa la mtoto kwa hiyo, mtoto lazima aangaliwe na wazazi wote wawili.

Na. 74

**Madini ya *Uranium***

**MHE. OMAR ALI MZEE** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi za viwanda duniani kama vile Marekani, Ujerumani, Ufaransa na nyingine hutumia madini ya Uranium kutengeneza silaha za maangamizi na kwa kuzalisha umeme na kwa kuwa utafiti uliofanywa na *Tanzania Commission for Science and Technology (COSTECH)* umeonyesha kuwepo kwa nishati hiyo Tanzania:-

Je, Serikali ina mpango gani kuhusu nishati hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mbunge wa Kiwani, naomba nitoe maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba utafiti wa kijiolojia uliofanywa miaka ya 1979 hadi mwaka 1982 ulionyesha uwezekano wa kuwepo kwa mashapo yenye madini ya *uranium* yanayoweza kuchimbwa kibiashara katika baadhi ya maeneo hapa nchini. Maeneo hayo ni pamoja na Bahi Mkoani Dodoma, Madaba katika Hifadhi ya Selous, Mkuju Mkoani Ruvuma na Galappo Mkoani Arusha.

Mheshimiwa Spika, utafiti huu ulifanywa na Kampuni ya Uranerzberghau GmbH ya Ujerumani ikisimamiwa na *Geological Survey of Tanzania (GST)* iliyoko hapa Dodoma. Kutokana na kuporomoka kwa bei ya madini ya *uranium* wakati huo, utafiti huu ulisitishwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya awali, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhamasisha wawekezaji wanaopenda kuja kuwekeza katika utafutaji na uchimbaji wa madini hapa nchini yakiwemo madini ya *uranium* ili kukuza uchumi wa Taifa letu. Tayari zimeshatolewa leseni kwenye maeneo yanayofahamika kuwa na madini ya *uranium* na shughuli za utafutaji zinaendelea. Iwapo matokeo ya utafutaji wa madini ya *uranium* utakuwa na mafanikio msisitizo wa Serikali ni kwamba madini ya *uranium* yatakayozalishwa hapa nchini na kutumika hapa nchini au kuuzwa nje ya nchi yatumike kuzalisha umeme na si kutengeneza silaha ya maangamizi.Mpango wa Taifa wa Nishati *(Energy Master Plan)* unaendelea kufanyiwa tathmini ili kubaini na kushirikisha vyanzo vya aina mbalimbali vya nishati vilivyopo hapa nchini.

Aidha, mkazo unatiliwa kwenye kuondokana na utegemezi wa nishati itokanayo na maji ambayo umeonyesha kuwa na matatizo. Hata hivyo, utafutaji wa madini ya *uranium* bado uko katika hatua za awali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na teknolojia ya nyuklia kuwa ngumu lakini suala kubwa linalokwamisha matumizi ya nishati hiyo hapa nchini ni kuwa matumizi yetu ya umeme bado ni madogo. Uzoefu unaonyesha kuwa mtambo mmoja wa kuzalisha umeme kwa kutumia vyukilia unaanzia na uwezo wa uzalishaji wa MW 500. Kwa nchi kama Tanzania kuweka mtambo wa namna hiyo kiutaalam haishauriwi kwani matumizi yetu bado ni madogo kwani mahitaji yetu *(peak demand)* hayajafika MW 1000.

Vile vile, mitambo ya nyukilia ina mwisho wake *(life time)*, hili likiwa ni tatizo kubwa linalozikabili nchi zinazotumia nyuklia pamoja na namna ya kutupa masalio

*(Waste Disposal Management)* baada ya muda wake kuisha. Suala hilo limeleta matatizo kiasi kwamba baadhi ya nchi sasa zinaondokana na teknolojia hiyo.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwa sababu inaeleweka wazi kwamba nishati hii ni muhimu na nishati ambayo ina nguvu kuliko zote. Na kwa bahati nzuri tunayo hapa nchini na sasa hivi mataifa mengi yanaendeleza kutengeneza nishati hiyo kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Je, Serikali haioni ya kwamba hiyo itakuwa ni tatizo ni kutatua tatizo la kudumu yaani kutatua tatizo la nishati ambalo linatukabili kwa sasa hivi kama tukiendeleza kutengeneza hiyo nishati hapa nchini kwa manufaa yetu na wataalam ambao wameshaisomea hapa nchini wapo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi Serikali inatafuta nishati mbadala ili tuondokane na matumizi ya nishati kutokana na vyianzo vya umeme. Lakini nilivyoeleza vyanzo vya maji, samahani. Lakini nilivyoeleza kwa kiwango cha matumizi ya umeme hapa nchini matumizi ya umeme kutokana na mitambo ya nyuklia muda huu bado sio muafaka.

Tathmini bado inafanyika. Serikali bado inaangalia na pale tutakapoona kwamba matumizi ya nyuklia kutokana na uwezo wetu wa kutumia, uwezo wetu wa kugharamia na uwezo wetu wa kutunza mitambo hii hapa nchini Serikali itaangalia.

**MHE. ALLY MNYAA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa *uranium* ni madini ghali kuliko madini yoyote duniani na kwa kuwa inaonekana asilimia 30 ya *uranium* inaweza kupatikana Tanzania kuliko nchi nyingi sana za Afrika na kwa kuwa wenzetu wa Malawi hivi sasa tayari wanafanya upembuzi yakinifu kwa kutumia kampuni ya *Paladin Resorces* ya Australia na kuwa nishati hii si lazima huwa tunahitaji kuwa na umeme wa kutosheleza hapa nchini petu.

Hivi sasa kuna mpango wa *Interconnector* baina ya Tanzania – Arusha na Nairobi. Kuna mpango wa *Interconnector* Tanzania na Zambia hata kama tutazalisha umeme zaidi tunaweza kuuza nchi nyingine. Kwa nini Tanzania haijaonyeshwa katika mpango wa maendeleo mpaka sasa hivi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI (k.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa majibu ambayo ametoa hapa. *(Makofi)*

Suala la nishati ni suala kubwa na kama nilivyolielezea kwenye hotuba ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2005 hapa Bungeni tumeeleza mambo mengi ambayo tutayafanya. Suala la kupanga ni kuchagua. Kwa hiyo, tumesema hivi, kama tutakumbuka vizuri. Kwamba tutatilia mkazo suala la kupata nishati kutokana na chanzo cha maji.

Pili, tutaweka mkazo kutokana na chanzo cha gesi na tatu tutaweka mkazo kutokana na chanzo cha mkaa wa mawe na makaa ya mawe yako tena mengi. Kwanza,

Kiwira tutaongeza mpaka kufikia MW 200. Lakini vile vile mpango wa nishati kwa ajili ya kutokana na mkaa wa mawe Mchuchuma utafikia MW 400.

Kwa hiyo, kadri tunavyoendelea ku-*build capacity* ya kuzalisha nishati basi tutaweza kutafuta njia nyingine mbadala moja wapo ni hiyo ya kutumia *uranium.* Lakini kwa sasa uwezo wa Taifa haupo wa kutosha ili kufanya upembuzi katika eneo la kutumia nishati inayotokana na *uranium.*

Na. 75

**Mradi wa Umeme Ntaba na Ipinda**

**MHE. DR. HARRISSON G. MWAKYEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 2002 Serikali kupitia Wizara yenye dhamana ya Nishati ilianza utekelezaji wa mradi wa umeme unaounganisha miji midogo ya Ntaba (Wilayani Rungwe) na Ipinda (Wilayani Kyela) kwa kuweka nguzo zote zinazohitajika. Baadhi ya vikombe na waya kwa kilomita zipatazo tatu hivi na kwa kuwa njia hiyo ya umeme, mbali na kusaidia kusukuma maendeleo katika maeneo hayo itakuwa njia mbadala inayounganisaha mfumo wa umeme wa wilaya hizo mbili:-

(a) Je, ni sababu zipi zilizopelekea mradi huo kusimama kwa zaidi ya miaka miwili?

(b) Je, wananchi wa Kyela na Rungwe ambao waliupokea mradi huu kwa nderemo na vifijo kiasi cha kuruhusu maeneo ya kupitisha umeme bila fidia, wategemee kukamilishwa kwa mradi huo lini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Harrisson George Mwakyembe, Mbunge wa Kyela, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa mradi ulisimama kwa zaidi ya miaka miwili kutokana na ukosefu wa fedha za kununulia vifaa. Gharama za mradi wa kupeleka umeme katika miji midogo ya Ntaba Wilayani Rungwe na Ipinda Wilayani Kyela inayohusisha kujenga laini ya msongo wa KV 33 yenye urefu wa kilometa tano (5) zinakadiriwa kufikia shilingi milioni 24.5.

Usimikaji wa nguzo umekamilika kwa asilimia 85 na ufungaji wa vikombe umekamilika kwa asilimia 80. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa *TANESCO* watakamilisha mradi huo kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Na. 76

**Utekelezaji wa Ibara ya 13(6)(e) na 14 ya Katiba ya Nchi**

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Katiba ya nchi, ibara ya 13(b) na ile ya 14 imepiga marufuku mtu yeyote kuteswa kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu za kumdhalilisha mtu na kwamba kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata hifadhi ya maisha yake kutoka katika jamii kwa mujibu wa sheria.

(a) Je, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita kumetokea matukio mangapi askari kutumia nguvu na kusababisha vifo?

(b) Je, ni raia wangapi wameuawa na askari katika kipindi hicho na ni kutoka maeneo gani?

(c) Je, ni askari wangapi wamechukuliwa hatua na kama bado hawajachukuliwa hatua ni kwa nini?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, naomba kumjibu Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka 5 iliyopita kuanzia mwaka 2001 – 2005 jumla ya matukio 14 ya askari yalisababisha vifo yaliyoripotiwa. Kati ya hayo matukio 8 ni kwa upande wa Tanzania Bara na matukio 6 kwa Tanzania Zanzibar.

(b) Mheshimiwa Spika, raia waliouawa katika kipindi hicho ni 11 kwa Tanzania Bara na 23 kwa Tanzania Zanzibar, akiwemo askari 1. Matukio hayo yalitokea kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| Mbeya | 1 |
| Kilimanjaro | 3 |
| Mwanza | 2 |
| Dar es Salaam | 5 |
| Zanzibar | 23 |
| **Jumla** | **34** |

(c) Mheshimiwa Spika, kwa Tanzania Bara askari waliohusika kwenye matukio hayo ni 19. Askari hao walifikishwa Mahakamani kwa makosa ya mauaji yasiyokuwa ya kukusudia. Kesi zao zinaendelea Mahakamani na zipo katika hatua mbalimbali. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar hakuna askari aliyechukuliwa hatua kwa sababu suala la

lraia na askari waliofariki, lilipata ufumbuzi wa kisiasa kupitia makubaliano ya muafaka. Aidha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliyafunga majalada yote kwa *NOLE PROCEQUE* tarehe 9 Mei, 2002.

**MHE. RIZIKI OMARI JUMA:** Mheshimiwa Spika, asante naomba nimshukuru mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini naomba niulize swali moja la nyongeza; Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu nia ya Rais aliyepita ilikuwa ni kuwapa angalau kifuta machozi wale ambao wameathirika.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini watapatiwa hawa angalau kifuta machozi wale ambao wameathirika hasa ukizingatia nia ya Mheshimiwa Rais wetu ambaye tunaye sasa hivi nia yake ya kujenga umoja na mshikamo na upendo katika kuimarisha muungano?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Riziki kwa kutukumbushia suala hili, napenda kumhakikishia kwamba Serikali italifuatilia kwa kina tunawasiliana na Waziri husika zingine ili kupata ufumbuzi muafaka wa jambo hili.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, baada ya jibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja dogo la nyongeza, kwa kuwa roho ni roho lakini swali lililoulizwa hapa Bungeni, linajielekeza kuuwawa raia tu.

Sasa Je, baada ya jawabu zuri la Mheshimiwa Naibu Waziri, huko Zanzibar yaani Ugunja na Pemba hakuna askari waliouwawa kikatili na kwa sababu zipi?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli wako askari waliouwawa kikatili akiwemo askari wa polisi mmoja na askari mmoja wa JKU na askari mmoja wa KVZ, kwa hiyo jumla ni askari watatu waliouliwa kikatili, na wao tutawafikiria kama watakavyofikiriwa wenzao.

**SPIKA:** Waheshimiwa kulingana na muda tungekuwa tunasitisha shughuli kipindi hiki cha maswali lakini tulikuwa na matangazo mengimengi kwa hiyo tutaendelea ili tumalize swali linalofuata Wizara hiyo hiyo ya Usalama wa Raia Mheshimiwa Nyami.

Na. 77

**Kuongezeka kwa Ujambazi Eneo la Ziwa Tanganyika**

**MHE. PANSIANO D. NYAMI** aliuliza:-

Kwa kuwa, ujambazi wa kupora mali za wananchi na hata kuuwa unazidi kuongezeka kwenye eneo la Ziwa Tanganyika. Hasa katika maeneo ya Kata za Kabwe, Kirando, Ninde, Wampembe na Kate Wilayani Nkasi na Karema Wilayani Mpanda:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani hasa wa kuongeza Askari pamoja na kutenga maeneo zaidi kwa ajili ya vituo kulivyo ilivyo sasa;

(b) Je, kwa nini Serikali isiongeze vyombo vya usafiri kwa askari wanaolinda maeneo hayo ili kurahisisha mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA NA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nyami, Mbunge wa Nkasi lenye sehemu (a) (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba kuna matukio ya ujambazi wa kutumia silaha na kupora mali za wananchi katika mwambao wa Ziwa Tanganyika. Kwa kutambua tatizo hilo Serikali ina mpango wa kuongeza Askari katika Vituo vya Mwambao wa Ziwa Tanganyika yakiwemo baadhi ya maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Maeneo ambayo yataongezewa Askari ni kama ifuatavyo:- Kituo cha Polisi Wanamaji Kipili; Kituo cha Polisi Kirando, Kituo cha Polisi Kabwe, Kituo cha Polisi Namasi, Kituo cha Polisi Kerema, Mheshimiwa Spika, pamoja na kongeza askari katika vituo hivyo Serikali pia imefungua kituo kipya cha Polisi Ikova.

(b) Mheshimiwa Spika, katika mpango wake wa muda mrefu Serikali inakusudia kununua mashua moja mpya ya doria. Aidha, vifaa vingine kama magari, pikipiki na Radio za mawasiliano vitaendelea kununuliwa kwa awamu kadiri Bajeti ya Serikali itakavyo ruhusu.

Mheshimiwa Spika, moja ya hatua ambazo tumeziandaa chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kuanzishwa kwa Operesheni Maalum ya kuwasaka majambazi, wahamiaji haramu na kukamata silaha zinazoingia nchini kwa njia ambazo sio halali katika mipaka yetu na nchi jiran. Utekelezaji wa hatua hii umevishirikisha vyombo vya usalama nchini.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, napenda kuwahakikisha wananchi wote kwamba Serikali inajali usalama wao na mali zao hivyo Serikali itachukua kila jitihada kuhakikisha inapambana na aina zote za uhalifu hapa nchini.

**MHE. PANSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nauliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa, marine boti ya polisi ilipelekwa Kigoma miaka minne iliyopita iliifanye kazi ya doria hadi Mkoa wa Rukwa, lakini mpaka sasa haijafanya kazi hiyo na hata pale wananchi walipojitahidi kuchangia mafuta bado haikufanya kazi, hiyo.

Je, tatizo nini na kwanini hilo boti lisikabidhiwe kwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania ambao wanafanya kazi nzuri sana katika eneo hilo la mpaka?

La pili kwa kuwa hata pale polisi wanapopelekwa vijiji vya mwambao wa Tanganyika, huwa wanazidiwa na hao majambazi na ujuzi pamoja na silaha na hao majambazi, je tatizo ni hasa ni mafunzo, vifaa, ofisi zisizokidhi haja au ni nini?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA NA RAIA**: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Nyami napenda ni kuhakikishie kwamba boti zilizoko huko sasa hivi zinafanyiwa kila jitihada kuhakikisha kwamba zinatengenezwa ili ziweze kufanya kazi yake. Zinatatizo dogo la kiutaalam lakini takuhakikisha kwamba boti ifanyiwa ukarabati wa kutosha ili iweze kutoa huduma ipasavyo kule.

Nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Nyami kwamba Jeshi la Polisi linauwezo mkubwa wa kukabiliana na matatizo ya uharifu nchini bila kusaidiwa na jeshi la wananchi wa Tanzania, kwa sababu kila mmoja anamipaka yake katika kufanya kazi.

Jibu (b) askari wetu wanautaalam wa kutosha wa kukabiliana na waharifu, hivi sasa hatua zinazochukua, nikuongeza askari katika maeneo hayo ili kuhakikisha usalama wa raia katika eneo hilo uko salama.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha, yapo matangazo hapa Mwenyekiti, wa Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Tanga, anaomba Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa huo wa Tanga wakutane mara baada ya kipindi cha maswali katika jengo la utawala pale karibu na pale kwenye visanduku vya barua vya Waheshimiwa Wabunge, Wabunge. Wabunge wa Mkoa wa Tanga kukutana mara baada ya kipindi cha maswali katika ukumbi wa zamani, karibu na eneo la visanduku vya barua za Wabunge.

Mwenyekiti wa Kamati za Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Msindai, anawaomba wajumbe wa Kamati yake hiyo ya LAAC yaani hesabu za Serikali za mitaa kuwa leo saa tano asubuhi watakuwa na kikao kitakachofanyika katika ukumbi namba 227 Jengo la Utawala ghorofa ya pili, kujadili majukumu ya Kamati yao yatakavyotekelezwa, mkutano muhimu wa kupanga ratiba yao. Wajumbe wote wa LAAC saa tano asubuhi chumba na 227.

Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Utendaji ya Amani *Forum*, wanaombwa kukutana hivi leo mchana saa saba chuma namba 219, Kamati ya Utendaji Amani *Forum* Wajumbe Waheshimiwa Wabunge wote ambao ni wajumbe wa Kamati ya utendaji mkutano ni saa saba mchana ghorofa ya pili chumba namba 219.

Waheshimiwa kwa hoja hizi za Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Mipango bado ninao wachangiaji 27, lakini hali halisi ni kwamba watakoweza kupata nafasi ni wachangiaji wanne au sana sana tukibahatika watano kwa asubuhi hii, na hapo itakuwa ni mwisho, kwa sababu gani kulingana na ratiba yetu Serikali itaanza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge za wiki nzima hii saa tano asubuhi Naibu Mawaziri watatu wataongea saa tano hadi saa sita, baada ya hapo Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji atajibu hoja saa sita hadi saba.

Tutasitisha shughuli tutakaporejea saa kumi na moja kama ilivyoutaratibu wetu na utamaduni wetu, Mheshimiwa Waziri wa Fedha atajibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa muda wa saa moja kuanzia saa kumi na moja, hadi saa kumi na mbili, baada ya hapo sasa kama mnavyofahamu kwa kupitisha hoja ya Waziri wa Fedha na pia hiyo ya Mipango inabidi sasa ipigwe kura kwa mujibu wa kanuni zetu, kura hizo ni jina kwa jina yaani *roll call vote* kila Mbunge, kila Mheshimiwa Mbunge ataitwa kwa jina na aseme kama anaunga mkono ama haungi mkono ama amekaa katikati tu.

Kwa hiyo, kwa utaratibu huu nasikitika kwamba kiasi cha Waheshimiwa Wabunge 23 hawatapa nafasi, lakini napenda niwahakikishie kwamba nitawapa kipaumbele kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu watapewa kipaumbele, na pia kipaumbele katika hoja za Wizara zozote watakazochagua kuchangia asante.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2005, Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2006/2007 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2006/2007

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. SAMEER I. LOTTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupewa nafasi hii kabla sijaanza na rafiki yangu pale Morogoro ni Mwenyeji wa Mkoa wa Kilimanjaro, yeye akifika kwenye baraza letu pale anasalimia kwa kusema salaam alekum kwa mpigo. Sasa na mimi nitasema hongera wanaostahili kupewa pongezi kwa mpigo. Isipokuwa ndugu salaam muhimu sana kwa wana jimbo langu la Morogoro Kusini Mashariki…

**SPIKA:** Samahani utaratibu tu, Mheshimiwa Waziri Pinda amepita katikati ya Spika, na msemaji, naomba jamani tufuate kanuni, asante unaweza kuendelea.

Mheshimiwa Spika, watu wa Morogoro Kusini wamenichagua kwa kunipa kura asilimia 85, mizengwe ilifanywa, ngazi ya Kata, ngazi ya Wilaya lakini wananchi wakasema wanataka kunichagua na wamenichagua nashukuru sana. Mgombea wa Urais alikuja pamoja na vikwazo vilifanywa pia asifike lakini akafika na kwa kweli jitihada zake, kampeni ilinisaidia katika kuongoza kura zangu, nashukuru kwa hilo pia.

Katika bajeti nitaongolea masuala mawili matatu haraka haraka, fedha zimetengwa kwa ajili ya mipaka ya vijiji hiyo ni jambo jema na ni vizuri sana hizi zikitumika ipasavyo, vijiji vyetu vitaweza kupanga mambo yake kwa uhakika zaidi na ninaamini katika bajeti zingine katika kipindi hiki basi tuweze kuweka fedha kwa ajili ya mipaka ya vitongoji pia. Maeneo kuna fedha zimepangwa kwa ajili ya wafugaji na wakulima kutenga maeneo ya wafugaji na wakulima, hili ni nyeti sana na katika hili juzi sio pesa tu maana yake kuna uwajibikaji pia unahitaji. Juzi mgombea wa urais huyo huyo alipokuja Morogoro kutoa shukrani zake, alisema kwamba kuna viongozi katika ofisi za Serikali za kimkoa, mahakama, polisi, chama, wilayani vilevile wanakuwa hawawajibiki ipasavyo

katika kutoa utatuzi, wa matatizo haya wanakuwa wanalemea upande mmoja kwa maslahi yao binafsi.

Aidha, wao ni wafugaji wenyewe au wamewekeza kwenye ufugaji hili ni suala nyeti sana pesa peke yake hazitoshi tunataka watu wawajibike. Kwa hiyo pesa zimetolewa lakiniwatu wawajibike na pesa zimetolea katika kuziendesha *SACCOS* zetu na hili nalo ni suala nzuri, naamini kabisa *SACCOS* zetu zinahitaji kuwezeshwa na wafugaji, wakulima, wananchi wa kawaida, wafanyabiashara wadogo wadogo wanajiunga kwenye *SACCOS* na hizi *SACCOS* zisaidiwe. Hapo nitaendelea, sasa naomba kupata ufafanuzi kwa vile Waziri wanaohusika katika kitabu hiki hapa, wamesema kwamba *VIT* inataka iondolewe kwenye *petrol*, je uliposema petroli wanakusudia petroli ama petroli, dieseli, na mafuta ya taa pamoja, hawakuwema hivyo wamesema *petrol* sio bidhaa za petroli. Wamesema kwamba wanataka kuzidisha kodi kwenye magari madogo, mimi sifahamu magari madogo ni yepi, je, hizi *saloon* ndio gari ndogo, je, *pickup* tani moja ni gari ndogo, je hizi shangingi ni gari ndgogo, je, tani mbili na nusu au tani tatu na robo ni gari ndogo, ningependa kujua ufafanuzi gari ndogo ni zipi.

Samahani, nina ushauri kidogo nilishawahi kuzungumzia wakati alipokuja Mheshimiwa Rais alipotembelea hapa alitoa hotuba yake nikasema naapa naongelea tena na mimi ni mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii nitatoa utafiti zimeshafanywa nyingi, takwimu zipo mimi nilikwenda Tanga tukaona Nimri Songea tumekwenda, *SUA* wamefanya tafiti, hizi tafiti zimeshafanyika nchi yetu zilishafanyika za kutosha lakini hazifikii walengwa zinakusanywa zinawekwa sasa hivi kwenye kompyuta zamani zinakaa kwenye mafaili, sasa hivi kwenye makompyuta hazifikii walengwa.

wa hiyo sasa tuache makongamano, mawarsha misamiati mikubwa mikubwa, mikutano inafanya nini inaishaia pesa zinapotea, lakini walengwa hawasaidiwi. Kuna *NGOs* kule kwetu kuna kiongozi mmoja wa Wilaya wameunda *NGOs* yao wamekuja vijijini kwetu kule wakatizama zahanati wakasema hii inataka kusaidiwa wakapiga picha, wakaleta wataalam, nikifuatilia pesa ziko wapi wanasema pesa hazijaja, je, kweli hazijaja ni nani chombo gani kinachoweza kunihakikishia kwamba *NGOs* zinapoomba pesa na pesa zinakuja zinapofika Wilayani tujue zinakwenda wapi na kama zinakuja.wanapiga wakinamama wamebemba ndoo za maji wakitembea kwenye msululu wanapiga watoto wenye kwashakoo, wanauza wanapata pesa. Hizi *NGOs* zidhibitiwe tujue kama pesa zinakuja, zinakuja wapi zinatumika vipi.

Mheshimiwa Spika, kodi ya mafuta ya taa, iondoke kabisa *VAT* kodi yote iondoke, tunaondoa mafuta ya ndege kodi tunaacha mafuta ya taa tumepunguza, hatujapunguza hii kodi ni shilingi 70 sio kodi kupunguza hiyo. Kodi iondoke kabisa hii ndio tutaweza kukomboa wananchi wetu, tutaweza kulinda mazingira, kila kitu kitatokana na kuondoa kabisa kodi kwenye mafuta ya taa. Sasa hivi kule kwetu ninaushahidi wananchi wanaungua kwa sababu mafuta ya ndege yanauzwa kama mafuta taa.

Mimi nashangaa kwenye vituo Turiani, au Kilolo au wapi unapeleka mafuta ya taa hata ndege hakuna, wanapeleka mafuta ya ndege wanauza kama mafuta ya taa, wao wanahusika vipi inafikaje mafuta ya ndege yanafika vijijini huku jamani, tunajua tuna ndege ngapi mafuta yapo kiasi gani, vitu vinajulikana, viwanja vya ndege vinajulikana,

mafuta ya ndege yakitembea vijijini yanafikaje huku watu wanaungua wanakufa jana niliona mwenzangu akisema Mwakyembe akisema kwamba gari zitaharibika, gari zitaharibika wakichanganya kwenye petroli, gari zitatengenezwa.

Binadamu wanakufa hatengenezwi tusichanganye mafuta ya ndege kwenye mafuta ya taa ambayo wanatumia wananchi wetu, kwa hiyo mafuta ya taa yakiondolewa kodi watu hawatachanganya mafuta ya ndege kwenye mafuta ya taa tutalinda mazingira na tutasaidia wananchi wetu.

Watendaji wa Serikali, Rais ameingia madarakani amehakikisha amefanya mabadiliko shurfling kwenye Wizara, Ma-RC, ma-RPC, anakuja sasa hivi nasikia kwenye ma-DC lakini huku watendaji kwenye Serikali za Mitaa wameng'ang'ania wamekaa muda mrefu wanajisahau kwenye Kata wamekaa, kwenye Halmashauri wamekaa wanakuwa wao ndio.. mtajaza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mazingira kule kwetu juzi huyu huyu mgombea wa Urais alipokuja, sasa ni Rais wenyewe alipokuja samahani alisema watu wasishushwe kiholela milimani, waandaliwe maeneo ambayo wakishuka wataweza kuendesha kazi zao. Sio kama sasa hivi uwaambie washuke washuke hapa. Lakini wakiandaliwa maeneo mimi nasema, sawa washuke waandaliwe maeneo lakini mimi nasema sawa washuke waandaliwe maeneo waje lakini mlima kule juu kutakuwa kukavu kwa sababu kulishachomwa moto.

Nani atakuwa najukumu la kwenda kupanda miti, nani atakuwa na jukumu la kusimamia miti hiyo, na wananchi watakuwa na bado wanahasira wanaweza kwenda kusoma miti kule. Kwa hiyo maeneo yale yabakie yawe mali yao lakini sasa kama anavyosema Mbunge wetu mpya aliyekuja hapa wapande miti ya matunda, miti ya matunda itahifadhi mazingira matunda yatapatikana yatanufaisha wananchi na ile *green* tunayotaka itapatikana, wao kule wasipande mananasi wasipande migomba, waje huku chini mahindi yao wapandie huku chini.

Mheshimiwa Spika, kule juu bado maeneo yabakie ya kwao lakini wapande miti ya kudumu, hii nafikiri tutaweza kuwapatia kipato zaidi na tutaweza kuhakikisha kwamba milima imehifadhiwa na mazingira yanapatikana mazuri.

Katika masuala ya mazingira juzi katika uzinduzi wa jengo hili wote tulifurahi na kweli linamadhari nzuri linapendeza lakini tunajua kweli kwamba ni miti mingapi imetuma katika kuufanya urembo huu humu ndani, tunasema kwamba miti, tumekata miti mingapi katika kuweka urembo huu hamna anayetaka kuzungumzia kwa sababu ndio ukweli wenyewe.

Lakini mimi nasema tumeharibu miti mingi sana katika kuweka urembo huu hapa Waziri wa Mazingira yumo ndani anaona, hasemi, sasa ninasema njia au dawa ya kuweza ni kwamba tutumie sasa *MDF* bodi hii hapa, *MDF* bodi hizi zikiondolewa kodi hii ya

haya madawati tusiyagonge sana kwa nguvu, haya yanavunjika, lakini ndio yanayotumika sasa hivi. *(Makofi)*

Madawati haya yakitumika mbao hizi zikitumi, *aluminium* zikitumika wananchi watakuwa wamepunguza kutumia mbao zaidi, tunasema shule zijengwe, tunasema hizo shule zinahitaji madawati, shule zinahitaji madawati, shule zinahitaji, milango, meza, makabati kila kitu, tutatoa mbao huko huko kwa hiyo badala yake tupendekeza hizi *MDF* ziondolewe kodi, *aluminium* ziondolewe kodi, nasikia kuna milango ya *plastic* inakuja imefanana mbao kutoka South Africa, China, sijui Indonesia wanatengeneza hili tunaweza kutumia mbadala ije itumike hapa.

Mheshimiwa Spika, juzi pia katika ufunguzi wa jengo hili tumedanganywa hapa yule nafikiri Bwana Mataka, alisema kwamba tumetumia pesa nyingi za wananchi katika kum-*stabilizer* akasema hapa kwamba umeme una waves ametudanganya sote au kama hajatudanganya basi *TANESCO* kwa sababu wanasema umeme wao hauna *waves*.

Vifaa vinaungua, friji zinaungua mpaka nyumba zinaungua wanasema wao umeme wao hauna *wave's* lakini sasa tumeambiwa hapa umeme una *waves* ndio maana tumeweka ma-*stabilizer* sasa nani mkweli hizo *stabilize* na huyo Bwana Mataka ambaye ametumia kutueleza sisi Bungeni au *TANESCO* wanaosema umeme wao hauna mawimbi na nyumba zinaungua huko, watueleze nani.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Rais alikuja kwetu akaahidi kama mgombea alivyokuja kwamba Mkuyuni kutawekwa barabara nzuri na alipokuja juzi katika shukuru akasema barabara ya Mbena, Ngerengere kwenda Tununguwe pamoja na daraja pia itashughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, viongozi wahusika barabara hizo zipewe kipaumbele, lakini pamoja na barabara ningependa Mkuyuni kupate umeme ili tuweze kuweka viwanda vya kusindika ziweze kupatikana ajira kuweza kuhifadhi matunda yetu yanaharibika, macheza yanaharabika, maembe yanaharibika, machungwa yanaharibika, yanauzwa mpaka shilingi kumi mpaka shilingi tano, kwa sababu hayana thamani kule, jamani tupatie umeme pale kilomita 20 tu kutoka umeme ulipo mpaka pale, naomba hili suala lifuatiliwe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo ni taarifa za uwongo viongozi kuzitoa, aidha Mawaziri wanapewa taarifa za uwongo na watendaji wao sisi tunapokwenda Halmashauri tunaambiwa taarifa za uwongo na tukija kuthibitisha taarifa za uwongo hao ambao wanatudanganya sisi wanaodanganya sisi wawakilishi wa wananchi, wanachukuliwa hatua gani jamani kwa hiyo sasa imefika wakati wanaosema uwongo ole wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa katika hili kusema kwamba kwa sababu ya majukumu yetu ya kitaifa yanatubana kuweza kuhudhuria vikao vyote vya Halmashauri kule chini, kwa hiyo wawe tunapata taarifa za kule Halmashauri matumizi na mapato ya kila mwezi kwamba Halmashauri imepata kiasi hiki mwezi huu, na imetumia kiasi hiki wapi zimetumika ili hata ule muda mdogo tunaoupata kukimbilia tusiende kwenye vikao tukaenda kwenye majimbo kule tukaweza kuthibitisha kwamba yale kweli yametendeka

yapasavyo, na Mawaziri wanaohusika wanapopeleka programu zao watueleze hapa bwana Wizara ya Fedha imefanya hiki na hiki huko ukienda kathibitishe, Wizara ya Afya imefanya hivi, Wizara ya Kilimo imefanya hivi tupate hapa takwimu zake si tuko hapa jamani pua na mdomo, mtupe basi hayo bwana tuweze kufuatilia hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mlolongo na wingi wa kodi, mimi juzi nilibahatika nilikuwa Dubai pale nikanunua gari yangu baadaye nikabakia na kama dola 1100 hivi nikasema sasa nifanyaje, nikamwambia Mhindi mmoja pale akaniambia bwana hizo usirudi nazo, nipe nikube gari, dola 1100 akanipa gari, *Corolla* moja.

Mheshimiwa Spika, ile gari imenigharimu milioni moja na lakini tatu maana yake kule Dubai, mpaka nimeitoa mpaka juzi nimeitoa ipo barabarani imenigharimu milioni tano na laki tatu, milioni nne katikati zimetumika. Mlolongo huu mdogo mdogo lipa pale lipa hapa lipa hivi lipa kile milioni nne, jamani gari ya milioni na laki tatu ya zawadi inafika milioni tano, tuangalie tunapokwenda siko.

Mheshimiwa Spika, katika awamu ya iliyopita Mawaziri wawili waligongana wakawa wanasema moja boti haziendi, mwingine anasema zinakwenda, mwingine barabara haifai mwingine inafaa hii ilikuwa ni kitu ambacho kwa kweli kilituambisha sisi sana, na juzi hapa tuko kwenye Bunge lile kuna Mawaziri wakagongana tena kidogo pale *friction* ikatokea, kuna mabaraza yao jamani mkagombane huko mkija huku mtuletee maamuzi ya Kiserikali pamoja, msiwe mnagongana gongana mbelel yetu hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia *TIC* yaani Viwango vya Uwekezaji, viwango vya uwekezaji kwa wawekezaji wa nje, dola 300,000 ni ndogo ziongezwe angalau dola milioni moja ziweze kuwatosheleza. Asante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, namuita sasa Mheshimiwa Aloyce Kimaro atafuata Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia.

Nitamruka Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama ili tumalizie na radha kidogo ya Upinzani nitakuita Mheshimiwa Philemon Ndesamburo.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nami nafasi ya kuchangia na kutoa mawazo yangu kwenye hotuba ya Waziri wa Mipango, Uwezeshaji na hotuba ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, mimi nianze kwa kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo langu la Vunjo kwa kuweza kunichagua kwa kura nyingi na kuondoa upinzani uliodumu kwa miaka 10 jimbo la Vunjo. Nawapongeza sana wananchi wangu nawaambia kwamba nami nitawatumiki, jembe lilikosa mpini kwa miaka 10 sasa limepata mpini litalima. (*Makofi*)

La pili, niwapongeze vilevile kwa kumchagua Mheshimiwa Rais Jakaya M. Kikwete kuwa Rais wa Tanzania, vilevile niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili jipya wote walioteuliwa na waliochaguliwa na Mawaziri walioteuliwa

nawapongezeni sana. Naliita hili Bunge ni Bunge la *intake* ya Ari Mpya, sasa naomba tufanye kazi ili hii *intake* ya Ari mpya iweze tena kurudi mwaka 2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikiendelea naomba niishukuru Serikali kwa kutoa ushirikiano wa haraka na wa hali na mali wakati mafuriko yalipotokea Jimbo langu la Vunjo pamoja na Moshi Mjini, nimpongeze sana Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kufika harakaharaka aliposikia kwamba kuna mafuriko na maafa Jimbo la Moshi Vijijini na Vunjo.

Nimpongeze pia Waziri Mkuu aliposikia kwenye vyombo vya habari kwamba kuna mafuriko alinipigia simu akaniuliza Kimaro hayo niliyoyaona ni kweli? Nikamwambia ni kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu akasema basi na sisi tutafika, namshukuru kwa kujali. (*Makofi*)

Namshukuru vilevile Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Juma J. Akukweti kwa kufika harakaharaka pamoja na watendaji wake, nawashukuru wote waliotoa misaada nikianza na Viongozi wa Dini pamoja na Serikali. Viongozi wa Dini Mheshimiwa Baba Askofu Amedeus Msarikie namshukuru kwa kusaidia maafa yale, namshukuru vilevile Mhashamu Askofu Martin Shayo KKT DAyosisi ya Kaskazini kwa kusaidia, nawashukuru wengine *UNDP*, *FAO*, *WFP*, na wengine wananchi wa kawaida waliochangia maafa yale. Natoa shukrani sana kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nianze kuchangia hotuba ya Fedha, nianze na kodi ya madini. Tunao wachimbaji na makampuni mengi sana ya madini hapa nchini, ninatoa mfano wa kodi moja unaosamehewa ambao wasingepaswa kusamehewa. Hakuna nchi duniani inayochimba madini ambayo huwasamehe wale wachimbaji kodi ambayo inaitwa *Fuel Levy*.

Mheshimiwa Spika, tukichukulia mgodi mmoja tu wa Geita, Geita kwa mwaka wanaagiza mafuta ya *petrol* lita milioni 58 na ukiangalia kodi wanayosamehewa *fuel Levy* inalipiwa shilingi 90 kwa lita moja kwa hiyo lita milioni 58 kodi wanayosamehewa ni bilioni 5.2 kwa mwaka, shilingi bilioni 5.2. Sheria inasema kwamba wawe wamewekewa kiwango maalum cha kulipa kwa mwaka *fuel levy* dola 200 kwa hiyo tunakosa kodi ya billion 4.97 kwa mwaka kwa mgodi huo mmoja sasa hebu fikiria tuna migodi mingapi?

Ukienda Kahama tuna migodi, Buhemba kuna migodi, Tarime kuna migodi sasa kwa ujumla wote huku tunalia barabara hazijengwi lakini hawa wachimba migodi tunawasamehe kodi ambayo ni wazi ile kodi tunayowasamehe ni gharama unapokwenda kuchimba unapokwenda kazini ni lazima kuwe na gharama kwa hiyo kununua mafuta ni gharama ya kuendesha migodi. Kwa hiyo mwisho wa mwaka unatoa zile gharama wakati unakokotoa mahesabu ya mwaka, sasa hawa wanakuja wanatudanganya tunasema eti ni mikataba mizuri mkataba huu naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha hii *fuel levy* turekebishe ile sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili tuingize kipengele hiki hawa watu walipe kodi na ukweli wenyewe ni kwamba pesa wanazo kwa sababu dhahabu kwa miaka mitano iliyopita imeongezeka bei maradufu sasa wao wanazo pesa wanataka sisi

tuwadai basi turekebishe mikataba wanatucheka wengine na ndiyo maana nimepata mimi toka kwao hasara hii ambayo tunapata wanashangaa kwa nini hatuai, naomba Mheshimiwa Waziri turekebishe hii tuendelee kuwadai.

Vilevile haya makampuni haya hayatusaidii chochote kule kwenye midogo chakula chote wanachokuwa wanaagiza nje na wanasamehewa ushuru, hata dobi wa kupasi nguo zao na kufua wanatoka nje, hata chakula cha paka wanaagiza kutoka nje na wanasamehewa kodi. Sasa tukisema kwamba ukienda Kahama ningetegemea zile barabara za Kahama kodi hizi ambazo tunawasamehe ndiyo zingejenga zile barabara, ukienda Geita vilevile, ukienda Tarime unakuta wale wananchi wanafukuzana kwa mapanga na wale wawekezaji kwa sababu wale wananchi hawafaidi kitu chochote pale wanasema bora madini yetu yabaki mbona hawa wanakuja hatufaidi chochote? Hawauzi mchicha, nyamba, kuku na wala hawatoi huduma yoyote kwa hiyo ile pesa haiingii kwao ndiyo maana wanalalamika. Naomba hii irekebishwe.

Mheshimiwa Spika, lingine nichangie kwenye usafiri. Hapa tulikua tunazungumzia suala la ndege ya Rais. Ndege ya Rais ilishanunuliwa kila leo ndege ya Rais hivi mnataka Rais wa Ari Mpya apande ndege gani? Naomba huu mjadala uishe tuende na Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya. Hii intake mpya ni ya mambo ya kisasa hata hili Bunge ni la kisasa, mwishowe mtasema hata hili Bunge tuliache turudi kuwe kwa zamani naomba wenye mawazo hayo yaishe twende mbele badala ya kurudi nyuma twende mbele kwa Kasi Mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nichangie lingine kwa harakaharaka nalo ni usafiri. Usafiri hasa wa daladala mijini na wa mabasi ni kero kubwa sana, ukienda kwenye vituo vya daladala ni kelele, wapiga debe wale wenye magari madereva hawana heshima kwa wateja wao ni kudaiwa tu kelele sana wateja kama kungekuwa na njia nyingine ya usafiri wasingepanda daladala lakini Serikali ipo inaona naomba itoe tamko kupunguza adha hii wanayopata hata wanafunzi. Wanafunzi wanakuwa hawana wenyewe, wazazi wanawaachi vituoni mabasi yanawaacha vituoni Serikali inaona haisemi kitu, naomba vyombo vinavyohusika vikae wanafunzi hawa wapate dawa waende shule na kurudi shule sawasawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni usafiri wa mabasi, mabasi yanaua watu kila leo lakini ukiangalia sasa hivi hakuna mabasi mapya yanayoingia nchini ni malori wanachukua huko nje wanakuja kubadilisha wanaweka mabodi *board substandard* inakuwa ni basi kwa hiyo dereva yuleyule tabia ya daladala anahamia kwenye mabasi yanayokwenda mikoani kwa hiyo unakuta anaendesha kwa speed kali gari linaanguka linakwisha kabisa kwanza kwa sababu zile board tunazotengeneza ni sub standard hakuna jinsi ya kuweza kuweka kiwango cha kutengeneza board ya gari. Gari likianguka linakuwa *flat* linaua watu wote lakini kama tungekuwa na viwango wanaotengeneza magari huwa wanakuwa na njia ya ku – *test* kwamba je, gari likipata ajali litaumia kiasi gani? Kwa hiyo wanakuwa wana njia ya ku-*crush* kabla board haijawa taabani. Lakini sasa hivi mabasi yetu ma – *board* yanatengenezwa huko Manzese kwenye viwanda vidogovidogo tunasema SIDO lakini tunawapeleka wananchi wetu kwenye hali ya hatari basi likianguka ni lazima liue watu wote.

Angalia kule Simanjiro Rafiki yangu Ole Sendeka nikupe pole na wale wa Bukoba kwa ajali waliyopata lakini kama yale mabasi yasingekuwa yanazidisha watu halafu na board zake ni imara likianguka haliwezi kuua watu wengi kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, nikirudi Simanjiro kwa Ole Sendeka kuna machimbo ya *TANZANITE* yapo kule, yale machimbo walikuwa wanachimba wachimbaji wadogowadogo na walikuwa wanafaidi mji wa Arusha umejengwa na wachimbaji wadogowadogo lakini baada ya hapo wananyanyaswa hawana kitu hata mji wa Arusha hauendelei sasa.

Naomba maeneo mengine tuwaachie wachimbaji wadogowadogo, kula Chunya dhahabu ipo unachimba mita tatu unapata dhahabu, Kusini kule Songea kuna madini basi tuwaachie wachimbaji wadogowadogo nao wafaidi. Hawa wachimbaji wakubwa tuwape sheria nzuri ambazo na sisi tutafaidi tuwapeleke kwenye maeneo yale ambayo madini yapo chini mita nyingi kwa sababu wana vyombo wachimbe wao ili na sisi wananchi tuweze kufaidi na mali ya asili tuliyo nayo.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hotuba hizi mbili za Bajeti ya Wizara ya Fedha pamoja Bajeti ya Wizara ya Mipango Uchumi na uwezeshaji.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia afya, uzima na kutuwezesha sisi Wabunge kuweza kukutana mahali hapa kwa ajili ya kutetea maslahi ya wananchi wetu wa Tanzania na kwa ajili ya kutunga sheria nzuri ambazo zitakuwa zinaendana na nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kuanza kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hizi za Serikali mia kwa mia. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji Dr. Juma Ngasongwa, kwa kuweza kuwasilisha vizuri kabisa hotuba yake ya Bajeti na pia nachukua fursa hii kumpongeza Waziri wa kwanza Mwanamke nchini Tanzania Waziri wa Fedha kwa kipindi cha miaka 40 iliyopita toka nchi yetu ilipopata uhuru mwaka 1961.

Nikianza kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Fedha pamoja na Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Naomba nianze na kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na nichukue pia fursa hii kuipongeza Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa bajeti yao kupanda kwa asilimia 53 ukilinganisha na bajeti ya mwaka jana. Mwaka 2005/2006 Serikali ilitenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 59,180,248,399/= kwa ajili ya Wizara hii ya Elimu lakini kwa mwaka huu pesa hii imeongezeka imekuwa bilioni 127,132,293,000/=

Mheshimiwa Spika, kwa jinsi ninavyoona hivi naamini kabisa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi itafanya mambo mengi makubwa kwanza niwapongeze kwa

mpango wao wa MMEM na MMES ambao umefanikiwa sana na umeweza kuiweka Elimu mahali pazuri katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tunaweza tukawa na madarasa mazuri, vitabu ndani yake, walimu wazuri, wanafunzi pia wapo lakini kama wanafunzi hao watashindwa kuwezeshwa kufika shuleni mapema na kwa muda unaotakiwa itakuwa ni kazi bure. Naomba niiombe Wizara ya Elimu na Mafinzo ya Ufundi iwajali kwa dhati kabisa wanafunzi kabisa kutokana na tatizo la usafiri hasa kwa mkoa wa Dar es Salaam kwa sababu Mkoa wa Dar es Salaam ndiyo ambao umekuwa ukitumia sana daladala kwa ajili ya kuwapeleka wanafunzi mashuleni.

Mheshimiwa Spika, Wanafunzi hao wamekuwa wakinyanyasika na makonda, wanafunzi hao kwa vile wamekuwa wanalipa shilingi 50/= inaonekana ni hasara kwa wamiliki wa mabasi. Najua Serikali ina mpango wa dhati kabisa kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi hao naomba nimpongeze Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mheshimiwa Lt. Yusuph Makamba kwa kusimama kidete kutetea na kutetea wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, lakini tukumbuke kwamba yale ni mabasi ya watu binafsi, ni soko huria na wao pia wana uamuzi wao wa kuwabeba wanafunzi wanapotaka ninachokuomba mimi kwa Serikali ni kuleta mabasi ambayo yatakuwa yapo maalum kwa ajili ya kuwabeba wanafunzi na kuwapeleka mashuleni.

Mheshimiwa Spika, miaka ya nyuma nilisikia mradi wa mabasi kwa wanafunzi kwamba upo lakini sijui umefikia wapi mpaka leo sijui kinachoendelea katika ule mradi wa mabasi ya wanafunzi. Tuachane na ya nyuma yaliyopita si ndwele kwa sasa hivi kutokana na Bajeti hii ambayo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi wanayo na pia najua wafadhili mbalimbali kutoka nje wamekuwa wakichangia kwa kiasi kikubwa katika Sekta hii ya Elimu nakuomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mama Margaret Sitta uwasaidie wanafunzi wa Mkoa wa Dar es Salaam waache kunyanyasika wanahitaji mabasi yao kutoka Serikali na si kwa watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, nikiingia katika upande wa Wizara ya Afya. Afya ni kitu muhimu sana katika maendeleo ya nchi yoyote ile nadhani hilo mnalifahamu, Wizara ya Afya Bajeti ya mwaka jana ilipangiwa shilingi bilioni 278,495,487,700/= lakini kwa Bajeti ya mwaka huu naona Bajeti hii imepungua sielewi ni kwa nini imetengwa bilioni 194,777,665/= ikiwa ni upungufu wa 42% hii nakisi kwa upande wa Wizara ya Afya. Tukumbuke kwamba wakati wa Kampeni Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kupitia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2005/2010 aliahidi ajira zaidi ya milioni moja kwa vijana na Watanzania wote kwa ujumla.

Katika ajira hizo nikimnukuu Mheshimiwa Rais alisema kwamba zitatokana na Sekta Rasmi na Sekta isiyo rasmi, alisema Sekta iliyo rasmi ambayo itachangia sana kupatikana kwa ajira hii ni pamoja na kwenye Elimu na kwenye Afya lakini nashangazwa kwa Bajeti hii kupungua kiasi hiki ambapo tuliambiwa Zahanati zitajengwa

katika kila Kata, vituo vya Afya vitajengwa katika kila Kata kwa ajili ya kuwasaidia wananchi na pia ajira ziweze kutoka hapo.

Wizara ya Afya imekuwa ikilalamikiwa kwa kipindi kirefu sana kwamba wananchi hawapati huduma zile ambazo zinatakiwa bado dawa zinakuwa hazipatikani mahospitalini, hospitali zetu pia zinakuwa zina upungufu wa mambo mengi. Sasa nashangaa tunapopiga hatua mbele sasa hivi badala ya bajeti hii ya Wizara ya Afya nilitegemea kwamba itaongezeka lakini nashangaa imepungua sielewi ni kwa nini nitaomba majibu yatakayoniridha kutoka kwa Wizara ya Afya watueleze watapata wapi pesa za kujenga hospitali ya ugonjwa wa Moyo ambayo imeahidiwa pia katika ilani ya Chama cha Mapinduzi kama Bajeti hii impungua? Watapata wapi pesa za kujenga zahanati, vituo vya afya ambavyo Mheshimiwa Rais aliahidi kupitia ilani ya Chama cha Mapinduzi? Naomba ufafanuzi katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapahapa katika Afya naomba nitoe masikito yangu makubwa sana kwa jinsi ambavyo akina Mama wajawazito wamekuwa wakipata tabu katika hospitali mbalimbali na vituo mbalimbali vya afya nchini kwetu. Nilibahatika kutembelea hospitali ya Temeke iliyopo Mjini Dar es Salaam nikenda mpaka kwenye *Ward* ya Wazazi halii niliyokuta mle ndani inatisha, hali iliyokuwepo kule ni mbaya sana akina Mama wako wengi wamerundikana *Ward* inakuwa haitoshi, hospitali hiyo hiyo inatumika na watu kutoka Mtoni, Temeke, Mbagala, Kigamboni na maeneo mengi sana ya mji wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, hali inatisha sana kwa sababu akina Mama wanakosa mpaka vitanda vya kujifungulia, nilikuta kwa wakati mmoja akina Mama zaidi ya 15 wanalia uchungu lakini hospitali ya Temeke ina vitanda vitatu tu na ma-*nurse* mle ndani ni watatu hawazidi wannne wataweza vipi kuwahudumia akina Mama 15 wanaolia uchungu kwa wakati mmoja wakati kuna vitanda viwili au vitatu tu hospitalini.

Ningeomba hili liangaliwe kwa uzuri kabisa ndiyo maana nikawa nasikitika bado kwa nini Bajeti yao imepungua wakati afya ni kitu muhimu na ninaomba tusifanye majaribio katika afya za binadamu, naliomba hilo.

Mheshimiwa Spika, nilichofikiria mimi ni kitu kimoja, kama Dar es Salaam ambayo watu wengi wanailalamikia wanasema pale ndiyo maendeleo yote yapo pale ukisema barabara basi zinajengwa Dar es Salaam, hospitali zipo Dar es Salaam ukiongelea huduma nyingi muhimu zinapatikana Dar es Salaam lakini tunashangaa Dar es Salaam hiihii bado inakuwa ina msongamano wa watu nikajaribu kufikiria je Babu zangu waliopo kule Namasakata Tunduru hali ikoje kama Dar es Salaam iko vile? Bibi zangu waliopo Lupembe huko Njombe Iyanjo hali yao iko vipi kama Dar es Saalam sisi ambao tunaambiwa ndiyo sehemu ambayo mafanikio yote yapo pale lakini bado kuna upungufu? Vipi pia kwa Babu zangu, Wajomba zangu, Shangazi zangu waliopo Kware kule Hai Moshi, Sengerema, Ukerewe hali iko vipi? bila kuisahau na Geita nakumbushwa.

Mshimiwa Spika, naomba tuliangalie kwa makini kabisa suala hili la afya kwa sababu ni suala nyeti na mwananchi yeyote wa kawaida akisikia kwamba pato la uchumi wetu limepanda kwa asilimia kubwa, kwa asilimia Fulani anategemea kabisa huduma katika jamii zinakuwa zimeboreshwa ikiwemo Elimu, Afya pamoja na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Wizara ya Afya nawaomba chondechonde kama inawezekana tujaribu angalau katika kila Wilaya tujenge hospitali moja ambayo itakuwa inashughulika na masuala ya akina Mama ya uzazi peke yake kwa sababu watoto ni kila siku wanazaliwa kwa hiyo tuangalie umuhimu wa hivi Viwanda Watu mimi naviita Viwanda Watu kwa sababu ndivyo ambavyo vinazalisha watu wanaweza kuzaliwa huko.

Kwa hiyo, ombi langu kwa Wizara ya Afya namba tafadhali tujitahidi angalau kujenga hospitali moja katika kila Wilaya ambayo itakuwa inatatua matatizo ya uzazi kwa akina Mama kwa sababu uzazi si kwenda kujifungua tu bali Mama anatakiwa aangaliwe wengine kabla ya miezi miwili au mitatu ya kujifungua wanakuwa wana matatizo kwa hiyo naomba tulilie hilo baada ya Mama kujifungua anatakiwa awekwe katika uangalizi mzuri tuweke mazingira mazuri.

Mheshimiwa Spika, nikiingia katika upande wa JKT yaani Jeshi la Kujenga Taifa kwanza napenda nichukue nafasi hii kuipongeza kwa kuwa inatoa mafunzo kwa vijana wengi ambao baadaye wanatakiwa kwenda kujiajiri kwa hiyo naomba nilipongeze Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, nilivyoangalia na wao pia mwaka jana zilitengwa shilingi bilioni 37,753,518,377/= lakini mwaka huu wametengewa bilioni 45,608,996,000/= hii imeongezeka kwa 17%. Japokuwa siyo asilimia kubwa sana lakini najua mtu huwezi ukavuka tu moja kwa moja kuna hatua ambazo unakuwa unafikia kwa hiyo basi ninachokiomba hapa Jeshi la Kujenga Taifa ni kweli wamekuwa wakitoa mafunzo kwa vijana kila baada ya mika miwili.

Lakini vijana hawa baada ya kutoka katika mafunzo ambapo wanakuwa wanafundishwa jinsi ya kutumia silaha, wafundishwa jinsi ya kupambana na majambazi, wanafundishwa jinsi kukabiliana na maadui, wanafundishwa ujasiliamali na vitu mbalimbali lakini baada ya mafunzo hakuna utaratibu mzuri ambao umeandaliwa na Jeshi la Kujenga Taifa kwa gharama zile ambazo Serikali ilitumia kuwaandaa vijana hawa ili waende kulitumikia Taifa lao vyema.

Mheshimiwa Spika, vijana baada ya kupata mafunzo kutoka Jeshi la Kujenga Taifa huwa wanarudi tu majumbani tukumbuke kwamba hao vijana wanaourudi majumbani wameshafundishwa kutumia silaha,wameshafundishwa jinsi ya kupambana na adui pamoja na mambo mengine mengi hii inachangia ongezeko kubwa la majambazi nchini kwetu kwa sababu wameshafundishwa kutumia silaha lakini wanakuwa hawaajiriwi wamekaa.

Naomba Jeshi la Kujenga Taifa kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana mnaweza mkaweka mpango mzuri kwamba kijana anapotoka JKT waangalie katika ajira zile ambazo zimepangwa kupitia Wizara ya Kazi vijana hawa wapewe kama kuna ajira yoyote katika makampuni ya ulinzi au kama kuna mikopo vijana watapewa baada ya yale mafunzo ambayo wamepewa kutoka kule JKT waweze kuyatumia kwa manufaa ya Taifa letu na hii fedha iliyotumika kwenye mafunzo kwa vijana hawa isipotee bure. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, najaribu kukimbizana na muda. Mwisho naomba nizungumzie suala la Wamachinga wa Kichina ambao wamevamia katika soko la Kariakoo, Jijini Dar es Salaam. Vijana wa Kitanzania, akina Mama wa Kitanzania wamepata mikopo katika Benki zao hapa nyumbani wanasafiri kwenda China wanalipa dola 1,000/= nauli ya kwenda na kurudi wanaleta mzigo wakifika hapa wanataka kuuza wanalipia malazi ambayo walilala kule China, wanalipia gharama za usafiri na vitu vingine vidogovidogo ili fedha yao iweze kurudi na waweze kurudisha hii mikopo ambayo wamekopeshwa.

Mheshimiwa Spika, la kusikitisha sasa hivi sijui ni wawekezaji kutoka China sielewi wamevamia pale Kariakoo, bei za vitu ambavyo akina Mama na Vijana wa Kitanzania wamekwenda kununulia China ndiyo hiyo hiyo Wachina hao wanaiuza bale Kariakoo kwa rejareja. Hivi kweli leo tunaahidi ajira zaidi ya milioni moja tunawaleta Wachina nao waje kuuza bidhaa kwa bei ya rejareja? Tunakwenda wapi?

Kama kweli Wachina ni wawekezaji mimi sina ugomvi na Wachina waje nchini kwetu wajenge viwanda Watanzania hao waajiriwe, waingie katika hivyo viwanda lakini siyo kutoa bidhaa kule kuja kuuza hapa. Naomba hili liangaliwe kwa upana zaidi na nitahitaji majibu kutoka kwa Wizara, Wachina wa pale Kariakoo ni wawekezaji au wachukuaji. Wamekuja kuchukua uchumi wetu hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, naomba ufafanuzi katika hili tuwahurumie wazawa, tuwahurumie wazalengo jinsi wanavyohangaika katika kupata kipato kama kweli wanataka kutusaidia basi Watanzania waache kusafiri walete vifaa hapa kwa bei ya jumla wauze kwa bei ya jumla, lakini si kwa rejareja wanakuja kutunyonya sisi Watanzania. Wanakuja kutunyonya sisi Vijana, wanakuja kuwanyonya Mama zetu ambao wameamua kuacha kazi zao na kufanya biashara.

Mheshimiwa Spika, sipendi nigongewe kengele ya pili naomba nimalizie kwa kumtakia kila la kheri Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika majukumu yake, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri pamoja na Manaibu Waziri, Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia na naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge ahsante kwa mchango wako mzuri. Waheshimiwa Wabunge, nikimwita Msemaji wa mwisho Mheshimiwa Philemon

Ndesamburo na nikizingatia kwamba Naibu Mawaziri wa tatu kila mmoja apate nafasi ya dakika 20, muda wa kuahirisha Bunge uliopo katika Kanuni utakuwa umepitwa kwa dakika 10.

Lakini ni muhimu tuitendee haki kwa Manaibu Mawaziri. Kwa hiyo, namwomba Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni au Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu tuweze kutengua kanuni inayotudai hapa tufunge Shughuli za Bunge saa 7.00 ili tufike saa 7.10. Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

## KUTENGUA MUDA WA KUMALIZA BUNGE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED S. KHATIB):** Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kutoa hoja kwamba kifungu kinachohusika kitenguliwe ili Bunge liendelee baada ya muda wake mpaka lifikie saa 7.10 mchana.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Kuongeza Muda wa Kumaliza Bunge iliafikiwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, walioafiki naona wameshinda kwa hiyo tutaketi hadi saa 7.10 ndipo tutakapositisha Shughuli za Bunge kwa asubuhi hii. Ahsanteni sana. Sasa namwita Mheshimiwa Philemon Ndesamburo.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia mchango wangu katika hoja hizi mbili za Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji.

Mheshimiwa Spika, kwanza nitoe pongezi zangu kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kwa kuonyesha njia kama kiongozi anayeweka Utaifa wa nchi yetu mbele. Ni matumaini yangu viongozi wengine wataiga mfano wake na kuweka Utaifa mbele badala ya mambo mengine yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa wakati nikirudi katika kuchangia hotuba hizi mbili, nianze na umeme. Tumekuwa na tatizo katika nchi hii wa umeme. Lakini tumeishawekeza sana katika nchi hii kwenye umeme. Tumewekeza kwa kiasi kikubwa katika Mtera ambayo ndiyo inatupa umeme mwingi katika nchi hii. Umeme wa maji ndiyo rahisi kuliko umeme mwingine wowote duniani.

Sielewi makosa yalitokea wapi tufanye umeme wa Mtera usiwe ndiyo chanzo kikubwa kwa Tanzania. Nasema hili kwa sababu tunalaumu jua, ukame na kutokuwa na mvua. Lakini nataka kuonyesha lazima kuna mapungufu fulani. Tukichukua nchi kama *Egypt* hawajui mvua, hawajui misitu, wanategemea *River Nile* kwa kuzalisha umeme wao. Kwa kutumia ma- *dam* ambayo wanayo wana namna ya ku-*re-circle* maji yakarudi nyuma na kujaza ma-*dam* yao na wanaendelea kuzalisha umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna bahati ya kuwa na mito ambayo haikauki, lakini tunayaachia maji yetu yanapotea kwa kwenda baharini. Badala ya kubuni mbinu yaku-*re-circle* maji na kuhakikisha kwamba maji tunayotupa baharini yanarudi na kujaza ma-*dam*, sasa tunakimbilia kuanzisha vianzo vipya vya umeme badala ya kutumia vile ambavyo tayari tunavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeanza vilevile kuleta madhara mengine kwa wakulima wa Mbeya wanaambiwa wasitumie mito yao kwa kuzalisha chakula. Hili ni tatizo lingine kubwa ambalo tunajaribu kulipika upya. Kazi ya Serikali badala ya kutumia fedha nyingi kuanzisha vianzo vipya tungekuwa tume-*re-circle* maji ya Mto Rufiji au mito ile inayoleta umeme yakarudi nyuma yakajaza yale mabwawa, tatizo tulilonalo sasa halingekuwepo kabisa na tungekuwa tunatafuta njia nyingine mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chakula ni kitu muhimu bila chakula tumeona matatizo tuliyoyapata kwa muda mfupi tu kwa kuwa tulikosa mvua. Kwa kukosa mvua tumekosa umeme na tumekosa na chakula. Lakini tumesisitiza ya kuwa kilimo cha umwagiliaji ndicho tunachokihitaji hapa Tanzania. Tunapowambia wakulima wasitumie maji ya mito eti ili tuweze kuzalisha umeme nadhani kuna kasoro na ningeomba tuliangalie upya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la msingi ardhi na watu ndiyo kitu cha maana katika nchi yoyote ile. Ardhi ndiyo mali ya nchi hii na bila ardhi hatuwezi kufanya chochote. Tunalia njaa, nchi inakuwa maskini kwa sababu ya hatutumii ardhi yetu inavyopasa. Wananchi hawana uhakika na ardhi yao, hata kipande cha kujenga kibanda mwananchi anaambiwa miezi 36 lazima ajenge nyumba, asipojenga Serikali inamnyang'anya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ardhi ni mali. Unamtazamiaje mfanyakazi wa Serikali hata mkulima anayepata shilingi 50,000/= kwa mwezi ajenge nyumba katika kiwanja ndani ya miaka mitatu, hawezi na ile siyo sheria. Hatujawahi kupitisha sheria kwenye Bunge hili inayosema mtu ajenge nyumba kwa miaka mitatu na zile ni Kanuni tu. Nadhani Bunge hili lingepitisha sheria ya kufuta Kanuni hizi.

Mheshimiwa Spika, juzi hapa tunakuwa na *double standard* za ajabu katika nchi hii. Unakuta mtu ana kiwanja miaka mitatu hajakiendeleza Serikali inamnyang'anya. Waziri alisema hapa juzi anataka ku- *involve* viwanja ambavyo watu wanavyo kwa miaka 20 hawajajenga. Je, Serikali ilikuwa wapi mpaka miaka 20 mtu hajajenga? Je, wamemwonaje mwenye kiwanja kwa miaka 4 hajakijenga wanakichukua na kiwanja cha miaka 20 kinaachwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tuwe na sheria ambayo inakuwa na usawa kwa wote katika nchi, tunalia kwa sababu hatuna sheria. Inapendeza kidogo kwa sababu kama ukirudi katika hotuba ya Waziri wa Fedha katika ukurasa wa 21, anasema ametenga fedha kwa ajili ya kufanya *survey* na kutoa *title deed* katika vijiji nadhani pamoja na Mijini.

Tunatoa hii ili watu waweze kuwa na hati za kuweza kuzitumia hata wakati wakitaka kukopa katika mabenki ili waweze kuendeleza uchumi wao na uchumi wa Taifa kwa ujumla. Hapo natoa hongera kwa sababu Waziri ameona mbali. Maana yake kwenye MKUKUTA tunatazama mtu mmoja mmoja akishakuwa tajiri akaweza kujiwezesha utajiri wa kupata mlo angalau miwili kwa kutwa ni *step* moja ya MKUKUTA ya kumwokoa Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ya kutenga fedha kwa ajili ya kufanya *survey* ya nchi ni *step* moja nzuri. Lakini vilevile tuelewe nchi hii ni kubwa sana tunaweza ku-*accommodate* wawekezaji. Tumeweka misingi yetu mikubwa kwa wawekezaji wa viwanda, tukasahau wawekezaji tunaowataka katika nchi hii zaidi kwamba ni wakulima wa chakula. Kiburi cha Mmarikani mpaka leo ni kuwa na chakula. Nchi yoyote yenye chakula cha kutosha ina kiburi cha kutosha. Tanzania ina ardhi ya kutosha kulima na kuweza kulisha Afrika nzima. Lakini tunakataa tunaacha kutumia utajiri huu kwa sababu moja ndogo, tumekataa kutoa *free hold* kwa watu wanaotaka kuja kuwekeza kwenye kilimo katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, unapompa mtu *free hold* hahami katika nchi hii na hatatoka katika nchi hii na ardhi nimezungumza katika Bunge hili lakini watu hawanielewi. Bila kuwa na *free hold* hatutakaa tupate wawekezaji kwenye kilimo katika nchi hii. Zimbabwe ilipokuwa na matatizo, wakulima walitaka kuja katika nchi yetu, walipokuja walikatazwa kupewa, walikwenda Msumbiji wakapewa na wamekwenda Zambia sasa wamepewa.

Tunabaki hapa na ardhi yetu tunaiangalia kwa nini tusitoe hiyo *free hold* baada ya miaka 50 watoto wetu watafuta, tukajikomboa katika matatizo haya ya sasa. Kama tungelikuwa na *free hold* hata wenyewe viwanja vidogo vidogo Serikali isingeweza kuvichukua maana ni mali yao. Mwenzangu ananiambia hapo nimejiua, sijajiua ndugu yangu, nchi zote duniani *free hold* ipo na *lease hold* ipo. Iko *free hold* na *lease hold*.

Mheshimiwa Spika, mtu anataka kuwekeza ni lazima awe na *guarantee* kwani atahama na nchi hii, nchi hii iko pale pale. Sisi tunachotaka ni kuleta utajiri katika nchi yetu ili wananchi wetu waweze kuondoka katika umaskini tulionao, tutaendelea hivi mpaka lini? Lazima tuwe na fikra mpya. Tumesema kuna ari mpya, tuwe na ari ya fikra mpya ya kuweza kukomboa nchi hii ili tuweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 39 Mheshimiwa Waziri amesema anapandisha ushuru wa bia inayotengenezwa kwa nafaka ambayo haijaoteshwa kutoka shilingi 150 mpaka 161.

Mimi sijui Mheshimiwa Waziri kuna bia ambayo ina nafaka ambayo haijaoteshwa, mimi sielewi. Labda ile bia wanasema *beer without apple*, lakini hata hiyo

bila kuoteshwa? Sijui kimefungwa fungwa kitu gani hapa hata pombe ya kienyeji lazima ioteshwe. Labda Mheshimiwa Waziri atatueleza wakati atakapokuwa anafafanua ana maana gani anaposema pombe ambayo haijaoteshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine tena nimeliona nadhani *page 36* anasema katika kurekebisha mambo ya *TRA*, kurekebisha kiwango cha adhabu kwa kosa la kushindwa labda msamiati ni mbaya. Mtu anayeshindwa unapigaje faini, hana kitu ni kumfilisi. Tunasema mtu huyu ameshindwa kulipa tunakubali sisi ya kuwa ameshindwa. Halafu tunaongeza kiwango cha adhabu ni kwamba utamwondoa katika shughuli ya kufanya biashara na ni kwamba atatoka kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijagongewa kengele ya pili. Sisi kama tukiwa ndiyo Waheshimiwa Wabunge tuanze kuonyesha njia kwa kudhibiti matumizi ya Serikali. Hapa tunajaribu kutafuta fedha za kuleta maendeleo. Sisi Waheshimiwa Wabunge tuanze kuonyesha mfano kwa kujaribu kupunguza matumizi.

Mheshimiwa Spika, nimeona tuna hulka au tuna tabia katika Bunge hili karibu dakika moja kila Mheshimiwa Mbunge anasifia na kupongeza ni matumizi mabaya. Dakika tano, kumi tunapongeza, tunapongeza nini? Wengine hata Waziri akijibu swali kama ni mbaya anasema pamoja na majibu mazuri na huku anasimama anapinga. Hii misamiati lazima tuiache ndugu zangu. Lazima twende na Ari Mpya na Mambo Mapya, tujisahihishe. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba kumalizia hapo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, ahsante sana kwa mchango huo. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, kwa jitihada zake binafsi, Wizara ya Fedha na Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge katika kutengeneza bajeti yenye mvuto na ambayo imekuwa ikingojewa kwa hamu kwa mwaka wa fedha wa Serikali, 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba lengo la kila bajeti ya Serikali lazima liwe ni kupanua msingi wa mapato ya nchi kwa kutoa vichocheo ambavyo vinapanua uzalishaji wa bidhaa na huduma katika uchumi wetu. Hii huwa na athari chanya za kuongeza ukuaji wa Pato la Taifa ndani *(GDP)* na kupelekea utengenezwaji wa ajira maradufu. Katika mtazamo wangu, ni vyema Serikali isiongeze msingi wa kodi nchini kwa kupandisha viwango vya kodi. Hii inaweza kupelekea kupungua kwa uzalishwaji wa bidhaa na huduma kutokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji kupitia kodi dhahiri na isiyokuwa dhahiri.

Mheshimiwa Spika, katika aya ya 8 ya hotuba ya bajeti ni rahisi kugundua kuwa baadhi ya vipengele vya bajeti hii haviendani kabisa na kipindi cha majirio ya upungufu wa chakula kutokana na ukame na bei ya mafuta inayozidi kupanda kila siku duniani hivyo kumekuwa na mfumuko wa gharama za uzalishaji na uwasilishaji wa huduma katika uchumi wetu. Wizara ya Fedha ni vyema ikawa macho katika kutoa vichocheo kwa sekta zote za uzalishaji kiuchumi ili kuongeza ajira maradufu. Kuongezeka kwa kodi ama kwa kupitia Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)*, kodi ya mapato *(Income Tax)*, ushuru wa forodha na kadhalika kwa hakika vinazuia uongezekaji wa ajira katika uchumi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kurejea aya ya 31(iv) na kutoa pongezi kwa jitihada za Wizara ya Fedha kuweka msisitizo zaidi kwenye kuboresha utendaji wa idara ya forodha kwa kuongeza uwajibikaji, utumiaji na upunguzaji wa urasimu ambao umekuwa chanzo cha kukatisha tamaa kwa walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kurejea vile vile katika aya ya 39(ii) ambapo Waziri wa Fedha anasisitiza kuongeza viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji baridi kutoka shilingi 41.50 kwa lita hadi shilingi 45 kwa lita, bia inayotengenezwa kwa nafaka ambayo haijaoteshwa kutoka shilingi 150 kwa lita hadi shilingi 161, bia nyingine zote kutoka shilingi 256 kwa lita hadi 274 kwa lita. Hii ni bahati mbaya kwa viwanda vyote vya vinywaji kwamba Wizara ya Fedha itaendelea kuiongezea kodi sekta hii yenye ushindani mkubwa kibiashara. Ni dhahiri kuwa viwanda hivi vitaongeza bei za bidhaa zao kwa wateja wao wa rejareja ili kufidia gharama zilizoongezeka za kodi.

Hata hivyo itakumbukwa kuwa jumla ya bidhaa zinazozalishwa viwandani itapungua kutokana na jumla ya mahitaji ya bidhaa hizi kutoka kwa walaji kutokana na ukweli kwamba watumiaji wa bidhaa hizi hawatokuwa tayari kutumia senti zao chache walizonazo kununua vinywaji hivyo. Upunguaji wa bidhaa zinazozalishwa na viwanda hivi utakuwa ni mkubwa zaidi ya mapato ya kodi inayotarajiwa yaani, kwa kutoza kodi kubwa kwa kila lita ya kinywaji husika, hii itapelekea upunguaji wa mapato toka katika sekta hizi. Kinachosikitisha zaidi ni ukweli kwamba Wizara imeenda mbali zaidi kwa kulinda viwanda dhaifu kwa kuviwekea hatua za kiulinzi ilhali viwanda ambavyo vimekuwa vikiwekeza milioni za dola za Kimarekani katika vifaa vya raslimali zisizohamishika na sekta zenye kuajiri maelfu ya Watanzania zimeachwa pasipo msaada wowote. Hakuna hatua zozote ambazo zimechukuliwa kupambana na uingizaji haramu wa bidhaa za vinywaji toka nje ya nchi zenye chapa ya bidhaa zinazozalishwa humu nchini.

Mheshimiwa Spika, katika aya ya 41(vi) Wizara ya Fedha imeongeza ushuru wa forodha kwa bidhaa za viberiti vinavyoagizwa toka nje ya Afrika Mashariki kutoka asilimia 35 hadi asilimia 50. Ukiachilia mbali nia nzuri ya hatua hii, kitendo cha kutoa ulinzi kwa baadhi ya viwanda ni kitendo kinachoenda kinyume na sera ya Serikali ya soko huria na mwitiko wa Serikali kuwa na soko huria kiuchumi. Wakati bidhaa za viberiti vya ndani zitapata ulinzi wa Wizara ya Fedha, jumla ya maelfu ya Watanzania watatozwa kodi kubwa kwa kutumia bidhaa ya viberiti vya ndani ambavyo bei yake ni maradufu kutokana na gharama ya uzalishaji kuwa kubwa zaidi ukilinganisha na vile

vilivyoagizwa toka nje ya nchi. Kwa mantiki hiyo, jamii yote ya Watanzania inalazimika kulipia zaidi kutoka katika vipato vyao duni kununua viberiti vinavyozalishwa ndani ya nchi wakati wangeweza kutumia gharama ndogo kama wangepata bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuizungumzia aya ya 42 inayohusu zao la miwa. Haieleweki bayana kama aya hii inajumuisha sukari nyeupe iliyokwishasafishwa itumikayo viwandani *(Industrial Sugar)* katika kutengeneza vinywaji au la! Hata hivyo, ningependa kutahadharisha kwamba Serikali isianze kugawa mamlaka yasiyokuwa ya lazima kwa Bodi ya Sukari ya Tanzania, mamlaka ambayo yanaelekea kumlinda mkiritimba mmoja mkubwa katika Tanzania yaani *Kilombero Sugar Limited.* Ni ajabu kuona kwamba haya yote yanatokea katika wakati ambao ukiritimba umekuwa ukivunjwa na Serikali mbalimbali duniani kote. Hatua hii ya kutoa kinga inaenda kinyume na taratibu za soko huria ambazo Tanzania imejidhatiti kuhakikisha zinastawi. Tujiulize ni kwa nini *Kilombero Sugar* haiwezi kuwa mzalishaji mkubwa wa sukari duniani kwa ubora na ufanisi isipokuwa tu kwa Serikali kupandisha ushuru wa forodha wa bidhaa za nje ili *Kilombero Sugar* iwauzie walaji wa Tanzania bidhaa zake kwa faida zaidi? Bodi ya Sukari imefikia hatua ya kujichukulia mamlaka kwa kuviandikia baadhi ya viwanda barua za kuvitaka viwanda hivyo kununua sukari ya Kilombero. Kwa maoni yangu, Bodi ya Sukari sasa inatoka nje ya mamlaka yake kisheria. Nia ibaki kuwa ni kuendeleza viwanda vya ndani tulivyonavyo sisi, si kwa kuleta madhara ama kwa walaji au viwanda vingine ili kuhakikisha tu kiwanda fulani kinafanya kazi zake kwa kupata faida.

Mheshimiwa Spika, nikirejea katika aya ya 43 (i) kinachozungumzia nia ya Wizara ya Fedha katika kupunguza matumizi ya kifungu cha 19(2) cha Sheria ya Uwekezaji Tanzania, kitendo hiki kitaanzisha desturi za kutofuata kanuni za utawala bora. Tanzania haiwezi kuwavutia wawekezaji kuja nchini kwa kupitia sheria moja tu na baadaye kufuta au kupunguza matumizi ya Sheria ya Uwekezaji mara baada ya mwekezaji kuwa amewekeza nchini. Hatua hii siyo bora na inaweza kuleta shaka kubwa kuhusiana na uimara wa sheria ya uwekezaji katika nchi. Vile vile ni vigumu kuelewa ni kwa nini Wizara ya Fedha inakuwa na ubaguzi kati ya viwanda vinavyosafirisha bidhaa nje na vile vinavyoingiza bidhaa ndani katika suala la kodi. Serikali ni vyema ikajiondoa katika ubaguzi na badala yake iwe na mtazamo wa kutoa vichocheo kwa viwanda vyote ambavyo vinaongeza ajira nchini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ningependa kurejea aya ya 46 ambapo nashindwa kuelewa ni kwa nini mafuta ya injini za ndege yameondolewa katika kundi la kulipiwa kodi ilhali mafuta ya aina nyingine ya petroli hayajafanyiwa hivyo. Wakati inadaiwa kuwa mafuta ya injini za ndege yanaathiri wasafiri wa ndani na nje ya nchi, ukweli ni kwamba uwezo wa msafiri au mtumiaji wa huduma ya ndege kama usafiri ndiye anayeweza kumudu gharama ya aina hiyo ya usafiri. Naamini kuwa Wizara ya Fedha ifahamu kwamba mashirika mengi ya ndege duniani yameanzisha mfumo wa malipo ya ziada ya nishati kwenye bei ya tiketi wanazowauzia abiria wao na hakuna mahali popote duniani ambako imethibitika kuwa mahitaji ya usafiri wa anga yamepungua kutokana na malipo ya ziada ya tiketi ili kugharimia kodi ya mafuta. Badala yake matumizi ya usafiri

wa anga yanaongezeka kila kunavyokucha. Hata hivyo, aina zote za bidhaa za petroli zilizoorodheshwa katika aya ya 46 (ii) (a) hadi (ii)(c ) ni muhimu sana katika sekta ya uzalishaji wa bidhaa, gharama zake zitapelekea uongezekaji wa bei za bidhaa kwa watumiaji wa rejareja kutokana na gharama za uzalishaji kuwa maradufu. Hii itasababisha kuongezeka kwa gharama za maisha katika nchi na mwisho wake kupelekea jumla ya mapato ya kodi kwa Serikali kuwa duni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono bajeti ya Serikali ningependa kuchukua fursa hii kushauri kwamba Wizara ya Fedha iwe inafikiria mambo yafuatayo katika kupandisha au kupunguza viwango vya kodi kwa sekta mbalimbali: -

(i) Uamuzi wa kuongeza kodi kwa bidhaa ambazo zimekuwa na mafanikio ni kama kuziadhibu sekta hizo kwa maendeleo yake badala ya kuzipongeza kwa mafanikio yake kwa kuwa na wateja wengi ndani ya nchi.

(ii) Kutokuendeleza desturi za ushindani usiokuwa sawa nchini na tabia ya ukiritimba kwa baadhi ya sekta za viwanda.

(iii) Kukwepa uongezaji wa kodi kwa baadhi ya sekta tu kwani kutofanya hivyo kutapelekea shinikizo lisilokuwa la lazima kwa baadhi ya viwanda na kusababisha mfumuko wa bei za bidhaa za viwanda hivyo na kupungua kwa jumla ya mahitaji ya bidhaa na hatimaye kupelekea upungufu wa kodi itakayokusanywa.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu sura ya bajeti, kiasi kikubwa mno (64%) cha fedha za ndani bado kinakwenda zaidi kwenye matumizi kuliko kwenye maendeleo. Japokuwa bajeti ya Matumizi ya Kawaida imeshuka kwa asilimia 4 kutoka asilimia 35 hadi asilimia 31, bajeti ya maendeleo imeongezeka kwa asilimia moja tu kutoka asilimia 17 hadi 18. Mwelekeo huu siyo mzuri sana. Iko haja ya kuangalia upya matumizi ya Serikali kwa lengo la kuyapunguza ili fedha zaidi za ndani zitumike kwenye maendeleo.

Mheshimiwa Spika, fedha nyingi (60%) za Matumizi ya Kkawaida bado ziko Wizarani. Halmashauri zimetengewa asilimia 23 na Mikoa asilimia 2. Japokuwa kuna ongezeko la kuridhisha mwaka huu la fedha zilizopelekwa kwenye Halmashauri, bado iko haja ya kuongeza kasi ya kuzijengea Halmashauri uwezo zaidi ili fedha nyingi zaidi zipelekwe moja kwa moja huko. Fedha zilizopelekwa kwenye Halmashauri zimeongezeka kwa asilimia mbili toka mgao wa mwaka wa fedha uliopita.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2006/2007 haina tofauti sana na zile za miaka mitatu iliyopita. *Tradition* imekuwa ile ile ya kuongeza *a percentage, over and above* ya bajeti iliyotangulia. Matarajio mengine yalikuwa kuona mabadiliko ya sura ya bajeti kuendana na malengo ya Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejitahidi kupunguza deni la Taifa kwa kiasi cha kuridhisha. Kiasi kilichotengwa ni asilimia 3 tu ya bajeti yote. Hii ni hali nzuri kwa kuwa Serikali sasa inaweza kukopa fedha zaidi kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bajeti za Wizara, sekta au maeneo kumi yaliyopewa kipaumbele cha kwanza kwa wingi wa fedha kwa mtiririko ni, Deni la Taifa, Afya na Ustawi wa Jamii, Ulinzi, Miundombinu, Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, Fedha, Usalama wa Raia na Ufundi, Ofisi ya Rais na Baraza la Mawaziri na Mhasibu Mkuu wa Serikali. Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika imechukua nafasi ya 11 ilhali Mambo ya Ndani (Magereza) imechukua nafasi ya 12. Kuna umuhimu mkubwa wa fedha zilizotengewa Wizara kiasi kikubwa kushuka chini kuhudumia uzalishaji wa bidhaa na huduma badala ya kuishia kutumika huko huko katika Wizara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bajeti za mikoa, bajeti kwa ajili ya mishahara kwenye mikoa inatofautiana sana na kuleta hisia kwamba pengine takwimu siyo sahihi. Mfano, (a) Mkoa wa Mtwara kuwa na *wage bill* sawa na Mara na kubwa kuliko ya Mbeya.

Mheshimiwa Spika, uwiano baina ya bajeti ya mishahara *(PE)* na matumizi mengine *(OC)* ni mdogo. Kuna baadhi ya mikoa ina *PE* kubwa sana lakini imetengewa *OC* ndogo sana. Mikoa hiyo ni pamoja na Kilimanjaro, Morogoro, Ruvuma, Iringa na kadhalika ukilinganisha na mikoa kama Pwani, Mbeya na Singida ambayo tofauti baina ya *PE* na *OC* ni kidogo. Mikoa kutengewa *OC* ndogo sana ikilinganishwa na *PE* ni kumaanisha kuwa kuna watumishi wengi wanalipwa bila kufanya kazi stahili kwa sababu ya kukosa vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, mikoa karibu yote, ukiondoa Mwanza na Tabora ambayo imepunguziwa fedha za *PE* na *OC* na Shinyanga, Mbeya na Mtwara ambayo imeongezewa kidogo, imepewa asilimia ile ile ya mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa *subvention* pamoja na *General Purpose Grant* kimkoa kwa ujumla umefanyika vizuri. Umezingatia mahitaji pamoja na ukubwa wa mikoa husika. Pengine kungekuwepo haja ya kuiangalia mikoa ya Mwanza na Tabora kwa maana ya kuiongezea mgao maana ndiyo peke yake iliyopunguziwa mgao. Punguzo hili ni kubwa mno, Mwanza imepunguziwa takriban shilingi bilioni 25 na Tabora imepunguziwa takriban shilingi bilioni 15.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bajeti ya Halmashauri, kwa ujumla kuna tofauti kubwa ya mgao wa fedha za ruzuku baina ya Halmashauri ndani ya mkoa mmoja. Kila mkoa ukiangalia kuna Halmashauri zilizopata ruzuku kubwa sana na nyingine ruzuku kidogo sana. Katika Halmashauri za Wilaya za Mikoa ya Arusha na Manyara kwa mfano, Ngorongoro, Babati na Simanjiro zimepata mgao kidogo zaidi. Mkoa wa Tanga, Pangani na Kilindi zimepewa ruzuku kidogo sana ukilinganisha na Halmashauri nyingine. Mafia nayo ingestahili kuongezewa zaidi.

Halmashauri za Mikoa ya Tabora na Lindi kwa ujumla zimegawiwa ruzuku kidogo zaidi ukilinganisha na Halmasharui za Wilaya nyingine. Masasi na Mbinga zimepata ruzuku kubwa mno ukilinganisha na Halmashauri nyingine kwenye mikoa husika. Mkoani Iringa, Ludewa, Makete na Kilolo pia mgao wake ni mdogo. Mikoa ya Kanda ya Ziwa kwa ujumla mgao wake ni *more even* isipokuwa tatizo bado ni lile lile la uhusiano usioridhisha baina ya *PE* na *OC.*

Karibu Halmashauri zote zimepata kiasi kidogo *(relatively)* zaidi za *OC* ukilinganisha na *PE.* Maana yake ni kwamba, Halmashauri nyingine watumishi watakuwa na vitendea kazi pungufu, hivyo kupelekea watumishi wengi kulipwa mishahara bila kufanya kazi kwa ufanisi unaotarajiwa. Halmashauri zilizoathirika zaidi ni pamoja na Jiji la Mwanza, Ukerewe, Kwimba, Manispaa ya Shinyanga, Musoma na Bukoba, Kishapu na karibu Halmashauri zote za Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Spika, bajeti kwa ujumla ni nzuri, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja.

Aidha, ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Zakia Meghji, kwa kuwasilisha hoja vizuri, imeeleweka vema.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba katika Ilani ya CCM ya mwaka 2005, pamoja na mambo mengine umakini mkubwa uwepo katika kuwezesha *SACCOS* za makundi mbalimbali ya jamii, hasa namna ya kufaidi mikopo ya benki.

Mheshimiwa Spika, benki zinatoza riba kubwa wakati *SACCOS* zinaanzishwa kwa mitaji midogo ya wananchi wanaojiunga pamoja. Nashauri liwepo fungu maalum la kukopesha *SACCOS.* Fungu hilo pia liwe na riba nafuu sana tofauti na mikopo ya biashara vinginevyo *SACCOS* zitakufa ama zitafilisiwa na wananchi watazichukia na kuikejeli sera nzuri ya CCM. Wakati wa majumuisho, naomba majibu ya Mheshimiwa Waziri katika hili.

Mheshimiwa Spika, pili, siungi mkono suala la kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye mawasiliano ya huduma ya simu za mkononi kutoka asilimia 5 hadi 7. Katika hili nashauri tutofautiane na wenzetu wa Afrika Mashariki. Sisi bado tunataka kuona wananchi wengi wanakuwa na simu zao wenyewe ambapo bado ni wachache wanaomiliki simu hizo. Ukitaka kuthibitisha hili, ujumbe wa bure wa tafadhali nipigie na naomba uniongezee fedha unashabikiwa sana kwa sababu wananchi wengi bado hawana uwezo wa kumudu hata hiyo asilimia 5 iliyopo.

Mheshimiwa Waziri, chonde chonde usiongeze ushuru. Nashauri Serikali itafute chanzo kingine cha mapato.

Mheshimiwa Spika, tatu, naipongeza Serikali kwa kudhamiria pamoja na mambo mengine kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma hasa kwenye Halmashauri za Serikali za Mitaa, pia kuunda kitengo maalum cha kufuatilia kwa karibu matumizi ya fedha hizo. Ni kweli matumizi mabaya yanajitokeza kwenye halmashauri za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, napendekeza hatua kali zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kurekebisha sheria za fedha na za kazi kwa ujumla. Mtumishi au mtendaji anapogundulika na kuthibitishwa amepoteza fedha ama amejipa mkopo badala ya

masurufu, sheria iangaliwe upya na taratibu za haraka ziwepo.  Kesi za wizi mahakamani haziishi, zinachukua muda mrefu.  Hili ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, nne na mwisho, suala la mazingira na namna ya kuyahifadhi lipanuliwe zaidi.  Serikali imejitahidi sana kupunguza ama kuondoa ushuru/kodi katika mafua ya taa na gesi na mitungi yake.  Hii ni hatua nzuri sana.  Hivyo, napendekeza yafuatayo: -

(i) Katika kutunza mazingira iwepo kampeni nchi nzima, mijini na vijijini ili wananchi waelewe vizuri, waulize maswali  na wajibiwe kwa usahihi.

(ii) Wananchi hasa wanawake waishio vijijini na familia zenye uwezo mdogo, siamini sana kama zimesaidiwa.  Hawa ni watumiaji wa kuni sana na kwa uchache mkaa. Sababu ni uwezo, hali ya nyumba zao na neno lenyewe gesi na mafuta ya taa ni mageni kwao.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwenye bajeti ya kilimo kupitia Wizara mbalimbali kuwepo utaratibu wa upandaji miti kila kaya, makundi na kadhalika na uangaliwe kwa karibu ili kudhibiti upungufu wa miti.  Itakuwa vigumu kuwazuia wananchi wasitumie kuni na mkaa kwa sababu hakuna/umepunguza ushuru/kodi ya gesi na mitungi na mafuta ya taa, mara moja.  Naamini miti hiyo itasaidia kupunguza upungufu wa miti inayotumiwa bila kurudishiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba majibu ya Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana. Ahsante sana.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kupitia Chama cha Mapinduzi kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Awamu ya Nne.  Nampongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania.  Pia, nampongeza Mheshimiwa Edward  Lowassa, kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mbunge na hatimaye kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu na kuthibitishwa na Bunge lako kwa kura nyingi.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe kwa kuchaguliwa kuwa Spika. Nampongeza Mheshimiwa Zakia H. Meghji, kuwa Waziri wa Fedha.  Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, naomba nitoe ushauari kwa lengo la kuboresha hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri katika maeneo yafuatayo: -

(i) Katika ukurasa wa 26 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Mazingira ibara ya 28, napongeza Serikali kutenga shilingi bilioni 9.4 katika bajeti ya mwaka 20006/2007 kwa ajili ya utekelezaji wa mkakati wa kutunza mazingira.

Ushauri wangu ni kwamba, ili fedha hizo ziweze kuwa na msukumo na kuzaa matokeo yatakayoonekana na ya kuridhisha, ni vema mwongozo kuhusu maeneo muhimu ya utekelezaji yabainishwe bayana Kitaifa, Kimikoa, Kiwilaya na Vijijini.  Nashauri

vikundi vya akinamama na wanafunzi wa shule wawe walengwa katika mgao wa fedha katika upandaji miti. Nguvu kazi vijijini ni akinamama na vijana.

(ii) Katika ukurasa wa 25, Uwezeshaji ibara ya 26 (vi) kuiwezesha *TIB* kutoa mikopo ya uzalishaji kwa viwanda, kilimo na utalii, naipongeza Serikali kwa hatua hii ya kimapinduzi ya kiuchumi kwa wananchi. Hata hivyo mikopo hii itakuwa kwa wenye uwezo wa kifedha kama vile wenye viwanda na kadhalika.

Ushauri wangu ni kwamba Benki ya Wanawake ndiyo ukombozi wa akinamama ambao ndiyo walio wengi na wanaobeba mizigo ya familia zao na Taifa kiuchumi. Benki hii isaidiwe kwa kupata mtaji wa kutosha ili iweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake. Naunga mkono hoja.

**MHE. RICHARD S. NYAULAWA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kwa matayarisho ya kina na mazuri. Hotuba yake ilieleweka vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa Wizara kupunguza ushuru kwenye karatasi zinazoagizwa kutoka nje kwa matumizi mbalimbali kama vile kuandikia na kuchapisha makala za magazeti kutoka asilimia ishirini na tano hadi asilimia kumi, ibara ya 41(iv).

Karatasi zenye *code number HS 4802: 55:00, HS 4804: 11: 00, HS 4810: 51:00* na *HS 4811:51:00* zimetajwa na kuonyeshwa waziwazi kwenye bajeti. Lakini *code number HS 4801:00:90* ambazo ni kwa karatasi za kuchapisha magazeti haijatajwa na kuonyeshwa bayana kwenye bajeti. Kwa hiyo, Maafisa wa Forodha hawatapunguza ushuru wa fedha.

Mheshimiwa Waziri, naomba *code number HS 4801:00:90* ya karatasi za magazeti uliingize kwenye hitimisho ya hotuba ya Wizara yako.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani zangu, ahsante.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kupongeza mwelekeo na maudhui ya hotuba za Wizara zote mbili yaani Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Nawapongeza Mawaziri wote pamoja na watendaji walio chini ya uongozi wa Wizara hizi.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuzungumzia huduma za Hazina Ndogo. Madhumuni ya kuanzishwa Hazina Ndogo kwenye kila Mkoa naamini yalikuwa kurahisisha malipo ya Serikali Mikoani. Aidha, madhumuni mengine yalikuwa kudhibiti fedha za umma zisifujwe vibaya.

Mheshimiwa Spika, yawezekana kwa kiasi fulani hili limewezekana. Hata hivyo, yapo matatizo yanayotokana na suala la *cash budget.* Yapo matatizo yanayozisibu Ofisi

za Wakuu wa Wilaya na hasa zile Wilaya ambazo zipo mbali na Makao Makuu ya Mikoa. Hutokea Mhasibu katika Ofisi ya Katibu Tawala wa Wilaya *(DAS)* anapofuatilia hundi na malipo katika Ofisi za Hazina Ndogo mara nyingi hakuti hundi zikiwa tayari. Hivyo analazimika kulala. Lakini bahati mbaya aliyonayo mhasibu huyu ni kwamba katika bajeti hakuwekewa kifungu cha posho (masurufu) ya kujikimu anapofika Hazina Ndogo na kubaini kuwa malipo hayajawa tayari.

Mheshimiwa Spika, nashauri ama wahasibu hawa wawekewe kifungu cha masurufu ili wanapokuta hakuna malipo yaliyo tayari waweze kujikimu au huduma za Hazina Ndogo zishushwe hadi kwenye ngazi ya Wilaya. Kuwe na Hazina Ndogo ngazi ya Wilaya ili kurahisha malipo ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa angalizo kwenye uchakavu wa pesa hususan noti na sarafu. Hapa inabidi nizungumzie uchakavu wa noti na sarafu katika Mkoa wa Kigoma. Uchakavu wa noti na sarafu unasababisha usumbufu tangu kwa wafanyabiashara na wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, Kigoma tunazo benki tatu muhimu ambazo ni *NBC*, *NMB* na *CRDB.* Bahati mbaya ni kwamba zinakuwa na kigugumizi cha kupokea noti na sarafu zilizochakaa. Hoja wanayotoa ni kwamba wao sio wakala wa Benki Kuu. Wanajenga hoja kuwa Serikali ihimize Benki Kuu iongeze matawi ili kushughulikia uchakavu wa sarafu na noti pia.

Mheshimiwa Spika, tatizo la maeneo ya vijijini yanasababishwa na watumishi kutokuwa na huduma za kibenki. Serikali hapo mwaka 2004 ilitoa agizo ambalo limeanza kutekelezwa kwa kusababisha matatizo kwa watumishi. Agizo hilo ni la watumishi kupokelea mishahara benki. Watumishi hususan walimu wanapofuata malipo (mishahara) benki Wilayani, hukwamisha masomo kwa wanafunzi. Watoto wanakosa masomo pengine kwa zaidi ya siku tano hadi wiki kwani walimu wanakuwa nje ya vituo wakifuata mishahara. Kwa hali hiyo, nashauri ama mabenki yahimizwe kufungua matawi kwenye ngazi chini ya wilaya au waanzishe *mobile unit system* ya huduma za benki.

Mheshimiwa Spika, naamini kwa ushauri huu uchumi wa Taifa letu utaweza kwenda mbele ikiwa utazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuunga hoja zote mbili mkono na kuziafiki.

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Spika, niliwahi kuandika dokezo kwa Waziri Mkuu na kwa Waziri wa Kilimo na Chakula na Waziri wa Ushirika na Masoko kuhusu mbolea ya ruzuku.

Mheshimiwa Spika, nilieleza kuwa utaratibu wa mbolea ya ruzuku unadumaza kilimo. Unafanya watu/wakulima waweke matumaini makubwa kwenye upatikanaji wa mbolea ya ruzuku. Ukweli ni kwamba mbolea hiyo kama mkulima atapata kihalali basi itakuwa kilogramu 10 au chini ya hapo. Mtu anayetegemea kilimo, hakika kilogramu 10

hawezi kulima kwa lengo la kujitosheleza kwa chakula na ziada auze ili apate fedha kwa shughuli nyingine.

Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 21 kwa mbolea ya ruzuku, dawa na mbegu bora. Maana yake ni kuwa mbolea inaongezeka kutoka tani 63,000 za mwaka 2005/2006 hadi pengine tani 100,000 kwa mwaka 2006/2007. Fedha imeongezeka kutoka shilingi bilioni 7.5 hadi hizo shilingi bilioni 21.

Mheshimiwa Spika, kiwango hicho cha fedha kinaonekana kuwa ni kikubwa. Ukweli ni kuwa ni kidogo sana. Mbolea ni bidhaa aghali sana. Fedha hii itawafaa wakulima kisaikolojia tu. Ongezeko la uzalishaji halitakuwa kubwa. Hata mfanye nini, usambazaji wa mbolea ya ruzuku ni mgumu sana. Unaleta rushwa, wizi na mbaya zaidi walengwa hawafaidi na kilimo kinavurugwa. Watu wanalima sana kwa mategemeo ya kupata mbolea hiyo. Wakati ukifika badala ya wakulima kununua hiyo mbolea, wanaanza kufukuzana na hiyo mbolea hadi msimu unapita.

Mheshimiwa Spika ushauri wangu ni kwamba, Serikali itafute makampuni yanayotengeneza mbolea ili walete mbolea hii nchini kwa wingi kufuatana na ushauri wa kitaalam kutoka kilimo. Mbolea hii iende kwenye kanda mbalimbali kutegemea na aina za udongo na mahitaji.

Mheshimiwa Spika, fedha hiyo ipelekwe kwenye benki kama *NMB, CRDB, SELF, SCULT* na Benki za Wananchi mahali ambapo zipo. Kuna *SACCOS* nyingine ni kubwa sana nazo zikope fedha hizo. Wananchi nchi nzima wahamasishwe kuanzisha *SACCOS* zao. Fedha hii itumike kukopesha *SACCOS* hizi kufuatana na shughuli wanazotaka kufanya. Maeneo ambayo ni ya kilimo basi *SACCOS* hizo zikopeshwe kwa lengo hilo. Maeneo kama Njombe wananchi wanalima mwaka mzima. Mtindo huu wa ruzuku wanalima mara moja tu na wanatakiwa kulima mahindi tu. Kumbe wangekuwa na mikopo kwenye *SACCOS* zao wangelima mahindi, viazi, maharage, njegele na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, wananchi wangekuwa wanaanza kuzoea kuweka na kukopa. Watu wangeanza kununua vifaa vya kisasa vya kilimo na kuachana na jembe la mkono. Wakulima wangeanza kutumia mbegu bora na kilimo cha maksai. Vijana wangepata ajira kwa sababu mtaji upo. Usumbufu wa kukimbizana na mbolea ungekwisha, rushwa ingekoma, wizi ungekwisha, uzalishaji ungeongezeka mara moja. Wananchi wangejifunza kuweka na kukopa. Fedha ya Serikali isingepotea moja kwa moja kama ilivyo sasa. Baada ya muda Serikali ingeacha kutenga fedha kwa ajili hii. Nawasilisha.

**MHE. USSI AME PANDU:** Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa ushindi wa kishindo, pia nitoe pongezi kwa Waziri Mkuu naye kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi za Wabunge.

Mheshimiwa Spika, lakini pia na wewe nikupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge hili kwa kura nyingi za Wabunge, pia niwapongeze Wabunge wote ambao wamepata heshima ya kuchaguliwa kuwa Wabunge wa Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kwa kutowashukuru wananchi wa Jimbo langu la Mtoni, Zanzibar ambao wamenichagua kwa kura nyingi na kunipa heshima ya kuwawakilisha katika Bunge hili. Naomba niwashukuru wote kwa heshima waliyonipa.

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue nafasi hii kwanza kuzipongeza hotuba zote mbili zilizotolewa, ile ya Wizara ya Fedha na ile ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kwa jinsi uchumi wetu unavyokua kama tulivyoona mwaka 2006/2007 - 2007/2008 na mwaka 2008/2009. Vile vile, bajeti hii ilivyoonyesha kutaka kumsaidia mtu wa chini pamoja na kuondoa umaskini kwa watu wote na kwa maana hiyo, lile lengo la awamu hii ya nne la kusema Tanzania ni yenye neema tele, maisha bora kwa kila mtu yatawezekana.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie mambo mawili nayo ni *TRA* na Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TRA*, chombo hiki kwanza nataka nikipongeze sana kwa jitihada zake za kukusanya mapato mpaka kuvuka lengo lile ambalo liliwekwa, lakini pia chombo hiki kinahitaji baadhi ya mambo yake yafanyiwe marekebisho ili kuondoa baadhi ya kero ambazo watu wa Zanzibar huwa wanazipata pale wanapoleta magari yao Tanzania Bara na yakawa yanakamatwa na maafisa wa *TRA* au pale Wazanzibari wanapoleta bidhaa zao na wakatakiwa kulipa fedha kwa mara ya pili wakati Zanzibar wameshalipia.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili ni kero ndani ya Jamhuri hii ya Muungano. Mheshimiwa Rais wetu ameshaagiza kwamba kero zote ndani ya Muungano zirekebishwe, tatizo hili ni kwa nini halirekebishwi? Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika kikao kilichopita alikubali na alikiri kwamba kweli ndani ya *TRA* kuna mapungufu na alisema kwamba tayari ameshaunda Tume na kwenye kikao cha bajeti taarifa ikatolewa kuhusu tume hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini la kushangaza ni kwamba mpaka leo hii Mheshmiwa Waziri bado hajaeleza lolote! Hivyo, ninamuomba Mheshimiwa Waziri atakaposimama kujibu hoja za kuchangia bajeti ya Wizara yake atueleze hiyo tume aliyounda imefikia hatua gani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, nachukua nafasi hii pia kuipongeza Wizara hiyo kwa jinsi ilivyotoa changamoto katika kukuza kiwango cha elimu nchini kote, hasa kwenye Vyuo Vikuu ambako watu wengi sasa wanajitokeza hasa pale Wizara ilipoamua kutoa mikopo na kuwakopesha wanafunzi wa Vyuo Vikuu mbalimbali ili tuweze kukuza wataalam katika nchi yetu. Hivyo, naiomba Wizara hii katika bajeti yake kama kuna uwezekano hasa kwenye mikopo ikaongezwa kusudi wanafunzi wengi wafanikiwe na kupata mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuo cha Taasisi ya Bahari kilichopo Buyu, Zanzibar, mwaka jana fedha ambazo zilitengwa kwa ujenzi wa chuo hicho hazikupatikana, hivyo naomba fedha ambazo zimetengwa kwa bajeti ya mwaka huu Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba zinapatikana na ujenzi ambao unaendelea kwa kasi ndogo uweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, mwisho nimalizie kwa kukushukuru kwa kuchangia kwangu kwa maandishi na naunga mkono hoja hii kwa asilimia zote.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Spika, naomba nami nichukue nafasi hii kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhusu Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2006/2007.

Miongoni mwa mambo ambayo yameelezwa katika hotuba hiyo kwamba yatazingatiwa ni pamoja na uwezeshwaji wa wananchi. Nia na madhumuni makubwa ya zingatio hili ni kuhakikisha kwamba kila Mtanzania anapata fursa zitakazomwezesha kuishi maisha bora.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeahidi kuimarisha mifuko iliyopo ya dhamana ili wananchi wengi waweze kutumia kujiletea maendeleo. Kadhalika taratibu zitakamilishwa na kuanzisha mfuko wa dhamana kwa mikopo ya maendeleo ili mfuko huo uweze kutoa dhamana ndani ya mwaka huu wa fedha. Azma hii ni nzuri hasa ukizingatia kwamba wananchi wengi wa Tanzania hawana mitaji ya kuzalisha ili kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mbalimbali kutoka kwa baadhi ya wananchi na hasa wafugaji kwamba hawafaidiki na mfuko huu. Utaratibu uliopo ni kwamba mifuko ya dhamana inasimamiwa na Benki Kuu ambapo mfugaji naye kama pangekuwa na utaratibu mzuri angeweza kutumia fursa hii kwa ajili ya kukopa na kuendeleza ufugaji wa kibiashara. Kwa bahati mbaya, benki ndizo ambazo zimepewa maamuzi kuamua ni wateja wa makundi yapi wakopeshwe. Benki za kawaida nazo hazijaandaa utaratibu wa kuwakopesha wafugaji kutokana na visingizio mbalimbali. Katika hali kama hii ni dhahiri kwamba wafugaji hawatofaidika na mikopo hii.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii basi kuishauri Serikali kuandaa utaratibu madhubuti na unaoeleweka utakaowapa fursa wafugaji nao kufaidika na mikopo ya namna hii ili nao waweze kuongeza kasi ya uzalishaji, kwani ushiriki wa wananchi akiwa mmoja mmoja au kwa vikundi katika uzalishaji ni jambo la msingi katika ukuaji wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa inasifika sana na wengine pia tunajisifu kwamba ni kisiwa cha amani na utulivu. Huu umekuwa ni wimbo wetu kila uchao. Amani na utulivu haviji hivi hivi tu, bila shaka kuna misingi yake. Msingi mkuu wa amani katika nchi yoyote ile ni lazima haki za binadamu ziheshimiwe na pili nchi iwe inaongozwa kwa misingi ya kufuata sheria na utawala bora. Katika msingi huo basi, Serikali huwajibika kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, katika awamu za uongozi zilizopita chini ya mfumo na utawala wa chama kimoja, ilikuwa ni nadra sana kusikia au kuona chaguzi za nchi zinatawaliwa na vurugu, raia kupigwa, kuuliwa, kunyanyaswa na kunyang'anywa mali zao. Chaguzi zilikuwa tulivu na kwa hivyo utulivu na amani ya nchi vilikuwa haviteteteki.

Mheshimiwa Spika, hali ilivyo sasa hivi ni kinyume kabisa, imekuwa ni jambo la kawaida chini ya mfumo wa utawala wa vyama vingi kushuhudia chaguzi zinazotawaliwa na ukiukwaji wa kiwango cha juu wa haki za binadamu. Raia wananyanyasika, wanapigwa, kunyang'anywa mali zao na hata kuuliwa. Mifano ipo mingi, lakini si vyema kukumbusha kilio matangani.

Nathubutu kusema kwamba baadhi ya wananchi wameanza kuziogopa chaguzi kwa kuhofia kukumbwa na maafa mbalimbali kama nilivyoeleza hapo awali. Hali hii ni ishara tosha kuona kwamba sasa ile sifa yetu ya amani na utulivu na kwamba Serikali inaongoza kwa msingi ya utawala bora na kuheshimu haki za binadamu inamomonyoka. Hii ni dosari kubwa na kwamba tunaipaka matope sura njema ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nadhani sasa umefika wakati dosari hii tuitafakari kwa kina ili tuipatie dawa ya kudumu ikiwemo kuvumiliana kisiasa ili hatimaye tuendeshe chaguzi zetu kwa amani, utulivu na kuheshimu haki za binadamu. Tuanze leo pamoja na kwamba tumeshachelewa. Ahsante.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia bajeti kwa kuunga mkono hoja za Mawaziri kwa bajeti nzuri ambayo ni yenye matumaini kwa wananchi wa Tanzania. Mafanikio ya kila nchi ni makusanyo ya mapato. Vyanzo vya mapato ni vingi, lakini maeneo mengine huzorotesha makusanyo kwa kutoa msamaha kwa ajili ya kupata asilimia ya mapato. Kwa kuwa tegemeo letu ni kodi, sasa umefika wakati wa kuangalia namna ya kuongeza mapato ili tupunguze utegemezi wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo ningependa kuzungumzia ni suala la mikopo kwenye mabenki yetu. Mikopo inaweza kupunguza umaskini, lakini masharti ni magumu hasa kwa wananchi wa kawaida. Kuna benki nyingine ambazo wanakopesha wananchi walio karibu na maeneo ya mijini, walioko vijijini hawapati mikopo eti kwa sababu wako mbali na mabenki. Imefika wakati wa kuwatambua kwani huko ndiyo kuwa maskini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu msamaha wa dawa za mifugo, tunashukuru kwa kusamehe kodi. Pamoja na msamaha huo, bado dawa ni bei juu sana, naomba kujua ni nani anayedhibiti bei ya dawa kwani bado ni kubwa. Namna ya kuwasaidia wananchi kiuchumi, ni afadhali kuwasaidia wananchi ambao wameanzisha *SACCOS* ili ziwasaidie wananchi wengi.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo hapa nchini ambayo yako nyuma kimaendeleo. Wizara ya Fedha ingefaa kuangalia jinsi ya kuwajengea nyumba nafuu ili watu wa hali ya chini waweze kunufaika.

Mwisho, mimi binafsi naipongeza sana *TRA* kwa kazi kubwa ambayo wamefanya tangu ianzishwe na kuongeza mapato yetu toka shilingi bilioni 25 hadi shilingi bilioni 160 kwa mwezi. Hiyo ni juhudi kubwa ambayo kama si ubinadamu wasingetuhumiwa. Utekelezaji wa miradi na kuongezeka kwa mishahara ni kwa ajili ya kazi yao. Nchi hii isingewezekana kuendeshwa kama siyo makusanyo ya *TRA.* Kwa kuwa kuna baadhi ya viongozi au watu wa kawaida ambao hawaoni juhudi za *TRA*, basi wasameheni bure. Nawapongeza sana, ongezeni bidii kwani hata mgonjwa anapotibiwa hulia, lakini baadaye hushukuru kwa kupata tiba hiyo.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote mbili kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba nijibiwe masuala yafuatayo, kwanza Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji inazisaidiaje Wizara nyingine kuhusu mipango yake na kwa nini Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji isiunganishwe na Wizara ya Fedha kama ilivyokuwa zamani?

Pili, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ina mipango gani ya kuzisaidia Wizara hasa ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi?

Tatu, je, Makamishna wa Tume ya Mipango kwa sasa wana umuhimu gani?

Mheshimiwa Spika,nne, kwa upande wa Sekta ya Kilimo tunazo hekta milioni 22.3 zenye uwezo wa kuendelezwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwa kuanzia, je, ni nini Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji imepanga kuhusu kuziendeleza au kutumia eneo hilo kwa ajili ya umwagiliaji ili kuongeza chakula pamoja na ziada ya kuuza nje ili kupata fedha za kigeni?

Tano, kwa kuwa matumizi ya mbolea hapa nchini ni kilo saba tu kwa hekta badala ya kilo 60 kwa hekta zilizopendekezwa na wataalam; je, Wizara ya Mipango inaisaidiaje Wizara ya Kilimo ili kilimo kiwe na tija?

Mheshimiwa Spika, sita, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, inasema nini kuhusu usindikaji wa mazao, ili tutoke asilimia 13 ya sasa angalau tusogee kwenye asilimia 20 kama walivyo Kenya asilimia 25?

Mheshimiwa Spika, nawapongeza *TRA* kwa kuweka utaratibu mzuri kwa upande wa mizigo inayotoka nje kwa kutumia teknolojia ya kisasa *(The new technology of assessing and collecting import duties of ASYCUDA)* tuliyoona Zanzibar, lakini Dar es Salaam *headquarter* bado haijaanza kutumika, je, utaratibu huo mzuri utaanza/utawekwa lini?

Kuhusu ubinafsishaji umetupatia mapato makubwa zaidi ya shilingi bilioni 33.309, lakini umeongeza ajira ngapi kwa vijana wetu wasomi au wangapi wamekuwa wahanga wa ubinafsishaji tulioufanya *declared redundants?*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kauli ya Rais wetu na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ni kujenga mazingira mazuri ya kuzalisha ajira mpya, hii haina maana kwamba ajira hizo zipo au zitatoka Ikulu au ndani ya CCM, Mfano, KAMATA ya zamani jijini Dar es Salaam hadi *airport* tumebinafsisha viwanda vyote, mbaya zaidi hao wawekezaji badala ya kuviendeleza viwanda tulivyowakabidhi wao wamefungua maduka ya samani *(furniture), show rooms* za magari mapya au mitumba.

Samani, magari yanayouzwa yote yanatengenezwa kwao na wanaingiza vitu hivyo nchini kwa soko la mauzo tu, tena kwa bei ya mamilioni ambayo kwa mtu wa kawaida hawezi kuvinunua. Hapa ubinafsishaji umejenga tabaka la walionacho na wasionacho. Mbaya zaidi ni kufunga kabisa viwanda hivyo na kufungua *show rooms.* Watu wengi wanapoteza ajira, hivyo mazingira mazuri ya kuongeza ajira kama Ilani inavyosema inakuwa haipo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuiomba Serikali, ubinafsishaji ni milango ya ajira mpya, wawekezaji wanapokuja katika mikataba iwabane na iseme:-

(i) Watakiendeleza tulichowabinafsishia;

(ii) Ajira za Wazalendo zilindwe kwa asilimia fulani na kwa masharti ya kazi *(scheme of services)* yanayolenga kuwaendeleza kitaaluma, kwa teknolojia ya kisasa, kwa mafunzo ya *inhouse training* au kuwapeleka huko huko kwao; na

(iii) Itajwe na kusisitizwa, wazalenzo lazima wawe na hisa ya asilimia fulani kwa kiwanda kinachobinafsishwa.

Kwa hiyo, jukumu la kwanza la mwekezaji wa kigeni iwe kumtafuta *partner* mzalendo wanayemkubali kwa njia zao wenyewe kupitia orodha ya wawekezaji wazalendo.

Msamaha wa magari ya kazi *(page 46 - utility vehicles)* nao ufutwe, kama ilivyo kwa magari madogo bonafsi *(non utility)* kwa sababu wawekezaji wengine baada ya kuyatumia kwa muda magari hayo huuzwa kienyeji kwa bei ya magari mitumba tena kwa bei kubwa na wao kuagiza tena magari eti ni magari ya miradi.

Mheshimiwa Spika, sheria ya ajira migodini *(page 47)* zinatisha, dereva Mwafrika wa kijiko cha kuchambulia mchanga wa madini analipwa mshahara wa shilingi 150,000 kwa mwezi lakini dereva Mzungu wa kijiko hicho hicho na gia hizo hizo mshahara wake shilingi 3,000,000 na *weekend allowance* ya shilingi 300,000. Usawa uko wapi wakati pesa yake haitozwi kodi?

Msamaha wa *VAT* kwa vipuri vya treni *(page 8)* sasa uelekezwe kwenye vifaa vyote vya mahospitalini (huduma za tiba) kama vile *ultra sound* na magonjwa ya upasuaji wa moyo kwani msamaha huo ulikuwa ni wa kutaka kuiokoa *TRC* ambayo ilikuwa dhoofu bin taaban kwa uchakavu mkubwa wa treni yenyewe na vitendea kazi, sasa inakodishwa hivyo Serikali isijiingize tena yatakuwa yale yale ya *TANESCO* na *DAWASA.*

Mheshimiwa Spika, msamaha wa *VAT* katika mafuta ya ndege *(page 48) (JET A1* na *AV gas)* ni kwa ndege zote za Mataifa ya nchi za nje au ni kwa ndege za hapa? Lakini je, baada ya msamaha huo nauli za ndege zetu zitashuka?

Mwisho, naomba Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji mwakani ipange mipango namna gani itaboresha elimu ili tuweze kuwekeza katika elimu. Mafuta yetu Watanzania kwa sasa ni watu, tusomeshe watu wetu, tujenge nyumba za walimu, vifaa na kadhalika. Yote yatafanikiwa tukiwa na watu waliosoma vizuri.

Mheshimiwa Spika, Tanzania yenye neema inawezekana. Naunga tena mkono.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja ya Wizara ya Fedha 2006/2007 katika maeneo yafuatayo: - (i) Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake na hata katika hatua mbalimbali za marekebisho ya kodi na ushuru hajagusia maeneo muhimu kama vile vifaa vya ujenzi, bei ya bati, sementi, misumari na mbao, imeendelea kupanda kwa kiwango cha kutisha cha kuwafanya wananchi wengi wa hali ya kawaida kushindwa kujenga nyumba zenye kustahili hadi ya binadamu na/au inayoendana na karne ya sayansi na teknolojia. Je, sababu zipi za msingi zinaifanya Serikali kufuta kabisa kodi na ushuru mbalimbali katika vifaa hivi muhimu kwa nia ya kuwasaidia wananchi katika vita dhidi ya umaskini?

(ii) Watanzania wengi hasa wa vijijini wameanza kuhamasika na kujiunga na kujinunulia simu za mkononi *(cellular phones).* Hali halisi inaonyesha kuwa simu hizi zimerahisisha sana mawasiliano kati ya wananchi siyo tu kwa shughuli za kibiashara bali pia za kijamii. Mawasiliano ni kitu muhimu sana katika kujenga mshikamano, udugu na umoja baina ya wananchi. Sababu zinazotolewa na Serikali kuoanisha viwango na vya Kenya na Uganda si ya msingi kwa vile tunatofautiana sana katika mambo ya msingi kama vile viwango vya *VAT.* Naishauri sana Serikali, ili kuwapa motisha Watanzania wengi zaidi, kodi na ushuru wa simu siyo tu ipunguzwe bali ifutwe kabisa ili watu wengi zaidi wajiunge.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani za dhati.

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri wa Fedha, Manaibu Mawaziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kutokana na hotuba nzuri na yenye kulenga jamii ya wananchi wa chini ambao ndiyo wengi katika Taifa hili na ndiyo nguvu kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato ya ndani kutoka ukurasa wa 27 - 29 kipengele (i) - (vi) nimekubaliana nao kabisa na ninaunga mkono uwepo tu usimamizi thabiti pamoja na ufuatiliaji, nina imani kubwa ya mafanikio makubwa sana. Hii isiwe kwa maandishi tu bali iwe kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa bandari zetu usimamizi wake si wa kuridhisha hususan bandari ya Dar es Salaam, wizi ni mkubwa na urasimu. Wafanyabiashara wanalalamika kwa urasimu mkubwa wa utoaji mali zao na kufikia hadi kushindwa. Gari

kuibiwa vifaa ni suala la kawaida na hakuna hatua zozote zinazochukuliwa. Hali hii inasababisha wafanyabiashara wanakwepa kupitisha baadhi ya biashara zao bandarini. Hii itatukosesha mapato na lile lengo lililokusudiwa halitofikiwa. Naomba Serikali ichukue hatua za makusudi ili kuondoa kasoro hizo zilizojitokeza kwa muda mrefu hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maslahi ya wafanyakazi, mara nyingi au kila mwaka fedha huongezwa kwa wafanyakazi, lakini kila fedha zinapoongezwa bidhaa nazo hupanda kwa kasi kupita kile kiwango cha matumizi alichoongezewa mfanyakazi. Kwa hali hii mfanyakazi haoni tija ya kuongezwa fedha hizo yaani bado hajakomboka kimaisha.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba, mfumuko wa bei kwa bidhaa kiholela lazima udhibitiwe. Kuna baadhi ya biashara hazina ushuru lakini uuzaji wa mfanyabiashara anauza kama aliyetozwa kodi. Iwapo hakuna udhibiti wa biashara mfanyakazi hatafaidika na nyongeza hizo na wala hatoweza kumudu maisha ya kila siku.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kwa njia ya maandishi kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kwake kushika dhamana ya nchi hii kwa kura za kishindo. Namwombea Mwenyezi Mungu amtangulie aweze kusimamia na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi kwa uadilifu mkubwa. Vile vile, nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa ushindi mkubwa alioupata na kuwa Mbunge wa Jimbo la Monduli na kuteuliwa kwake na Mheshimiwa Rais kushika wadhifa huo uliopata baraka za Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe mwenyewe pia kwa ushindi mkubwa ulioupata na kukuwezesha kuwa Mbunge wa Jimbo la Urambo Mashariki na pia kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kura nyingi. Nimalizie pongezi hizi kwa dada yangu mpendwa Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, kwa imani kubwa waliyonayo kwake wananchi wa Njombe Kusini waliomchagua kuwa Mbunge wao, imani ambayo imetiririka hadi hapa Bungeni na kumfanya achaguliwe kwa kishindo kuwa Naibu Spika wa Bunge letu. Ikiwa ni ushindi ambao umetujengea heshima kubwa wanawake wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru wanawake wa Mkoa wa Singida kwa kunichagua tena kuwa Mbunge wao kwa awamu ya pili. Kupitia Bunge lako Tukufu, napenda kuwaahidi kwamba nitaendelea kuwa mwaminifu kwao kwa kutetea haki na maslahi yao kwa lengo la kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia, napenda nimpongeze dada yangu Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, kuwa Waziri wa Kwanza wa Fedha Mwanamke nchini Tanzania. Ninamwombea Mwenyezi Mungu aendelee kuimudu nafasi hiyo kwa kauli mbiu ya Mheshimiwa Rais yaani ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Nimpongeze pia Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na Manaibu Waziri, Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Abdisalaam Isaa Khatib na Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Manaibu Waziri wa Fedha, Makatibu Wakuu wa Wizara zote mbili na watendaji wote walioshiriki katika kuandaa bajeti hizi zenye mwelekeo wa kuwaletea maendeleo Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengi mazuri yaliyoainishwa katika bajeti hii, napenda kushauri maeneo kadhaa kwa niaba ya wanawake wa mkoa wa Singida kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu mishahara. Naipongeza sana Serikali kwa kupandisha bajeti ya mishahara ya watumishi wetu Serikalini, jambo ambalo linaonekana kupokelewa vema na Watanzania na kuwaongezea ari ya kfuanya kazi. Hata hivyo, naishauri Serikali kuwa nyongeza hiyo waboreshewe zaidi watumishi wa chini na wa kati maana ndiyo wenye mishahara midogo zaidi ambayo haiendi sambamba na gharama za maisha ya sasa.

Pili ni kuhusu bei ya umeme. Umeme ni nishati muhimu katika kuchochea maendeleo ya nchi maana unahitajika na watu wa chini kwa shughuli za majumbani mwao na watu wa juu kwa shughuli za viwandani na sehemu mbalimbali za uzalishaji. Hivyo basi, umeme unapobakia kuwa wa bei ya juu zaidi, huchangia uzalishaji kwa mtu wa chini kuwa mdogo zaidi na kumfanya Mtanzania mwenye kipato kidogo ashindwe kabisa kumudu malipo yake. Hivyo basi, naishauri Serikali kutafuta chanzo mbadala cha kufidia gharama za uzalishaji wa umeme ili mlalahoi wa Tanzania aweze kukabiliana na ongezeko hili la bei ya umeme. Kwa mfano, vitu kama pombe na sigara vingepandishwa bei zaidi ya inavyotamkwa sasa.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu mafuta ya taa. Naipongeza Serikali yetu kwa kushusha bei ya nishati hii maana itasaidia sana katika kuhifadhi mazingira yetu hasa kwa kupunguza ukataji ovyo wa miti vijijini kwa lengo la kupata mkaa. Hata hivyo, naishauri Serikali kupitia idara zinazohusika iimarishe ukaguzi wa ubora wa nishati hii kuliko ilivyo sasa ili kuwadhibiti wafanyabiashara wasio waaminifu wanaochanganya mafuta ya taa na vimiminika vingine kama vile maji, petroli na kadhalika. Nazungumzia hilo kwa sababu tayari kuna Watanzania ambao wamekwishaathiriwa na mafuta hayo kwa kutowaka ama kulipuka ovyo mkoani Singida.

Mheshimiwa Spika, nne ni kuhusu ruzuku za fidia pamoja na mifuko mbalimbali ya maendeleo. Naomba niipongeze Serikali yetu kwa kuandaa utaratibu wa kutoa ruzuku ya fidia ya kodi zilizofutwa baada ya kuonekana kuwa kero katika halmashauri zetu. Hata hivyo naishauri Serikali kuwa ni vema kiasi cha fidia hiyo kiwiane na fedha ambazo halmashauri zilikuwa zinapata kutokana na vyanzo vya kodi vilivyofutwa kwani imedhihirika kuwa baadhi ya halmashauri zinafidiwa kidogo zaidi kuliko walivyokuwa wanapata kabla ya vyanzo hivyo kufutwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mifuko mbalimbali ya maendeleo, mifuko hii inasaidia sana kuharakisha maendeleo katika halmashauri zetu maana inatumika katika

kuendesha miradi mbalimbali ya maendeleo ingawa ningependa kushauri kuwa upelekaji wa fedha za mifuko hii ulingane na kauli mbiu ya Mheshimiwa Rais kwa maeneo inayohitajika. Fedha hizo zinapopelekwa katika halmashauri kwa kucheleweshwa zaidi, zinawafanya watendaji kuzitumia kwa shughuli ambazo hazikustahili ama kuziacha tu bila kutumika hivyo kusababisha halmashauri kupata vikwazo katika kupata kasma nyingine.

Mheshimiwa Spika, suala la tano ni kuhusu mifuko ya rambo. Mifuko hii ni hatari kwa wanyama wetu wanapoimeza kwa bahati mbaya na hatari kwa uchafuzi wa mazingira. Naipongeza Serikali yetu kwa kupandisha bei yake kama hatua muhimu katika kupunguza ununuzi na usambaaji wake.

Ningeishauri Serikali kutafuta mbinu zaidi ili mifuko hii hatari isitumike kabisa, badala yake mifuko inayotengenezwa kwa njia za asili kama vile ukindu, katani na kadhalika ingehamasishwa zaidi. Kwa kufanya hivyo, nafikiri akina mama wa Kitanzania kwa namna moja ama nyingine wataweza kujipatia ajira katika kutengeneza mifuko hiyo.

Mheshimiwa Spika, suala la sita ni kuhusu michezo. Naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne kwa jinsi ilivyoanza kwa kasi kubwa katika nyanja mbalimbali za maendeleo ya Watanzania ikiwemo michezo. Mataifa mbalimbali sasa yameanza kuelewa kuwa michezo siyo afya na burudani tu, bali pia ni ajira. Hata hivyo nimesikitishwa na kitendo cha Televisheni yetu ya Taifa kutoonyesha michuano mbalimbali ya dunia inayoonyeshwa sasa moja kwa moja kutoka nchini Ujerumani. Nilifikiri pengine stesheni hiyo ingetumia muda wake fulani kuonyesha michezo hiyo na kuwafanya Watanzania waone na kujifunza wenzao wanafanya nini katika mashindano yanayoendelea.

Mheshimiwa Spika, suala la saba ni udhibiti wa uagizaji holela wa magari. Hili pia ni eneo lingine ambalo napenda kuipatia Serikali yetu pongezi za dhati maana wimbi la uagizaji na uingizaji wa magari yaliyokwishatumika toka nchi za nje ulianza kukua kwa kasi mno madhara ya moja kwa moja yakiwa ni ongezeko la ghafla la uchafuzi wa mazingira, misululu mirefu ya magari barabarani pamoja na baadhi ya ajali barabarani. Nashauri Serikali yetu isimamie kwa dhati lengo hilo zuri ililojiwekea ili nchi yetu isijegeuzwa dampo la vyuma chakavu.

Mheshimiwa Spika, suala la nane ni kuhusu fedha za UKIMWI kutoka Taasisi zisizo za Kiserikali. Ni dhahiri kuwa vita dhidi ya gonjwa hili la UKIMWI ni yetu sote maana gonjwa lenyewe halibagui. Naunga mkono Sera ya Taifa kuhusu vita dhidi ya UKIMWI japokuwa ningependa kushauri jambo moja hasa kuhusu matumizi halisi ya pesa zinazoombwa kwa wafadhili na Taasisi mbalimbali zisizo za Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu, imedhihirika kuwa fedha hizo hutumika kwa kiasi kikubwa kuwanufaisha waendeshaji wa semina hizo kwa njia ya posho kuliko kuwanufaisha waathirika halisi ama watu ambao wako katika mazingira ya kuweza kuathirika. Itakuwa ni busara zaidi endapo sehemu kubwa ya fedha hizo kutoka Taasisi zilizojitangaza kuwa zipo kwa ajili ya kupambana na ugonjwa wa

UKIMWI ikatumika katika kununua dawa za kupunguza makali ya virusi, kuwanunulia wagonjwa vyakula, vyandarua na mahitaji mengine yanayofaa kuliko kukidhi tu haja za kiuchumi za wenye Taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, suala la tisa ni kasi ya kupima viwanja kwenye miji midogo na vijijini. Ardhi ndiyo raslimali pekee na ya karibu mno kwa Mtanzania wa kawaida kuitumia katika kujikwamua kiuchumi. Mtanzania wa chini na wa juu zaidi kimaisha anaweza kuitumia ardhi kama dhamana ya kuombea mkopo toka Taasisi mbalimbali zenye kutoa mikopo endapo kuna hati halali za Mtanzania huyo kumiliki ardhi hiyo. Cha kushangaza zaidi ni kwamba, kasi ya Serikali zetu kupima viwanja kwenye miji yetu midogo na kwenye vijiji imekuwa ndogo sana na mahali pengine haipo kabisa.

Ningependa kuishauri Serikali yetu izingatie umuhimu wa ardhi hiyo kwa Watanzania katika kujikwamua kiuchumi hasa pale ardhi hiyo inapokuwa imepimwa na kutolewa vibali vya umiliki na mamlaka halali inayohusika kisheria. Sambamba na hili, napenda vile vile kuishauri Serikali kuwawezesha wananchi wetu kujenga na kuishi katika nyumba zenye viwango vya kuridhisha kwa kuwapunguzia bei za vifaa vya ujenzi ili wananchi waweze kujijengea nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, ni wakati muafaka sasa kwa wananchi kufanya hivyo na wameonyesha dhamira hiyo Serikali nayo ingewasaidia kwa kuwapunguzia bei za vifaa kama vile bati, saruji, vigae na kadhalika.

**MHE. AME PANDU AME:** Mheshimiwa Spika, kwanza naanza kwa kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kupata kura nyingi sana za Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuteuliwa na kuthibitishwa na Bunge kushika wadhifa huo. Pia niwapongeze Mawaziri wote pamoja na Manaibu Waziri wote kwa kuteuliwa kushika nyadhifa hizo.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe pia na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi zangu hizo, nami nichangie kwenye bajeti ya nchi yetu ya mwaka huu 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, bajeti ni nzuri na ni ya kutupa matumaini sana. Kuhusu maendeleo, maendeleo ya nchi yetu Watanzania hayako mbali, bali tatizo ni utekelezaji wa yale tunayoyapanga kuyafanya, kutokuwa waaminifu kwa baadhi ya watendaji wa Serikali na pia kutokuwa wafuatiliaji kwa maagizo yanayotolewa kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, tukishakuwa na tabia ya kuwa na maneno machache na vitendo vingi, muda si mrefu Watanzania tutakuwa ni wenye kupiga hatua kubwa ya maendeleo kwani sisi Watanzania ni hodari sana wa kusema lakini vitendo vyetu ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umaskini, Tanzania ni tajiri ila Watanzania ndio maskini. Umaskini huo walionao Watanzanaia utawaondokea kabisa iwapo Serikali ya Tanzania itawafanyia Watanzania hawa haya yafuatayo, kuwafikishia barabara, maji, umeme, shule zenye walimu, kuwasogezea mabenki mikoani/wilayani mwao, pia Serikali izitumie malighafi zilizomo humu nchini kwa faida ya Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ili iondokane na umaskini, itumie ardhi yake kwa kilimo cha umwagiliaji, mito, maziwa, mvua yote tunayo basi tuitumie. Pia madini, bahari za Tanzania itumike kwa kuwaletea maendeleo na kuwaondolea umaskini Watanzania na siyo wageni.

Mheshimiwa Spika, Watanzania tusijione hatuna teknolojia lakini tunayo mali, usemi huu ndio ukawa ni sababu ya kugawa mali zetu kwa wageni, kwa thamani ndogo tu. Kitendo hicho ni kibaya kabisa, Watanzania tunayo teknolojia lakini ni ndogo, tuitumie teknolojia hiyo ndogo ili ikue, tuitumie kwa mambo yetu.

Mheshimiwa Spika, kupandishwa kwa ushuru wa simu za mkononi na ushuru wa barabara kutazidisha umaskini.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huo na mimi naunga mkono bajeti kwa asilimia moja.

**MHE. MWAKA ABRAHMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nimpongeze Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, kwa hotuba yake nzuri na pia niwapongeze Manaibu Waziri wa Fedha na watendaji kwa kuitayarisha hotuba hiyo.

Mheshimiwa Spika, nianze kutoa mchango wangu kama ifuatavyo, kwanza, napenda kuipongeza Serikali kwa mapendekezo yake ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2006/2007.

Kwa kweli bajeti hii ni nzuri kwani imelenga kuwasaidia wananchi wa hali ya chini na pia kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upandaji wa ushuru wa simu za mkononi *(mobile phones airtime)*, kwa kweli simu ni matumizi muhimu kwa binadamu na hasa tukizingatia kwamba zinamsaidia tajiri na maskini. Hivi sasa kuna baadhi ya vijiji haujafika mtandao wa simu na watu wanaoishi katika vijiji hivyo wanahitaji mawasiliano na kama inavyoeleweka kwamba maisha ya vijijini ni magumu, leo hii ushuru wa simu unataka kupandishwa, je, ni kweli tunataka kumsaidia mwananchi wa chini au tunamdidimiza?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Zanzibar, mpaka hivi sasa bado jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais halijajengwa, hatuelewi ni nini kinachokwamisha, kwa hiyo, tunaomba Serikali kuliangalia suala hilo ili jengo hilo liweze kujengwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hotuba zote mbili mia kwa mia.

**MHE. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kutuwezesha kuliwahi Bunge letu jipya, Bunge la kisasa, Bunge lenye hadhi ya Kimataifa. Aidha, nakushukuru wewe kwa ushupavu wako wa kusimamia vyema Bunge letu kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Mheshimiwa Spika, nazipongeza hotuba zote mbili. Kuhusu hali ya uchumi, pamoja na kwamba uchumi wetu unakua lakini bado kuna haja ya kuangalia vyema kilimo kwani asili ya Mwafrika ni nguvu zake ni kilimo, lakini tuimairishe kilimo cha kisasa tena kiwe cha umwagiliaji na pia kuitumia milima yetu kwa kilimo maalum.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda, viwanda vingi tulikuwanavyo, lakini karibu viwanda vingi vimelala au kufa kabisa. Kwa hiyo, tuna wajibu wa kuangalia vyema kuimarisha tena viwanda vyetu ili kuimarisha uchumi wetu na kuwapatia ajira vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utalii, utalii unachangia sehemu kubwa ya pato letu la Taifa. Sehemu kubwa ya mbuga zetu za utalii zinahitaji utunzaji mzuri, kwani ziko baadhi zinakatwa miti na nyingine kuunguzwa moto na kusababisha hasara kubwa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, aidha, maeneo ya historia kama Ujiji kule Kigoma, eneo la Sokwe Mtu na mengineyo yanapasa kuimarishwa vyema.

Mheshimiwa Spika, elimu ni ufunguo wa maisha ya mwanadamu. Aidha, ni sehemu moja kuu ya kuondoa ujinga na umaskini. Kwa maana hiyo, ni haki kabisa katika kuimarisha elimu katika nchi yetu. Naunga mkono katika kujenga zaidi Vyuo Vikuu na nashauri hali yetu ya uchumi itakaporuhusu ni vyema ile mikoa inayoongoza kwa idadi ya watu vijengwe Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa kuanza kushughulikia kero za Muungano kwani kuondoshwa kwa kero hizo ndio kuimarisha Muungano wetu, pamoja na kushughulikia suala la mgao ambao kwa sasa ni asilimia 4.5, lakini Serikali ya Awamu ya Nne mwaka huu imetoa shilingi bilioni 21. Kwa Serikali ya Zanzibar, jambo hilo mimi binafsi na wananchi wa Zanzibar tunalipongeza na kulifurahia.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena ninaipongeza Serikali kwa ujumla pamoja na wewe na Bunge lako lote kwa kazi nzuri ya kulitumikia Taifa kwa ujumla. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Bumbwini, tunaunga mkono hoja zote mbili yaani Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Wizara ya Fedha kwa asilimia mia moja.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Waziri wa Fedha kwa kutoa madokezo ambayo yanahitaji kurekebishwa katika mfumo wa kodi kwa Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni masuala muhimu yanayotakiwa kufanyiwa marekebisho katika mfumo wa kodi kwa Sekta ya Madini bila ya kutakiwa kujadiliana na Makampuni ya Madini yenye mikataba na Serikali. Uchambuzi wa kina uliofanyika umebaini kwamba maeneo haya yanatakiwa kufanyiwa marekebisho ya haraka ili kuleta uwiano wa mapato baina ya wawekezaji katika Sekta ya Madini na Serikali. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo: -

(i) Kodi kwenye bidhaa za mafuta ya petroli, hali ilivyo sasa ni kwamba Makampuni ya Madini yanalipa kodi moja tu kwenye bidhaa za mafuta inayoitwa *fuel levy* (zamani ikiitwa *road toll*) kwa kiwango kisichozidi Dola za Kimarekani 200,000.00 kwa mwaka. Kiwango hiki ni kidogo sana ikizingatiwa kwamba matumizi ya mafuta kwa Makampuni ya Madini ni makubwa na kwa kutumia kiwango hiki Serikali inapoteza kodi kubwa sana. Kwa mfano, katika kipindi cha kati ya mwaka 2002 hadi 2005, wastani wa matumizi ya mafuta kwa kampuni moja ya *Geita Gold Mine (GGM)* ni lita milioni 58.0 kwa mwaka. Kwa kutumia kiwango cha sasa cha kulipa *fuel levy* cha shilingi 90 kwa lita, wastani wa kodi inayotakiwa kulipwa na *GGN* ni shilingi bilioni 5.22 kwa mwaka. Hata hivyo, kampuni ya *GGM* inalipa wastani wa shilingi milioni 250.0 kwa mwaka (ukitumia *exchange rate* ya shilingi 1,250/Dola ya Kimarekani kama *fuel levy* (hii ni sawa na kodi ya matumizi ya wiki tatu tu) kutokana na mkataba kati ya kampuni hiyo na Serikali. Kwa hali hii, Serikali inapoteza wastani wa Shilingi bilioni 4.97 kwa mwaka kwa kampuni moja tu ya *GGM* kwa kutolipa kodi inayostahili ya *fuel levy*.

Pamoja na hayo, Makampuni ya Madini yamesamehewa kulipa kodi ya ushuru wa bidhaa kwenye mafuta *(excuse duty on petroleum products).* Hatua hii inaifanya Serikali ipoteza mapato makubwa sana. Msamaha huu kwenye Makampuni ya Madini hauna msingi wowote ikizingatiwa kuwa gharama za kodi kwenye bidhaa za mafuta ya petroli zinazolipwa na makampuni hayo ni miongoni mwa gharama zinazoruhusiwa kupunguzwa kwenye mauzo wakati wa kukokotoa kodi ya makampuni *(allowable expenses for deductions)* chini ya Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004.

Inapendekezwa kuwa Makampuni ya Madini yalipe kodi yote ya *fuel levy* bila ya kuwa na ukomo katika ulipaji kodi hii. Aidha, inapendekezwa Makampuni ya Madini yalipe kodi ya ushuru wa bidhaa kwenye mafuta kama ilivyo kwenye Sheria ya *Excise Management and Tarriff Act* kwa sababu kodi hizi siyo mzigo kwa Makampuni ya Madini maana zinaruhusiwa kupunguzwa kama matumizi ya kawaida wakati wa kukokotoa kodi ya makampuni (Hakuna nchi yoyote duniani yenye madini inayotoa msamaha wa kodi kwenye mafuta isipokuwa Tanzania).

(ii) Msamaha Maalum kwenye Kodi ya Ongezeko la Thamani *(Special Relief on VAT),* msamaha maalum kwenye Kodi ya Ongezeko la Thamani unaotolewa kwa Makampuni ya Madini hauna msingi wowote kwa sababu bidhaa zote zinazozalishwa na makampuni hayo huuzwa nje ya nchi ambapo hutozwa kodi kwa kiwango cha sifuri *(zero rated).* Makampuni hayo yanarejeshewa malipo ya *VAT (input VAT)* kwa mujibu wa sheria. Utaratibu uliopo unatosheleza na una kipengele kinachoibana *TRA* kulipa riba *(interest)* ikiwa mlipakodi atacheleweshewa marejesho yake ya kodi bila sababu za msingi katika kipindi kisichozidi siku 30 (kifungu 28(5) cha *VAT Act,* 1997 kinahusika).

Kuwepo kwa msamaha maalum *(special relief)* kunatoa mwanya mkubwa wa udanganyifu wa matumizi mabaya ya fursa hiyo kwa kuhusisha bidhaa au huduma zisizohusiana na masuala ya mgodi kama kwa mfano kodi kwenye gharama za malazi na chakula kwenye mahoteli, uagizaji au ununuzi wa bidhaa nyingi zisizolipiwa kodi kuliko mahitaji halisi ya migodi hiyo, kutoa mwanya wa *sub-contractors* kushirikiana na Makampuni ya Madini kufanya *transactions* kwa nia ya kukwepa kodi na kadhalika. Inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye jedwali la tatu kifungu cha saba cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 1997 kwa kufuta kifungu cha sasa na kuingizwa maeneo yafuatayo, *Importation or domestic supplies of goods and services by Prospecting licence holders that will be used solely for prospecting activities.*

(iii) Msamaha kwenye Ushuru wa Forodha, wakati Makampuni ya Madini yalipokuwa yanaingia mikataba na Serikali mwishoni mwa miaka ya tisini, Tanzania ilikuwa na mfumo wa ushuru wa forodha uliokuwa na viwango vingi pamoja na kutoza kodi kwenye mitambo na malighafi. Hii ililazimisha Makampuni ya Madini kuomba kusamehewa kodi kwa kupewa kiwango cha ushuru wa forodha kisichozidi asilimia tano (5%) chini ya ushuru wa forodha ya mwaka 1976. Hali hii ilirekebishwa kuanzia mwaka 2001 wakati Serikali ilipofanya mageuzi makubwa ya mfumo wa ushuru wa forodha kwa kupunguza viwango toka 12 hadi 4 tu. Aidha, Serikali iliondoa ushuru wa forodha katika mitambo ya mashine pamoja na malighafi. Hatua hii iliyafanya Makampuni ya Madini kufaidika na kutolipa kodi hiyo pia katika vifaa husika, ingawa mikataba ya makampuni hayo inasema walitakiwa kulipia asilimia tano (5%).

Mheshimiwa Spika, kuanzia Januari, 2005, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki zilianza kutumia Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ya mwaka 2004. Chini ya Sheria hiyo, kodi ya ushuru wa forodha ka mitambo ya malighafi *(capital goods and raw-materials)* hazitozwi ushuru wa forodha. Kwa kuwa vifaa vyote vinavyohusiana na migodi ya madini havitozwi tena ushuru wa forodha chini ya sheria ya ushuru wa forodha ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na kwa kuwa sheria hii inazifunga nchi wanachama kutotumia sheria zilizokuwa zinatumiwa na nchi wanachama kabla ya sheria hii, Tanzania kama mwanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki inalazimika kutumia Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa kutoza ushuru kwa viwango vilivyo ndani ya sheria hii. Kwa kuwa kiwango cha asilimia tano hakipo ndani ya sheria ya ushuru wa forodha ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, inapendekezwa kwamba Makampuni ya Madini yalipe ushuru wa forodha kwa kutumia viwango chini ya sheria ya ushuru wa forodha ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ambavyo ni 0%, 10% na 25%.

(iv) Kodi za Zuio *(Withholding Taxes).*

(a) Kodi ya Zuio kwa Huduma za Kitaalam *(Withholding Tax on Technical Services)*,makampuni ya Madini yanalipa kodi ya zuio ya asilimia 3 kwa makampuni ya kigeni na makampuni yaliyosajiliwa hapa nchini yanayotoa huduma za kitaalamu kwa makampuni hayo. Sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2004 imeweka viwango vya asilimia tano kwa makampuni yaliyosajiliwa hapa nchini na asilimia kumi na tano (15%) kwa makampuni ya kigeni.

(b) Kodi ya Zuio katika Ada ya Menejimenti *(Withholding Tax on Management Fees*, kutokana na mikataba, makampuni ya Madini yanalipa kodi ya zuio katika ada ya menejimenti ya asilimia tatu iwapo kiwango cha ada ya menejimenti hakizidi asilimia mbili ya gharama za uendeshaji wa mgodi. Ikiwa kiwango cha ada ya menejimenti kikizidi asilimia mbili ya gharama za uendeshaji wa mgodi, kodi ya zuio katika ada ya menejimenti ni asilimia ishirini. Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 imeweka viwango vya asilimia sifuri kwa makampuni yaliyosajiliwa hapa nchini na asilimia kumi na tano kwa makampuni ya kigeni.

(c) Kodi ya Zuio kwenye Riba ya Mikopo *(Withholding Tax on Loan Interest),* katika mikataba ya madini, Makampuni ya Madini yanalipa kodi ya zuio kwa malipo ya riba ya mikopo inayokopwa kutoka nje ya nchi. Mfumo huu unatoa mwanya kwa makampuni yenye uhusiano kukopeshana bila uwazi. Aidha, mfumo huu unatumiwa na Makampuni ya Madini kuanzisha Vyombo vya Fedha nje ya nchi kwa ajili ya kukopesha makampuni mama yaliyo kwenye uzalishaji kwa riba kubwa na hivyo kutoa mwanya wa utoroshaji wa faida ya makampuni hayo kwa njia ya riba isiyotozwa kodi. Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 imeweka kiwango cha asilimia kumi kama kodi ya zuio kwenye riba ya mikopo yote inayokopwa nje na ndani. Kiwango hiki ni cha ushindani Kimataifa maana nchi nyingi duniani zinatoza kiwango zaidi ya hicho. Aidha, kodi haitozwi kwenye mapato ya Kampuni ya Madini. Inapendekezwa kuwa kodi za zuio zilizoorodheshwa hapo juu zilipwe kwa kutumia Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa kama nilivyosema awali tunakaribisha wachangiaji kutoka Serikalini. Tutaanza na Naibu Waziri, Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia ambaye atafutiwa na Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustapha Mkulo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo utaratibu unahitaji mimi nitatoa baadhi ya maelezo na Mheshimiwa Waziri atakuja kutoa maelezo mengine na kukamilisha hoja hii iliyo mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ni maelezo na ufafanuzi wa hoja za Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba ya Waziri wa Mipango, Uchumi, Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Mbunge, wakati alipowasilisha Bungeni muhtasari wa Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2005/2006 na Mapendekezo ya Mpango wa Muda wa Kati na Mfumo wa Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2006/2007 hadi 2008/2009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naanza. Kulikuwa na hoja kwamba iundwe Kamati inayoshirikisha sekta mbalimbali ili uwanja wa Songwe uweze kuwa na manufaa ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wachangiaji walikuwa ni Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi na Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda. Ushauri huu ni mzuri na utafanyiwa kazi na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimwia Spika, hoja inayofuata Serikali ianzishe kiwanda cha mbolea. Hoja hii pia imetolewa na Mheshimiwa Richard Nyaulawa na Mheshimiwa Godfery Zambi, Serikali inashughulikia suala hili na inaendelea kufanya mazungumzo na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, hoja inayofuata Serikali iongeze bajeti ya sekta ya maji. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Fred Tungu, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Raynald Mrope na Mheshimiwa Juma Njwayo. Serikali itaendelea kuongeza fedha za bajeti hususan kwenye shughuli za huduma za jamii ikiwemo sekta ya maji kadri uwezo wa kibajeti utakavyoruhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni msisitizo wa mazingira umewekwa tu kwenye upandaji miti, vipi kuhusu taka za sumu. Hoja hii imetolewa na Mheshimwia Fred Tungu na Mheshimiwa Raynald Mrope. Si kweli kwamba hifadhi ya mazingira inafanyika kwa kupanda miti tu, sera ya Taifa ya Hifadhi ya Mazingira inajumuisha masuala mbalimbali yakiwemo uharibifu wa ardhi, kutokupatikana kwa maji safi na salama, uchafuzi wa mazingira, upotevu wa makazi ya viumbe na baionuwani, uharibifu wa makazi ya viumbe vya majini na uharibifu wa misitu. Suala la udhibiti wa taka za sumu linajitokeza katika baadhi ya masuala hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kudhibiti taka za sumu, Serikali imeridhia mikataba mbalimbali ya Kimataifa chini ya Mkataba wa Stockholm unaohusu Udhibiti wa Kemikali Hatari zinazochukua muda mrefu kuoza. Mwaka 2005 tani 1,200 za kemikali chakavu za kilimo zilitambuliwa na mkakati wa kudhibiti madhara ya kemikali hizo uliandaliwa. Aidha, chini ya Mkataba wa BAZILI wa mwaka 1989 unaohusu utupaji wa taka za sumu na usafirishaji wake baina ya nchi na nchi mwaka 2005. Mafunzo yalitolewa kwa wataalam zaidi ya 100 juu ya mbinu za uzalishaji bora kwa viwanda 47 vya Mkoa wa Dar es Salaam, Mwanza, Tanga, Arusha, na Manispaa za Morogoro, Moshi, Unguja na Pemba.

Hoja inayofuata ni ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma uende sambamba na uboreshaji wa barabara, umeme, maji na miundombinu mingine. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Mariam Mfaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma ambao utaanza kwa kutumia Jengo la Chimwaga pamoja na miundombinu mingine iliyopo utakamilika utakapokuwa na huduma zote muhimu za Chuo Kikuu cha kisasa ikijumuisha barabara, maji, umeme, huduma za afya na mahitaji mengine. Hivi sasa kamati ya wataalamu inaendelea kufanya kazi ya kubainisha mahitaji yote ya uanzishwaji wa Chuo hicho ili awamu ya kwanza ya wanafunzi waweze kudahiliwa ifikapo mwezi Septemba, 2007 mwakani wakati shughuli za ujenzi zikiendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja inayofuata manufaa ya kukua kwa uchumi hayajawafikia wananchi. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Ephraim Madeje na Mheshimiwa Aggrey Mwanri.

Mheshimiwa Spika, si kweli kuwa manufaa ya kukua kwa uchumi hayajawafikia wananchi, yawezekana manufaa hayo hayajabainishwa vya kutosha kwa wananchi wote. Ili kufafanua dhana ya manufaa ya ukuaji uchumi ninaomba nieleze kwa ufupi tu kuwa viashirio vya ukuaji uchumi ni pamoja na moja, kuongezeka kwa viwango vya uzalishaji wa bidhda na utoaji wa huduma katika nchi. Bidhaa zinapoongezeka na viwango vya utoaji huduma kupanda ni dhahiri wananchi wananufaika na ongezeko la upatikanaji wa bidhaa hizo ikiwa ni pamoja na chakula, bidhaa za viwandani na huduma.

Pili, kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji na ongezeko la viwango vya utoaji huduma, mapato ya Serikali kwa njia ya kodi na makusanyo mengine yanayotozwa kwenye bidhaa na huduma nayo yanaongezeka. Kutokana na kupanuka kwa wigo wa kodi, mapato ya Serikali yanapoongezeka uwezo wake wa kutoa na kuboresha huduma muhimu kwa wananchi nao unaongezeka. Kwa njia hiyo, wananchi nao wananufaika na tatu, uchumi unaokua unapanua fursa za ajira kwa wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo mafupi ni dhahiri kuwa wananchi wananufaika kwa kukua kwa uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja inayofuata, kwa kuwa Serikali inapitia upya mikataba ya madini, upitiaji huo uendane pia na mapitio ya sera za sheria ya uwekezaji. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Elisa Mollel na tunasema ni ushauri mzuri na Mheshimiwa Rais ameshaunda kamati maalum ya Mawaziri kwa ajili ya kushughulikia suala hilo na mapendekezo yake yatasaidia kuboresha sera, mifumo na sheria.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine, Mradi wa *TASAF* unajenga barabara bila madaraja kama vile barabara ya Vumilia-Ukooni. Hoja hii, imetolewa na Mheshimiwa Mwinchoum Msomi. *(Makofi)*

*TASAF* inafadhili miradi inayoibuliwa na kutekelezwa na wanajamii wenyewe na kwamba kukamilika kwa mradi wowote kunategemea pia mchango wa jamii husika. Barabara ya Vumilia-Ukooni iliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge iligharamiwa na *TASAF* kwa kiasi cha shilingi 45,740,550/= kama wanajamii walivyoomba. Kutokana na gharama za vifaa kupanda bei fedha hizo hazikutosha kumaliza madaraja. Manispaa ilikubali kumalizia madaraja lakini haikutoa fedha. Ili kukamilisha mradi huu jamii husika inashauriwa kuomba fedha za kumalizia kutoka Awamu ya Pili ya *TASAF* au kukumbushia Manispaa husika yaani Temeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine uwanja wa kisasa wa michezo ujengwe Dodoma. Hoja hii imetolewa na Meshimiwa Mwinchoum Msomi.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa uwanja wa kisasa unajengwa Jijini Dar es Salaam. Serikali itaangalia uwezekano wa kujenga viwanja vingine vya kisasa katika Mikoa mingine kadri hali itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa umeme na uendeshaji wa reli vibaki kuwa kazi ya Serikali. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Aggrey Mwanri. Katika ubinafsishaji wa mashirika ya huduma na miundombinu, Serikali itaendelea kumiliki miundombinu na mashirika ya umma hivyo kuwa na jukumu la kuwekeza na uendeshaji wa mashirika husika. Sekta binafsi itakodishiwa uendeshaji wa biashara tu za mashirika hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja inayofuata ni miradi iliyomo kwenye Ilani ya Uchaguzi kuna mingine ambayo haipo kwenye mpango wa maendeleo. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Herbert Mntangi, hii ni kwa kuwa mpango wa maendeleo ni wa mwaka mmoja na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ni wa kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, hoja inayofuata ubinafsishaji unazingatia zaidi rasilimali fedha na majengo lakini siyo rasilimali watu. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa John Lwanji na tunasema kwamba Serikali imekuwa ikizingatia mafao ya wafanyakazi pale inapokuwa na uwezo. Masuala ya wafanyakazi yamezingatiwa kikamilifu na Serikali hasa katika kuwaruhusu wafanyakazi kumilikishwa baadhi ya Mashirika, kuwalipa mafao na pensheni iwapo wataachishwa kazi au kustaafu na Serikali kulipa madeni ya Mashirika husika.

Mheshimiwa Spika, nini uhusiano wa vitambulisho vya Taifa na maendeleo. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa John Lwanji.

Mheshimiwa Spika, kuwa na kitambulisho kutasaidia katika utambuzi, kupata mikopo, kupata huduma, kupata hati, kusimamia masuala ya usalama wa raia, kuandikisha mali na mengineyo mengi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba sekta isiyo rasmi inachangia katika ajira haijatengewa fedha. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Charles Kajege.

Mheshimiwa Spika, sekta isiyo rasmi inashughulikiwa na miradi na programu mbalimbali ambazo zimekuwa zinatengewa fedha. Baadhi ya programu hizo ni MKURABITA, *TASAF* na *SELF* ni miongoni mwa jitihada nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha nyingi zimetolewa kwenda MKUKUTA *monetary* kiasi cha shilingi bilioni 11, badala ya kuzipeleka *SELF* ambayo imepata bilioni 3.4 na *TASAF* ambayo imepata bilioni 3.5.

Mheshimiwa Spika, kwa nini shilingi bilioni 11 za MKUKUTA zisipelekwe katika kuondoa umaskini? Hoja hii imeletwa na Mheshimiwa Charles Kajege, tunasema kwamba fedha za *TASAF* zinazopitia Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ni zile zinazotoka *OPEC Fund*. Shilingi bilioni 3.5 ambazo ni mahsusi kwa ajili ya Mikoa ya Lindi na Mtwara tu. Fungu kubwa ya fedha za *TASAF* linapitia Ofisi ya Rais, ambako fedha nyingi zaidi zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Jamii. Fedha za *SELF* zinatoka *ADB* yaani *African Development Bank*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu shilingi bilioni 11 ufuatiliaji ni kwamba hizi ni kwa ajili ya kufanya *survey* na chambuzi mbalimbali kama ifuatavyo:-

Moja, kuna *survey* ya hali ya kipato na ajira katika ngazi ya kaya. *Survey* kama hii ilifanyika mwaka 1991 na 2001. Gharama za *survey* hii ni kubwa ndiyo maana hufanyika kila baada ya miaka 5. *Survey* hii ni muhimu sana kupima hali ya umaskini katika kaya.

Pili, *survey* ya hali ya ajira nchini ambayo ilishaanza, tatu, uchambuzi wa takwimu za utafiti wa afya na idadi ya watu na *survey* ya kilimo iliyofanyika mwaka 2004, nne, tafiti za hali ya umaskini zifanyazwo na *REPOA*, tano, kuboresha ukusanyaji wa takwimu za kiutawala na sita, uelimishwaji na uhamasishaji wa wananchi kuhusu sera ya mikakati na kupunguza umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja inayofuata ni bila ongezeko katika tija nchi haitapiga hatua katika maendeleo. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Lazaro Nyalandu na Balozi Getrude Mongella.

Mheshimiwa Spika, tunakubaliana na Waheshimiwa Wabunge hao na Serikali inaweka mkazo katika kuendesha Elimu ya Juu, ufundi, ujasiriamali na stadi nyinginezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nini kinafanyika katika bandari ya Tanga? Hoja hii imesemwa na Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, ipo mikakati inayoandaliwa kuipanua Bandari ya Tanga. Wizara husika itafanunua zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiundwe chombo ambacho kitakuwa ni *think tank* ya uchumi wa nchi. Hoja hii imesemwa na Mheshimiwa Lazaro Nyalandu. Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji imepewa jukumu hilo na inaratibu mawazo mbalimbali ya kiuchumi na ya kijamii kutoka kwa wadau na Wizara itafanya midahalo mbalimbali ambayo itashirikisha wataalamu na wanataaluma ili kupata ushauri wa kuendeleza nchi kiuchumi kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini miradi ya Liganga na Mchuchuma haikuguswa kwenye hotuba ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Hoja hii imesemwa na Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe. Ni kweli hakukutajwa moja kwa moja katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ila katika aya namba 57 ya hotuba hiyo mstari wa mwisho imeelezwa kwa ujumla naomba kunukuu: "Juhudi za kuongeza vyanzo vingine vya kuzalisha umeme badala ya kutegemea maji zitapewa msukumo zaidi." Mwisho wa kunukuu. Hivyo, kutotajwa katika hotuba siyo kwamba tumepuuza suala la miradi ya Liganga na Mchuchuma ili kulipa uzito unaostahili suala hili litatolewa taarifa baadaye.

Mheshimiwa Spika, ijengwe barabara kutoka Madaba hadi Mchuchuma. Hoja hii imeletwa na Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi. Mipango ya Serikali ni kuweka miundombinu kwa ajili ya kuendeleza machimbo ya makaa ya mawe ya Mchuchuma kwa

ajili ya kuzalisha umeme na chuma ya Liganga katika utekelezaji wa miradi ya *Mtwara Development Corridor.*

Mheshimiwa Spika, pawepo na udhibiti katika vyombo vya usafiri majini. Hoja hii imeletwa na Mheshimiwa Raphael Mwalyosi na Mheshimiwa Elizabeth Batenga. Serikali itazingatia ushauri huo na itashirikiana na vyombo husika yaani *SUMATRA* katika kudhibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuanzisha *Agro Agriculture Zones*. Hoja hii imeletwa na Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi. Tayari Serikali ilishaanzisha kanda za mazao ya kilimo cha umwagiliaji. Kwa sasa tuna kanda saba za uzalishaji mazao na saba za kilimo cha umwagiliaji maji.

Mheshimiwa Spika, misaada na mikopo ielekezwe katika sehemu zinazoleta tija hasa kilimo. Hoja hii imeletwa na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa. Ushauri huu ni mzuri. Hata hivyo Serikali imekuwa ikielekeza misaada na mikopo kwenye sekta za uzalishaji hususan kilimo kwa kupitia miradi na programu mbalimbali kama *Agricultural Development Programmse, Participatory Irrigation Development Programmes, Districts Agriculatural Sector Investiment* na *Agricultural Investment Support Programmes.* Kuwepo na makakati wa makusudi wa kuwaendelea vijana ili washiriki kikamilifu na kuongeza tija katika kilimo hususan kilimo cha pamba. Hoja hii ililetwa na Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella na suala la kuongeza tija katika uzalishaji sio tu katika zao la pamba bali linahitaji wananchi kujituma na kutumia kikamilifu raslimali zilizopo katika kujiletea maendeleo yao wenyewe. Serikali itaendelea kulititilia mkazo wa elimu hususan kwa vijana ili waweze kujishughulisha kikamilifu na kujua njia bora rahisi na za kisasa za kuongeza tija katika shughuli za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine kuna mkakati gani miaka minne ijayo ya kuwaendeleza vijana walioingia kidato cha kwanza mwaka 2006. Hoja hii vile vile imetolewa na Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella. Tunasema kutokana na mafaniko ya *MMEM* na *MMES* Serikali inalazimika kuendeleza *Treasury Education* na Serikali inafanya majadiliano na wahisani ili kuweza kupata msaada wa kuboresha Elimu ya Juu hususan Vyuo vya Ufundi na stadi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninaomba niunge hoja mkono na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninazo dakika 5? Naomba niendelee ni-*take advantage* ya dakika 5. *(Makofi)*

**SPIKA**: Unazo

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka wa Udhibiti kwa mfano Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* zipewe meno zaidi. Hoja hii ililetwa na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe na tunasema Serikali itazidi kuboresha Mamlaka za Udhibiti ikiwemo *TBS.*

Mheshimiwa Spika, kuwe na mkakati wa kuendeleza raslimali watu. Hoja hii imeletwa na Mheshimiwa Chacha Wangwe na Serikali tunasema mwaka 2006/2007 Serikali itafanya utafiti kuhusu mahitaji na aina ya taaluma zinazohitajika kulingana na mahitaji ya soko huria. Matokeo ya tafiti hizi yatatumiwa na Taasisi za Elimu ya Juu ili ziweze kutoa fani hizo. Aidha, Serikali imeshaandaa Sera ya Taifa ya Ushauri ili kuendeleza raslimali watu.

Mheshimiwa Spika, mipango inaisaidiaje Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ili kilimo kiwe na tija? Hoja hii imeletwa na Mheshimiwa Chacha Wangwe. Mipango ina jukumu kwa Wizara zote ikiwemo Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na kuandaa mwongozo wa mpango wa Bajeti kila mwaka. Mwisho bajeti imekuwa ile ile ya miaka ya nyuma na imekuwa ni mazoea kuongeza kiasi kidogo tu. Hoja hii imeletwa na Mheshimiwa Dr. Festus Limbu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya mwaka wa fedha 2004/2005 bajeti ya maendeleo ilikuwa asilimia 6 tu ya bajeti yote na uamuzi wa makusudi ulifanywa ili bajeti hiyo isiwe chini ya asilimia 15 pamoja na kuzingatia maeneo yaani *clusters* matatu ya MKUKUTA. Bajeti ya fedha za maendeleo imeongezeka na matokeo ya matumizi haya yanalenga maeneo ya kipaumbele tuliojiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii na naomba nitamke kwamba naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Kilosa, napenda kuchukua nafasi hii kuchangia katika baadhi ya hoja zilizojitokeza wakati wa kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Wachangiaji katika hotuba ya Waziri wa Fedha walikuwa wengi na hoja zilikuwa nyingi kwa hiyo, wote waliochangia watatajwa na mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ambayo ilijitokeza ni kwamba Mfuko wa *Export Credit Guarantee Scheme* ujumuishe bidhaa zote zinazouzwa nje ya nchi na uendeshwe nje ya Benki Kuu ili kuongeza ufanisi. Mfuko huu ulipoanzishwa miaka minne iliyopita ulilenga hasa Vyama vya Ushirika ambavyo vilikuwa vinapata taabu kupata mikopo ya Benki ya kununulia mazao ya wakulima. Mfuko huu sasa umeanza kutoa dhamana kwa viwanda vinavyozalisha kwa ajili ya kuuza nje. Zoezi la kupanua mfuko huu litaendelea kwa kuzingatia ushauri wa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na Msemaji Mkuu kwa masuala ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja namba sita Serikali ianzishe *mortgage financing* na *lease financing*. Uchambuzi wa mahitaji muhimu ya kuwa na mikopo ya nyumba yaani

*mortgage financing* na *lease financing* nchini unakaribia kukamilika. Matokeo ya awali ya uchambuzi huo yameonyesha kwamba kuna haja ya ama kutunga sheria mpya au kurekebisha sheria zilizopo. Uchambuzi utakapokamilika Serikali itakuja Bungeni na mapendekezo ya ama kutunga sheria mpya au kuboresha sheria zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja namba saba, suala la riba katika Mabenki na upatikanaji wa mikopo kwa jumla. Moja ya malengo makuu ya awamu ya pili ya maboresho katika sekta ya fedha yaani *Second Generation for Financial Sector Reforms* ni kuongeza ushindani na ufanisi katika sekta ya fedha nchini. Kadri ushindani unavyoongezeka na huduma za sekta hiyo kupanuka tunatarajia kuwa riba kwa amana nazo zitapanda na zile za mikopo zitashuka. Mpango unalenga kuondoa vizingiti vya kimfumo vinavyosababisha hali hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, kama ilivyoelezwa katika hotuba ya bajeti na Mheshimiwa Waziri wa Fedha Serikali imekubaliana na Benki za hapa nchini kuunda kamati ya pamoja kuangalia masuala yote yanayohusu huduma za sekta hiyo likiwemo la riba, upatikanaji wa mikopo ya uzalishaji, mikopo ya kibiashara, mikopo ya nyumba na mikopo ya ukodishaji ili yale yanayoweza kutatuliwa kwa haraka yaweze kupatiwa ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya tisa ilihusu hisa za Serikali za asilimia 21 katika Benki ya *NMB* kuuziwa wananchi. Wakati wa kubinafsisha *NMB* kwa kuuza asilimia 49 ya hisa zake Serikali iliahidi na ikawekwa kwenye sheria kwamba katika kipindi cha miezi 18 Serikali itauza kwa wananchi na kampuni za Watanzania tu asilimia 21 kati ya asilimia 51 za hisa zilizobaki. Kwa kuwa hisa za Serikali asilimia 49 ziliuzwa rasmi tarehe 30 Septemba, 2005 kwa Muungano wa wawekezaji wakiongozwa na *RABO Bank* ya Uholanzi inatarajiwa kuwa hisa hizo asilimia 21 zitauzwa kwa wananchi ifikapo mwishoni mwa mwezi Machi, 2007. Maandalizi ya zoezi hili yataanza hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja kumi na tisa ilihusu *NBC* na Benki nyingine hapa nchini kuwa na *main servers* au *data processing centres* nje ya nchi. Mwelekeo wa Makampuni duniani kwa sasa zikiwemo Benki na Taasisi za Fedha za Kimataifa ni kuwa na mahali pamoja duniani ambapo kuna *main server* ambapo ndipo mahali uchambuzi wa taarifa za kampuni husika zinapotengenezwa na kuhuishwa *(Consolidated Financial Statements).* Hivyo baadhi ya Benki ambazo ni Kampuni Tanzu za Makampuni ya Kimataifa zilizopo hapa nchini nazo zimeingia kwenye wimbi hili la utandawazi na maendeleo ya teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mabenki ya *NBC* na *Standard Chartered Bank* ni kati ya benki ambazo zina *main servers* zao na *data processing centres* nje ya nchi. Hata hivyo katika kuruhusu Benki na Taasisi za Fedha kufanya hivyo Benki Kuu inazitaka Taasisi hizo kutunza taarifa zote muhimu *(source documents)* kwenye ofisi zao hapa Tanzania ambazo ni pamoja na taarifa za kiutendaji, taarifa za bodi zao, Wahasibu na Wakaguzi. Aidha, taarifa za wateja wa Benki hizo zinapatikana wakati wowote zikihitajika bila kuchelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya 20 ilihusu mafunzo kwa wananchi vijijini ili waanzishe *SACCOS* na kuongeza upatikanaji wa mikopo wa wananchi wenye uwezo mdogo. Kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ya bajeti Serikali inatekeleza mkakati wa kupanua huduma za fedha vijijini chini ya mpango wa fedha wa pili wa marekebisho wa sekta ya fedha nchini. Hii ni pamoja na kuimarisha uendeshaji wa Benki Kata na vyombo vingine vidogo vya wananchi vya Kuweka na Kukopa *(Member Based Micro Bank Facilities)* pamoja na *SACCOS.*

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa Serikali kupitia Benki Kuu inatayarisha miongozo ya uendeshaji bora kwa Taasisi za aina hii. Baada ya miongozo hii kukamilika Serikali inaamini kwamba wananchi wa vijijini watanufaika na mpango huo kwa kuanzisha vyama vyao vya Kuweka na Kukopa ambavyo vitarahisisha upatikanaji wa mikopo vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya 21 ilikuwa ni kwa nini Benki Kuu haizuii kuporomoka kwa thamani ya shilingi yaani *exchange rate*. Kwanza kabisa nakubaliana na maelezo yaliyotolewa kwamba kushuka kwa thamani ya shilingi yetu dhidi ya fedha za kigeni kunasababisha bei za bidhaa zinazoagizwa nje kama vile chakula na mafuta kuwa juu. Aidha, nakubali kuwa kwa muda sasa shilingi yetu imeendelea kushuka ukilinganisha na dola ya Kimarekani. Kama Waheshimiwa Wabunge mnavyofahamu thamani ya shilingi ya Tanzania inawekwa na soko la fedha za kigeni ambalo linategemea ugavi na mahitaji ya fedha za kigeni *(supply and demand).* Benki Kuu huingia katika soko hilo kama muuzaji au mnunuzi wa mwisho *(buyer or seller of last resort)* pale ambapo inatokea mabadiliko makubwa ya thamani. Jambo hilo mpaka sasa halijatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ni kwamba bado tuna nakisi kubwa katika urari wa malipo ya nje. Tunaagiza bidhaa na huduma kutoka nje zaidi ya tunavyouza bidhaa na huduma zetu huko nje. Hivyo tuna nakisi katika urari wa malipo ya nje. Kwa mfano kwa hivi sasa mahitaji ya fedha za kigeni ni makubwa sana kwa ajili ya kununua mafuta, ma-*generator* ya umeme na chakula. Hali hii imechangia sana kushuka kwa thamani ya shilingi yetu katika kipindi cha miezi michache iliyopita.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sababu hizi Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Benki Kuu inatafakari hatua za kuchukua kuzuia shilingi isiendelee kuporomoka. Moja ya hatua hizo ni kupiga marufuku tabia ya wafanyabiashara hapa nchini hasa mahoteli na kampuni za simu kudai malipo ya huduma zao kwa dola ya Marekani badala ya shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha halali kwa malipo ya huduma zozote hapa nchini ni shilingi ya Kitanzania na sio fedha za kigeni. Hata hivyo ufumbuzi wa kudumu wenye matokeo makubwa ni kuongeza uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya kuuza nje ya nchi ili kuongeza ugavi wa fedha za kigeni. Kwa hiyo, hatuna budi kujizatiti kutekeleza mipango yetu ya uchumi ya kuongeza uzalishaji na kuuza kwa wingi bidhaa na huduma nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hoja ya 24 ilihusu ugawaji wa fedha kwa Halmashauri. Ugawaji wa fedha kwa matumizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa sasa unatumia *formula* maalum. Utaratibu huu ulibuniwa kutokana na hisia kwamba ugawaji wa fedha haukuwa na misingi inayohakikisha haki na usawa miongoni mwa Mamlaka tofauti kwa Serikali za Mitaa. Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanalalamika sana kuhusu utaratibu wa zamani ndipo Serikali ikatafuta utaratibu mzuri zaidi. Utaratibu huu unatumia vigezo vya kisekta kama ifuatavyo, moja, elimu, kigezo kikuu ni idadi ya watoto walio katika umri wa kwenda shule. Kigezo cha pili kilimo, idadi ya vijiji na wakazi wa vijijini na kiwango cha mvua katika mamlaka husika na cha tatu, barabara, urefu wa barabara, ukubwa wa eneo la Halmashauri, kiwango cha umaskini katika Halmashauri husika na sehemu ambazo ni maskini zaidi zipatiwe fedha zaidi. Kigezo cha nne ni maji. Idadi ya watu waishio vijijini ambao hawana huduma ya maji na kiwango cha mfuto *(equalization).* Kigezo cha tano ni afya, idadi ya watu maskini katika sehemu husika, urefu au umbali wa safari za magari kuwafikia wananchi vijijini na kiwango cha vifo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni muhimu nitoe angalizo kwamba vigezo hivi sio vya kudumu. Wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa kutoa maoni yenu na kama kutakuwa na umuhimu wa kurekebisha ama kuongeza vigezo vingine Serikali itakuwa radhi kuvitekeleza au kuyatekeleza mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, hoja ya 28 ilihusu Halmashauri mpya hazikutengewa fedha za ujenzi wa Ofisi kwa mwaka 2006/2007. Kiasi cha shilingi milioni 800 kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Halmashauri mpya kwa mwaka 2006/2007 kwa mchanganuo ufuatao, Babati imetengewa shilingi milioni 120, Kilindi imetengewa shilingi milioni 120, Tandahimba imetengewa shilingi milioni 120, Mvomero imetengewa shilingi milioni 120, Kishapu imetengewa shilingi milioni 120, Kilolo imetengewa shilingi milioni 120, Namtumbo imetengewa shilingi milioni 120 na Karatu imetengewa shilingi milioni 80. Fedha hizo zimetengwa katika bajeti ya mikoa husika ambazo Halmashauri hizo ziko.

Mheshimiwa Spika, hoja ya 39 ni kwamba Serikali imetenga fedha kwa ajili ya mikoa ya pembezoni kwa nini isiwe pamoja na mikoa iliyo nyuma lakini sio ya pembezoni kama vile Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna mikoa ambayo siyo ya pembezoni lakini iko nyuma kimaendeleo. Hata hivyo kwa mikoa iliyo pembezoni mwa nchi gharama za uendeshaji ni kubwa kuliko mikoa iliyo karibu na Dar es Salaam kama vile Pwani. Kimsingi mikoa hiyo inastahili kuongezewa fedha ili iweze kumudu gharama za uendeshaji. Gharama za kusafirisha mafuta kwa mfano ya petroli kutoka Dar es Salaam hadi Mkoa wa Kigoma, Kagera au Mwanza hailingani na gharama ya kusafirisha mafuta hayo kwenda Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mikoa ya pembezoni ambayo imepewa nyongeza ya mgao kwa ajili ya gharama za uendeshaji ni pamoja na Kigoma, Mara, Kagera, Mtwara, Mwanza, Rukwa na Lindi. Hata hivyo nia ya Serikali ni kuongeza bajeti za mikoa ili

ziweze kumudu gharama za uendeshaji. Ongezeko litategemea kadri mapato yanavyoongezeka.

Mheshimiwa Spika, hoja ya 40 ilihusu Halmashauri ya Ilala kwamba ilikuwa haijapokea fedha za kufidia vyanzo vya mapato vilivyofutwa kwa kiasi ya shilingi milioni 500. Ni kweli kabisa kwamba wakati Mheshimiwa Mbunge wa Ilala anaondoka jimboni kwake kuja Bungeni fedha za Halmashauri yake zilikuwa bado kufika. Napenda nimpongeze Mheshimiwa Mussa Zungu, kwa kufuatilia fedha zao za jimbo lao. Napenda pia kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa fedha zote za fidia zimeshatumwa kwenye Halmashauri zote mwezi huu ikiwa ni pamoja na shilingi milioni 500 za Ilala.

Mheshimiwa Spika, hoja ya 51 ni kwamba Serikali iondoe kodi ya zuio *(withholding tax)* kwenye gawio litokanalo na faida kwa Makampuni yaliyosajiliwa na Soko la Hisa Dar es Salaam. Wawekezaji katika Makampuni yaliyosajiliwa katika Soko la Hisa Dar es Salaam wamepewa unafuu wa kodi kwa upendeleo ndani ya Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 kama ifuatavyo:-

Kwanza, punguzo kwenye kodi ya zuio *(withholding tax)* inayokatwa kutoka kwenye malipo ya gawio *(dividend)* imepunguzwa kutoka asilimia 10 hadi asilimia 5.

Pili, mapato yatokanayo na uhamishaji wa umiliki wa hisa *(Transfer of shares)* hayatozwi kodi na tatu, punguzo la kodi ya mapato ya makampuni yamepunguzwa kutoka asilimia 30 hadi asilimia 25 kwa makampuni yatakayotimiza masharti yaliyotangazwa katika hotuba ya bajeti ya mwaka ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upendeleo huu mimi naona si busara kwa wakati huu kuongeza misamaha zaidi hadi hapo tutakapofanya tathmini ya matokeo ya vivutio vilivyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya 52, Serikali iondoe kodi ya mapato kwenye mikopo inayotolewa na waajiri kwa wafanyakazi. Kimsingi mikopo iwe kwa wafanyakazi au watu wengine haitozwi kodi. Endapo mikopo hiyo inarejeshwa na haijatolewa katika misingi ya kukwepa kodi. Hata hivyo Sheria ya Mapato ya mwaka 2004 inatoza kodi kwenye manufaa *(benefits)* yatokanayo na mikopo ambayo mwajiriwa anayapata kwa kupewa mkopo usio na riba au riba ndogo ukilinganisha na riba inayotozwa na Taasisi za Fedha. Manufaa hayo ni sawa na mengine mengi ambayo sheria inatambua na kujumuisha katika pato linalotokana na ajira. Lengo hapa ni kutambua kuwa unafuu wa riba unatolewa kwa mwajiri kwa kuwa tu mkopaji ni mwajiriwa wake na kwa hiyo ni sehemu ya mapato kutokana na ajira husika.

Mheshimiwa Spika, hoja ya 53 ni kuhusu msamaha wa *VAT* kwenye kahawa. Mapendekezo ya kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwa kahawa iliyosindikwa ni wadau katika sekta hiyo na yalijadiliwa na Kamati Maalum ya Kodi. Nia ni kuhamasisha walaji wa kahawa hapa nchini. Hivi sasa chai ambayo inatumika kama zao mbadala inasamehewa kodi ya ongezeko la thamani. *(Makofi)*

Hoja ya 54 ilihusu kuingiza karatasi zinazotumika kuchapisha magazeti katika mfumo wa msamaha. Katika hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipendekeza kupunguza ushuru kwa karatasi zinazotumika kuandika na kuchapisha makala mbalimbali kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10. Napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kuwa karatasi zinazotumika kuchapisha magazeti ni mojawapo ya karatasi zitakazofaidika na punguzo hilo la ushuru wa forodha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya 55 ilihusu kodi ya mazingira. Ni wazo zuri kuwa na kodi ya mazingira kwa nia ya kulinda na kuhifadhi mazingira. Hoja hii imezingatiwa katika mfumo wetu wa kodi ikiwemo kodi kwenye mifuko ya *plastic,* mafuta ya petroli, magari binafsi yenye kutumia mafuta kwa wingi na kwenye magari machakavu yanayoingizwa nchini. Hivyo pendekezo la kuongeza kodi kwa lengo la kulinda mazingira linahitaji kufanyiwa uchambuzi wa kuwahusisha wadau mbalimbali katika sekta hiyo kwa mantiki hiyo hoja hii itawasilishwa na kujadiliwa kwenye Kamati Maalum ya Kodi ambayo itatoa mapendekezo yake kwa Serikali ili yaweze kujumuishwa katika bajeti ya mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, hoja ya 58 ilihusu Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kutowasilisha Benki Kuu makusanyo yanayouzwa na mauzo ya *visa*. Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ilipewa kibali maalum cha kukusanya na kutumia mapato yake moja kwa moja katika Ofisi za Ubalozi. Utaratibu huu umesaidia kuepuka gharama kubwa ambayo Serikali ingelipata ikiwa Ubalozi ungetuma mapato yaliyokusanywa na baadaye mapato hayo kurudishwa Ubalozini kulingana na bajeti za Balozi husika kuzuia hasara kubwa kutokana na *exchange rate*. Kwani Balozi zetu zinakusanya mapato hayo kwa fedha za kigeni na zinapotumwa hapa nchini zinabadilishwa na kuwa fedha za Kitanzania. Wizara ya Fedha inapotoa mgao wa fedha kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa hutoa pungufu kwa kiasi cha makusanyo yaliyofanyika kwenye Ofisi za Kibalozi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge hakuna fedha iliyopotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya 63 ilihusu teknolojia mpya ya kukokotoa na kukusanya ushuru wa forodha. Mamlaka ya Mapato chini ya mpango wake wa miaka mitano inatumia teknolojia ya kisasa katika kukokotoa na kukusanya ushuru wa forodha *(accessing and collecting duties)* teknolojia hiyo ya *ASYCUDA plus plus* ilianza kutumika katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Kambarage Nyerere tarehe 7 Machi, 2005 baadaye teknolojia hiyo ilianza kutumika katika kituo cha huduma cha forodha *(Customs and health centre)* zamani ikiitwa *long room*, bandari ya Dar es Salaam na Tunduma.

Aidha, teknolojia hiyo imeshaanza kutumika Zanzibar bandarini na Uwanja wa Ndege tangu tarehe 1 Juni, 2006. Mamlaka ya Mapato pia ina mpango wa kusambaza teknolojia hii katika vituo vyote vikubwa vya forodha ifikapo mwisho wa mwaka huu. Manufaa ya matumizi ya mtandao huu ni kuhakikisha utoaji wa mizigo na kupunguza gharama za utunzaji mizigo bandarini.

Mheshimiwa Spika, hoja namba 64 ni utambuzi wa *TIN*. *Tax Payer Identification Number* ni namba ya utambulisho wa mlipa kodi. Namba hii ni maalum *(unique number)* na inatumika kusajili na kumtambulisha mlipa kodi katika masuala yake ya kodi zote zinazosimamiwa na Mamlaka ya Mapato pamoja na ukadiriaji kodi, ulipaji kodi kupitia Benki au Ofisi ya Mamlaka Mapato na Mawasiliano yote ya kikodi kati ya mlipa kodi na Mamlaka ya Mapato.

Mheshimiwa Spika, *TIN* haitolewi kwa walipa kodi ambao hulipia kodi zao kwa mfumo za zuio au *withholding* au makato ya mishahara *(PAYEE)* isipokuwa pale mlipa kodi anapokuwa na mapato mengine anayolipia kodi nje ya utaratibu huu. *TIN* uhitajika kwa mlipa kodi anapoingiza mali au bidhaa kutoka nje ya nchi au anaposajili gari au hati nyingine kwa Mamlaka ya Mapato.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote kabla sijachangia hoja ya Mheshimiwa Waziri natamka kwamba naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru wapiga kura wangu wa jimbo la Makunduchi walionichagua tena kwa mara ya tatu mfululizo kuwawakilisha Bungeni. Naahidi kuendelea kuwapelekea maendeleo kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa vile hii ni mara yangu ya kwanza kuchangia katika Bunge hili, nachukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa ushindi wa *Tsunami* na namshukuru sana kwa kuwa na imani juu yangu na kuniteua tena kwa nafasi hii kwa mara ya tatu. *(Makofi)*

Pia nampongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuchaguliwa na wananchi wa Monduli kwa kura ya zaidi ya asilimia 90 na pia kumpongeza kwa kuteuliwa kwake na Mheshimiwa Rais na kuthibitishwa kwa kishindo na Bunge lako Tukufu kuwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe pia pamoja na Naibu Spika, kwa kuchaguliwa kwenu. Pia nawapongeza Waheshimiwa Wenyeviti Mheshimiwa Job Yustino Ndugai na Mheshimiwa Jenista Mhagama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nami kuchangia hotuba ya Waziri wa Fedha kwa kujibu baadhi ya hoja kama ifuatavyo:-

Hoja juu ya hali ya Kiwanja cha Ndege vya Mwanza na Kagera. Ni kweli hali ya viwanja vyetu vya ndege vya Mwanza na Kagera sio ya kuridhisha kama ilivyoanishwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia hotuba ya bajeti ya Serikali. Serikali inalitambua tatizo hili na kwa kuanzia imeshafanya mazungumzo na Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Kiafrika *(BADEA)* ili kutoa mkopo wa masharti nafuu na Benki hii imekubali kuingiza Kiwanja cha Ndege cha Mwanza katika mpango wake wa

ushirikiano wa Tanzania wa mwaka 2006/2008. *BADEA* imeshapitia uchambuzi yakinifu wa ujenzi wa Kiwanja hicho na kimsingi Serikali yetu na *BADEA* tumekubaliana kuhusu utekelezaji wa mradi huu na timu ya *BADEA* itakayofanya maandalizi ya mradi itawasili hapa nchini kabla ya mwisho wa mwezi Julai, 2006. Haya yalithibitishwa na Mkurugenzi Mkuu wa *BADEA* alipotembelea Tanzania mnamo tarehe 11 hadi 13 Juni, 2006. Mradi huu unategemea kugharimu dola za Kimarekani shilingi milioni 15.3 kwa kuwa *BADEA* yenyewe haitaweza kutoa fedha zote hizo Serikali itawasiliana na Mfuko wa *OPEC* ili ichangie. Aidha, mchanganuo utaainishwa mwezi Julai 2006 kuhusu nani atatoa kiasi gani kati ya *BADEA*, *OPEC* na Serikali. Kuhusu Uwanja wa Ndege Wizara husika itaeleza wakati wa kuwasilisha bajeti yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spik,a kulikuwa na hoja juu ya daftari ya mali za kudumu za Serikali. Sheria ya fedha ya mwaka 2001 inamtaka kila Afisa Mhasibu kutunza daftari la mali za kudumu na kuambatanisha kwenye hesabu zake za mwaka jedwali linaloonyesha mali hizo na thamani yake. Kwa kuwa kabla ya kutungwa kwa sheria hiyo ya mwaka 2001 Serikali haikuwa na utaratibu huu Wizara yangu iliamua mali za Serikali zithaminiwe kwa awamu. Awamu ya kwanza ilijumuisha Wizara nane na zoezi lilihusu kuhesabu mali zote, kuandaa orodha inayoonyesha mali zinazotumika mahali zilipo, thamani yake na kubandika namba za utambulisho *(Identification Code),* kuandaa orodha ya mali chakavu na kupendekeza utaratibu na mfumo wa kupunguza thamani ya uchakavu. Zoezi hili limekamilika kwa kiwango cha asilimia 80. Awamu ya pili inahusisha Wizara 11 itaanza mwezi Julai, 2006 . Nia ya Serikali ni kutunza kumbukumbu hizo kwenye mtandao ili daftari liwe linarekebesha kila ununuzi unaofanyika kwa maana ya *LPO*, hutolewa na malipo kufanyika. Kulikuwa na hoja juu ya kuanzisha hifadhi ya mafuta, Serikali inakubali hoja hiyo kimsingi na inaifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya wananchi kuwezeshwa kupata matrekta kupitia *SACCOS*, sera ya mikopo midogo midogo yaani *micro-finance policy* ya mwaka 2000 inahimiza wananchi kujiunga katika vikundi vidogovidogo vya *SACCOS* na *SACCAS* ili wawezeshwe kupata huduma mbalimbali za kifedha ikiwemo mikopo. Kwa upande wake Serikali imeondoa kodi zote kwenye matrekta na pembejeo nyingine zote za kilimo ili ziwe na bei nafuu. Serikali imeanzisha mpango kutoa udhamini wa mikopo wa *SME's* unaolenga vikundi kama hivi. Mfuko wa Pembejeo za Kilimo ambao ulianzishwa na Serikali miaka mingi iliyopita unaweza kutoa mikopo ya namna hii kwa vikundi kama hivi. Wabunge wawahamasishe wananchi kuunda *SACCOS* na *SACCAS* ili waweze kutumia fursa hizi na kujipatia matreka. Utaratibu muafaka wa kuhakikisha kwamba matrekta yanaagizwa hapa nchini utafanyiwa utafiti yakinifu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja juu ya utoaji wa mikopo kwa wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii yaani *Pension Funds*. Mifuko ya Hifadhi ya Jamii hutoa mikopo kwa wanachama wao kwa mujibu wa taratibu walizojiwekea kwa wananchi wasio wanachama. Mikopo inayotolewa ni ya uwekezaji kwa mujibu wa sera za uwekezaji wa mifuko hiyo yaani *investment policies*. Kwa mujibu wa sera hizo wanaostahili kukopeshwa kwa utaratibu huu ni makampuni yaliyosajiliwa kisheria taasisi za umma na vyama vya ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanachama wa mfuko wanaweza kukopeshwa na mfuko wenyewe au kupitia benki ambayo ina makubaliano na mfuko husika ya kutoa mikopo wa riba nafuu, vigezo muhimu vinavyotakiwa ni kuhakikisha kuwa mradi unoombewa mkopo unakidhi kanuni na masharti ya mikopo. Kanuni hizo ni pamoja na usalama wa mtaji, faida, ukwasi na majukumu ya mfuko katika kuendeleza jamii na kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lengo kuu ni kutunza akiba ya uzeeni ya wananchama wake na mifuko haitegemei kuwa na utalaam wa kusimamia mikopo kama ilivyo mabenki. Serikali hivi sasa inaandaa mpango utakaowezesha mifuko hiyo kutoa mikopo kwa kushirikiana na mabenki. Aidha, Serikali iko kwenye zoezi la kuandaa sheria mama itakayosimamia utendaji wa mifuko ya jamii, aidha, chini ya sheria hiyo kutakuwa na muongozo wa uwekezaji yaani *investment guideline* ya mifuko ya Hifadhi ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hoja juu ya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi hakikutengewa Bajeti kwa mwaka 2006/2007. Katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika Moshi kimetengewa Bajeti ya matumizi ya kawaida pamoja na matumizi ya maendeleo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa matumizi ya kawaida chuo hiki kimetengewa jumla ya shilingi 4,989,632,000/= kwenye kifungu 280500 *Transfers and Subsidies.* Chini ya kifungu 3001 ya Elimu ya Juu katika Kitabu cha pili cha makadirio ya fedha za Serikali. Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika Moshi, ni sehemu ya Chuo Kikuu ch Kilimo cha Sokoine kwa hiyo Bajeti ya maendeleo ya Chuo Kikuu Kishiriki hicho imejumuishwa katika Bajeti ya Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kiasi cha shilingi milioni 200 kimetengewa kwa ajili ya shughuli za maendeleo za Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika kwa mwaka huu tunaoendea wa fedha 2006/2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu ni mwanzo mzuri kwa chuo hasa ikizingatiwa chuo hiki hakikuwa na bajeti ya maendeleo kilipokuwa chini ya Wizara ya Ushirika na Masoko. Wizara yangu inaandaa utaratibu wa kukipatia kasma ya maendeleo chuo hiki katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja juu ya *NMB* ina uhaba wa maafisa wa kushughulikia mikopo midogo midogo. Kama tunavyokumbuka Benki ya *NMB* ilibinafsishwa mwezi Septemba, 2005. Hivi sasa benki hiyo ipo katika harakati za kujipanga ili kutekeleza majukumu yake kukidhi matarajio ya wananchi. Juhudi hizi pamoja na kuajiri na kufunza wafanyakazi wa kutosha wenye sifa zinazotakiwa katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na usimamizi wa mikopo. Aidha, hivi karibuni tumeshuhudia matangazo kwenye vyombo vya habari vya ajira ya maofisa mbalimbali wa *NMB*.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaamini kwamba tatizo la upungufu maafisa mikopo midogo midogo katika *NMB* itakwisha sio muda mrefu ujao. Hoja kuhusu Serikali inatumia vigezo gani katika kugawa fedha za matumizi, Wizara za Fedha, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI wote hushirikiana katika kugawa fedha za matumizi kwa Serikali na vyomba vyake. Katika zoezi la kugawa

fedha za matumizi vigezo vinavyotumika au kuzingatiwa ni pamoja na mapato ya Serikali ambayo hujumuisha mapato ya ndani na yale yanayotoka kwa wahisani, deni la taifa likijumuisha *pension* pamoja na mishahara ya watumishi wa Serikali, miadi ya Serikali na maamuzi mengine ya Kitaifa, Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa Chama Tawala, dira ya maendeleo 2025, malengo ya MKUKUTA kama ilivyoainishwa na *clusters* mbalimbali na taarifa mbalimbali za utekelezaji wa Bajeti katika mwaka unaoisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara, Mikoa na Taasisi za Umma zilizohusika katika kila sekta ndiyo wanapanga matumizi yao ndani kwa kuzingatia vipaumbele pamoja na *strategic plans* zao. Kwa mfano Wizara ya Miundombinu ndiyo inayoamua ni barabara zipi za kukarabati au za kujengwa upya kwa kuzingatia kiasi cha kiwango cha mradi kilichotengwa.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine, Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ndiyo inaamua kiasi gani cha fedha ziende chuo kipi au taasisi ipi na kadhalika. Hivyo naamini Wizara za sekta zitakapowasilisha hotuba zao hapa Bungeni zitaweza kutoa maelezo ya kina kuhusu mgao wa matumizi ya fedha katika mafungu yao. Kulikua na hoja juu ya fedha za dawa za korosho ambazo ziliahidiwa na Waziri Mkuu. Fedha hizo zilitolewa na Hazina kwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa awamu mbili. Kiasi cha shilingi milioni 700 zilitolewa katika mwezi Mei mwaka huu na shilingi milioni 300 zilitolewa Juni, 2006.

Hoja kuhusu maafisa ununuzi na ugavi wanalo jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba ununuzi unazingatia sheria, kanuni zake lakini hotuba ya Bajeti haikuainisha mikakati yoyote ya kukuza ajira na kujenga uwezo wa wataalam hao.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha kwa kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Umma imeandaa mapendekezo ya kuanzishwa vitengo vya ununuzi katika kila taasisi kama ilivyoainishwa katika sheria ya ununuzi wa umma. Vitengo hivyo vitaajiri wataalam wa ununuzi na ugavi ili kutosheleza mahitaji ya Serikali na taasisi zake. Wizara pia imeeandaa mikakati ya kujenga uwezo wa wataalam wa ununuzi na ugavi ambao utaanza kutekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2006/2007. Vile vile katika mwaka huu wa fedha wa 2005/2006 mamlaka ya udhibiti wa ununuzi wa umma iliendesha mafunzo ya muda mfipi kwa maafisa ununuzi zaidi ya 1,200 kutoka Wizara zote, idara inazojitegemea na mashirika ya umma. Mwaka ujao wa fedha mafunzo hayo yataelekezwa kwenye Halmashauri za Wilaya. *(Makofi)*

Hoja kuhusu kukamata magari yenye usajili wa Zanzibar ni unyanyasaji na hakuna sheria inayokataza magari yenye usajili wa Zanzibar yasitembee Tanzania Bara. Usajili wa magari Tanzania unasimamiwa na sheria mbili tofauti za Bara na Visiwani. Sheria hizo ni sheria ya usalama barabarani ya mwaka 1973 ya Tanzania Bara na sheria ya usafiri wa barabara ya mwaka 2003 ya Zanzibar. Ni kweli kwamba kuwepo kwa sheria mbili tofauti kunasababisha kero kwa wananchi wa Zanzibar wanapotaka kutumia magari yaliyosajiliwa kwa Tanzania Bara. Suala hili litapelekwa katika tume

inayosimamia kero za Muungano ili kuangalia uwezekano wa kuwa na sheria moja au kila sheria kuruhusu utumiaji wa magari yaliyoandikishwa chini ya sheria nyingine.

Katika mchakato wa kusajili magari katika mfumo mpya kwa mujibu wa sheria Tanzania Bara, Mamlaka ya MapatoTanzania imekamata magari 78 ya Tanzania Bara mengi ya kifahari yaliyolipiwa ushuru pungufu na hivyo kukusanya jumla ya shilingi 378,434,562/= kwa ushuru uliokwepwa na faini. Aidha, Mamlaka ya Mapato Tanzania imefanikiwa kukamata magari mengine 806 yaliyokuwa na usajili bandia au ubadilishaji batili *(illegal transfers)* na kukusanya kodi na faini zenye thamani ya shilingi 209,429,962. Vile vile wakati wa uandikishaji magari hayo kwenye mfumo huu mpya magari 174 yenye namba za Zanzibar yaligunduliwa kulipwa ushuru pungufu. Kodi ya shilingi 66,775,573 ilikusanywa kufidia upungufu uliodhihirika. Hivyo zoezi hili halilengi tu magari ya usajili ya Zanzibar bali pia magari ya usajili wa Tanzania Bara na halikufanywa kwa ubaguzi bali lilihusu magari yote na yalizingatia sheria zote zilizopo.

Sambamba na hili Mamlaka ya Mapato inaendelea kufanya uchunguzi kuhusu ukwepaji huo wa ushuru wa magari na kwa vifungu vingine yaliyojitokeza ili kuona kama kuna maafisa waliohusika moja kwa moja kusaidia ukwepaji huo ili hatua za kinidhamu zitachukuliwa kwa mujibu wa taratibu za mamlaka. Ili kuondoa tatizo la ukadiriaji ushuru pungufu wa magari kwa upande wa magari kwa upande wa Zanzibar na Tanzania ambao unalazimisha ukadiriaji wa pili Mamlaka ya Mapato imefunga mtandao wa *ASYCUDA plus plus* ambao unahakikisha viwango vya ukadiriaji wa ushuru na taarifa za ushuru uliolipwa zinakuwa kwenye mtandao na zinalingana ili kupunguza kero wakati wa uhamishaji wa umiliki na usajili mpya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgao wa fedha kwa sekta ya kilimo imetolewa hoja kwamba mgao wa fedha kwa sekta ya kilimo ni mdogo na hasa ukilinganisha na malengo tuliyokubaliana chini ya mpango wa *SADC* wa kugawa asilimia kumi kwa Bajeti ya sekta hiyo. Napenda kurudia kusema kuwa kweli ina maaeneo mengi ya upendeleo chini ya MKUKUTA yaliyopewa kipaumbele katika mgao wa fedha kila mwaka na sekta ya kilimo ni moja ya maeneo hayo yaliyopewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, sekta ya kilimo kwa tafsiri pana ikijumuisha kilimo, uvuvi, ufugaji, masoko na barabara vijijini imetengewe jumla ya shilingi bilioni 271.8 ongezeko la shilingi bilioni 38.5 au asilimia 16.5. Ukilinganisha na Bajeti ya mwaka uliopita. Kiwango hicho cha shilingi bilioni 271.8 ni sawa na asilimia 6 ya matumizi yote ukiondoa deni la taifa hivyo tunaendelea hatua kwa hatua kuongeza mgao wa fedha kwa sekta hii ili kufikia malengo ya *SADC* kadri ya hali ya fedha itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, wakati juhudi za kuongeza mapato ya ndani zikiendelea Serikali inaendelea kujadiliana na wahisani mbalimbali ili nao waongeze misaada yao na mikopo yao ya masharti nafuu.

Hoja kuhusu sababu ya upungufu wa fedha za misaada kwa miradi ya maendeleo. Katika fedha za nje kuna misaada *(grants)* na mikopo *(loans)*. Misaada iliyotolewa kwa njia ya fedha taslimu yaani *cash* na njia ya vifaa au huduma ambavyo vinapelekwa moja

kwa moja kwenye miradi husika kwa namna ya vifaa au huduma. Sababu za kutohesabika kwa fedha zote za maendeleo ni pamoja na hizi zifuatazo. Kwanza baada ya nyaraka zilizotumika kununuliwa vifaa zilikosekana au ama kupatikana baada ya mwaka wa fedha husika kupita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali hii inasababisha baadhi ya vifaa vya misaada kutoingizwa katika hesabu. Sababu hii ilichangia kupunguza kiwango cha utekelezaji wa miradi husika. Pili, baadhi ya huduma za kupewa wataalam ilikuwa vigumu kuthaminiwa kutokana na kutokujua mishahara yao na hivyo kusababisha sehemu ya matumizi ya fedha katika miradi ya husika kutoingizwa katika kumbukumbu hali iliyosababisha kiwango cha utekelezaji wa miradi husika kupungua, na tatu fedha ziizoahidiwa na baadhi ya wahisani hazikutolewa kabisa bali ni hali ambayo pia ilichangia kupunguza kiwango cha utekelezaji kwa miradi husika. Aidha, mwaka wa Fedha 2005/2006 haujaisha hivyo ni mapema mno kujua kama kiwango cha utekelezaji kitafikia au hakitafikia asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kutatua matatizo yaliyotajwa hapo juu, Wizara imechukua hatua mbalimbali za kuboresha utaratibu wa kihasibu mapato na matumizi yatokanayo na misaada ya wahisani. Hoja ya matumizi ya fedha ya kawaida, ni kweli kwamba matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mwaka 2003/2004, ulikuwa na matumizi zaidi ya Bajeti. Hata hivyo maelezo zaidi ya *statement of the expenditure* yatawasilishwa katika Bunge lako Tukufu kulingana na ratibu ya Vikao vya Bajeti vya 2006/2007. *(Makofi)*

Kuhusu masurufu yasiyorejeshwa katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, ni kweli kulikuwa na masurufu yasiyorejeshwa mnamo tarehe 30 Juni, 2005 ya shilingi 2,183,938,622 wakati tukifunga mwaka wa fedha. Masurufu hayo yalitolewa kwa ajili ya shughuli za Serikali katika Wizara na Idara mbalimbali mwezi wa fedha lakini yalirejeshwa baadaye. Kwa sasa masurufu yamerejeshwa kwa kiwango kikubwa na bakaa wahusika wanakatwa mishahara yao.

Kuhusu hatua zilizochukuliwa kwa Wizara zinazopata hati chafu, kabla ya hatua hazijachukuliwa kuhusu wale wanaopata hati chafu sababu za kupata hati hizo zinachunguzwa na kisha hatua kuchukuliwa. Aidha, Wizara ya Fedha imefanya yafuatayo ili kuzuia kutokea kwa hati chafu. Kwanza inaboresha mfumo mzima wa uhasibu, pili imesomesha na inaendelea kuwasomesha wahasibu wote kuanzia Serikali Kuu hadi Halmashauri zote na tatu ni *Search Agent Penalty Regulation* ya mwaka 2005ambapo adhabu zimeainishwa na zitaanza kutumika kwa wale wote wanaokiuka taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga hoja mkono. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa namwita mtoa hoja wa kwanza Mheshimiwa Waziri wa Mipango Uchumi na Uwezeshaji. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii kukushukuru kwa dhati kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa muhtasari wa maelezo kuhusu hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Vile vile naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao ya hapa Bungeni kwa kauli na vile vile ya maandishi. Vile vile na mimi naomba nimpongeze Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Meghji, kwa hotuba ya Bajeti nzuri, muafaka ambayo haijawahi kutokea, nami naiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Tatu, naomba niwashukuru Mwenyekiyi wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni na Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, ambaye ni Waziri mwenzangu, lakini yeye ni kivuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja na michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika kujadili hotuba yangu inaonyesha nia yetu thabiti ya kuendeleza gurudumu la maendeleo la nchi yetu. Kwa ujumla hoja na michango hii mingi imelenga katika mageuzi ya kilimo, uboreshaji wa miundombinu ya barabara, uwezeshaji wa wananchi kiuchumi upatikanaji wa uhakika wa nishati, elimu, maji, uwajibikaji wa utekelezaji na uboreshaji wa michango ya sekta mbalimbali katika pato la Taifa. Yote haya kwa kweli yanalenga katika kutekeleza kwa nguvu zaidi Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005. Napenda kusisitiza tu kwamba utekelezaji wa Ilani ya Chama chetu ni ya miaka mitano na mpango na Bajeti hii ni ya mwaka wa kwanza katika mchakato wetu huu wote. Kwa hiyo, nina matumaini kwamba kila tunavyoendelea tutaendelea kupanga na kutekeleza ilani kwa nguvu zaidi na kuweza kufanikiwa malengo yetu ifikapo mwaka 2010. Vile vile tukumbuke kwamba kupanga ni kuchagua kama alivyotufundisha Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia hapa Bungeni wachangiaji wote walikuwa 96 lakini waliochangia kwa maandishi walikuwa nane kwa waliochangia humu ndani ni 87.

Kwanza, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Fedha na Uchumi, pili Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Thomas Mwang'onda, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Suleiman Saddiq, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Joyce Machimu na Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

Wengine ni Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Dr. Omari Nibuka, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Damas Nakei,

Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Balozi Hamis Kagasheki, Mheshimiwa Juma Suleiman Nh'unga, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Siraji Kaboyonga, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Mussa Zungu, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Stephen Galinoma na Mheshimiwa Elizabeth Batenga.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa Fred Tungu, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Elisa Mollel, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Ezekiel Maige na Mheshimiwa Aggrey Mwanri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Charles Kajege, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi na Mheshimiwa Phares Kabuye.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Dr.Guido Sigonda, Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu na Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa.

Wengine ni Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Sameer Lotto, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Amina Mpakanjia, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Salome Mbatia, Mheshimiwa Mustafa Mkulo na Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya na Mheshimiwa Susan Lyimo.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Salome Mbatia, Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, katika kunisaidia kujibu baadhi ya hoja hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nipitie hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo, kwanza hoja imetolewa na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda ambazo ziko

nyingi lakini nitazitaja zifuatazo, kwanza mpango na Bajeti zetu lazima ziwe nyenzo yaani *tools* za kuchochea malengo ya jumla badala ya kuwa ni zoezi la utaratibu tu.

Ushauri huu ni mzuri na tutaendelea kuuzungatia na Serikali mara zote imekuwa ikitumia mpango na bajeti katika kutekeleza shughuli zake na ndiyo maana mipando na katika kutekeleza shughuli zake na ndiyo maana mipango na bajeti hubadilika mwaka hadi mwaka. Kwa kuzingatia vipaumbele vilivyokubaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbili, mipango iwe endelevu, iimarishwe na kuboreshwa ili uchumi ukue zaidi na huduma kwa wananchi ziongozeke. Ushauri huu ni mzuri na umezangatiwa katika maandalizi ya mikakati ya mipango ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, aidha, juhudi zaidi zinaendelea kufanywa ili kuimarisha na kuboresha utekelezaji wa mipango na hali kadharika katika ngazi zote za Serikali. *(Makofi)*

Tatu, mpango wa Bajeti za Serikali hazina budi kujiwekea utaratibu na mikakati inayolenga hasa katika kutatua na kutoa ufumbuzi wa changamoto zilizopo zilizosababisha upungufu wa chakula na nishati ya umeme. Ni kweli pia mikakati ya Serikali huzingatia vipaumbele kulingana na changamoto zilizopo, ukame ukiwa ni changamoto moja wapo ya mwaka huu wa fedha yaani 2006/2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nne kuna haja baada ya mipango na Bajeti kuwasilisha Serikali ipange ipi ianze ipi ifuate. Ni utaratibu wa Serikali wa kuandaa mpango wa kazi unaozingatia vipaumbele. Aidha, utaratibu huu utaendelea kuboreshwa ili uwe na mafanikio zaidi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu kutokana na ufinyu wa rasilimali hatuna budi kuelekeza fedha za kutosha katika maeneo machache yatakayochochea maendeleo yetu kwa haraka zaidi na hivyo kuahirisha au kuzipa rasilimali kidogo shughuli zingine na tano, Serikali iendelee kuimarisha uwezo wa viwango vya Taifa vya hifadhi vya chakula kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Taifa pamoja na kurejea uwamuzi wa makusudi wa kuanzisha hifadhi ya mafuta ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, lakini pia imetolewa na Mheshimiwa Elisa Mollel na Mheshimiwa Ezekiel Maige. Maelezo ni utaratibu, ushauri wa Kamati wa kuhusu hifadhi ya chakula unazingatiwa aidha, uanzishwaji wa hifadhi ya Taifa ni ushauri mzuri na Serikali itaufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine, umefika wakati wa mpango kabambe wa kilimo cha umwagiliaji utekelezwe wa nguvu zaidi na sambamba na upatikanaji wa pembejeo na huduma za ugani yaani *extension services*, Mheshimiwa Ephraem Madeje, Mheshimiwa herbert Mntangi, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo na Mheshimiwa Yono Kevela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri huu ni mzuri Serikali inaendelea kuboresha na kutekeleza mpango kabambe wa kilimo cha umwagiliaji maji yaani *irrigation master plan* kwa kuzingatiua uwezo uliopo mikakati na mipango mbalimbali imeandaliwa kutekelezwa ili kukuza kilimo chetu kama vile programu ya maendeleo ya sekta ya kilimo, mkakati wa maendeleo wa sekta ya kilimo na mkakati wa maendeleo vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi ya umwagiliaji inayoendelea ni pamoja na *Small Holder Development Program for Marginal Areas* na mwingine unaitwa *Participatory Irrigation Development Program* na *Agricultural Sector Pprogram Support* na *River Basin Manament Program*. Miradi hii iteelezwa kwa kina na Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika na vile vile Waziri wa Maji wakati wakiwasilisha Bajeti zao hapa Bunguni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taaluma na manufaa ya kuvuna maji ya mvua na ujenzi wa mabwawa na malambo ya hifadhi ya maji izingatiwe, hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda pamoja na Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Mariam Kasembe na Mheshimiwa Damas Nakei.

Mheshimiwa Spika, ushauri huu unazingatiwa, Serikali inahimiza taaluma ya kuvuna maji ya mvua ya ujenzi wa mabwawa na malambo hasa kwenye maeneo yenye ukame ambapo mikakati mbalimbali imeboreshwa na kuzingatiwa katika mipango na hili litazungumzwa vizuri na Waziri wa Maji, Waziri wa Mazingira pamoja na Waziri wa Maendeleo ya Mifugo. *(Makofi)*

Taifa ya maendeleo 2025 MKUKUTA na Ilani na CCM ya Uchaguzi ya mwaka 2005 ambavyo viliandikwa kwa kushirikisha wadau wote kwa kina. Maandalizi ya mipango na Bajeti ni mchakato shirikishi ambao hufanywa hatua kwa hatua.

Waheshimiwa Wabunge, hata hivyo kupitia Kamati mbalimbali hupata fursa ya kutoa maoni na michango yao ambayo huzingatiwa kikamilifu katika kukamilisha matayarisho ya mpango na Bajeti katika mwaka husika. *(Makofi)*

Halafu suala la kuanzisha Vituo vya Matrekta ili wananchi wakodishe badala ya kuendelea kutumia jembe la mkono, waliozungumzia hilo ni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya na Mheshimiwa Mollel. Kutokana na Serikali kujiondoa katika shughuli za kibiashara, itaendelea kuhimiza Sekta Binafsi kuanzisha na kuendesha Vituo vya kukodisha Matrekta kwa wakulima. Aidha, Serikali itaangalia utaratibu muafaka ikiwa ni pamoja na kutumia utaratibu wa *leasing and high purchase* ili kuwawezesha wananchi kupata mikopo ya matrekta.

Suala la matrekta ni muhimu katika kuboresha kilimo chetu. Serikali izingatie vyanzo vya mbadala vya nishati hususan kutokana na mazao kama mawese, nazi,

korosho, pamba, miwa na gatrofa, ni ushauri mzuri na Serikali itaendelea na juhudi za kuhakikisha wananchi wanapata nishati kwa kutumia vyanzo mbadala.

Aidha, Serikali kupitia mpango wa *mini-tiger* 2020 imepanga kuanzisha kilimo cha mazao yatakayozalisha *bio fuel*. Hivi sasa tunavyosema, Serikali imeshaunda Kamati ya Watalaam ya *bio fuel.* Kwa hiyo, jambo hili tunalitilia mkazo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vitambulisho vya Taifa, alizungumzia Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Kwa kushirikisha wadau mbalimbali, Serikali imeazimia kuanza kutekeleza mradi huu katika mwaka huu wa fedha 2006/2007. Kwa hiyo, tunalitambua hilo.

Pia, juu ya nchi iwe na Kanda za Maendeleo na kila Mkoa utayarishe mipango ya maendeleo na programu za utekelezaji kwa kuangalia *regional profiles,* ametoa ushauri huo Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya. Ushauri huu utazingatiwa na Serikali itaendelea na zoezi la kuhuisha vitabu vya hali ya uchumi na maendeleo ya jamii ya Mikoa na Wilaya ili isaidie kuibua fursa za uwekezaji wa ndani na nje. Aidha, Mikoa inashauri kutoa kipaumbele katika kujitayarishia taarifa za hali ya uchumi na maendeleo ya Mikoa yao ili kuainisha fursa na maeneo kwa lengo la kuvutia Wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezeshaji wa wananchi kiuchumi uwe kwa Wizara zote, hili walizungumzia Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Mollel na Mheshimiwa Martha Mlata. Dhana nzima ya uwezeshaji inalenga katika kuwapa wananchi upendeleo maalum kwa kuwapatia huduma bora za elimu na mafunzo ya ujasiriamali, kujenga miundombinu na kuwapa fursa za kushiriki katika kubuni, kupanga na kutekeleza mipango ya uchumi. Uwezeshaji wa wananchi kiuchumi ni suala mtambuka. Kama ilivyo kwenye hotuba yangu ya hali ya uchumi, Sekta zote zina wajibu wa kupanga na kutekeleza mipango na mikakati ya kisekta ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi.

Pia, takwimu zionyeshe malengo yaliyowekwa na mafanikio yaliyofikiwa. Hilo ameliongelea Mheshimiwa Dr. Mzindakaya. Ushauri huu unazingatiwa na Serikali imekuwa ikifanya hivyo na itaendelea kuboresha kwa kutoa takwimu kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa.

Halafu Serikali ihamasishe uanzishwaji wa *SACCOS* katika jamii na kuhakikisha *SACCOS* hizo zinawezeshwa kwa mafunzo na uendeshaji na mitaji na mikopo. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Kahama, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Yono Kevela na Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi. Serikali inakubaliana na hoja hii ya Waheshimiwa Wabunge, ni kweli kabisa kwamba jukumu la kuhamasisha jamii kuunda *SACCOS* ni la Serikali hasa ikizingatiwa kwamba kwa kupitia *SACCOS* azma ya Serikali kupunguza umaskini wa kipato kwa walengwa na hasa walio Vijijini inaweza kufikiwa.

Mabenki na asasi nyingi hazijahamasika vya kutosha na kuwa na uwezo wa kutoa huduma za akiba na mikopo. Suala hili limezungumzwa na Waziri wa Fedha. Tutaendelea kulishughulikia ili tuweze kupata mafanikio makubwa zaidi.

Vile vile, barabara ya Korogwe – Handeni – Turiani – Dumila- Kilosa – Mikumi amezungumzia Mheshimiwa Suleiman Saddiq. Uamuzi umeshafanyika wa barabara hii kujengwa kwa kiwango cha lami, ufafanuzi utatolewa na Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu. *(Makofi)*

Pia, Serikali ipime maeneo na kutoa hati ambalo wameliongelea Mheshimiwa Joyce Machimu na Mheshimiwa Charles Keenja. Serikali inaendelea na zoezi la kupima maeneo na kutoa hati. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi itatoa maelezo ya kina kuhusu suala hili.

Vile vile juu ya idadi ya wanawake ngazi za maamuzi iongezeke ili ifikie asilimia 50 ambalo limezungumzwa na Mheshimiwa Joyce Machimu, Serikali inaendelea kuwapa uwezo wanawake kwa kuwapatia fursa za elimu ili waweze kushindana na kushiriki katika ngazi mbalimbali za maamuzi.

Halafu Serikali ijenge nyumba na kuwauzia watumishi, hili amelizungumzia Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir. Utaratibu unafanyika kuanzisha *mortgage and leasing finance*. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mwongozo wa Spika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa saa 7.00 imefika na kwa kuwa hatujatengua Kanuni....

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ndiyo shida ya kutokuwemo Ukumbini. Kanuni ilikwishatenguliwa na Bunge hili, ndiyo maana nimemruhusu Mheshimiwa Waziri aendelee. *(Makofi)*

**MHE. WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utaniongeza dakika tano zingine kufidia mambo haya. Pia Mheshimiwa Nibuka, kuanzia mwaka wa 2006/2007 kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Ofisi ya Waziri Mkuu Tamisemi Wizara ya Mipango na Uwezeshaji, imeazimia kufanya ufuatiliaji wa kila robo mwaka ya utekelezaji wa Bajeti na mpango kwa kufuata maeneo makuu ya MKUKUTA. Kwa hiyo, hili kila kitu tutafanya.

Halafu baadhi ya wawekezaji wanakwamishwa, amelichangia Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, kupitia MKUMBITA. Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, ikiwa ni pamoja na kubadilisha utoaji wa huduma na mtazamo wa Sekta ya Umma kuhusu Sekta Binafsi.

Malighafi nchini zitumike katika viwanda, amelizungumzia Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, sawa kabisa Serikali inaendelea kuhimiza uzalishaji wa malighafi kwa wingi na kwa ubora unaotakiwa kwa ajili ya masoko ya ndani na masoko ya nje.

Wananchi wasaidie kuandika mchanganuo wa miradi *(project write up and appraisal)* amezungumzia Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro. Kama ilivyobainishwa katika Sera ya Taifa ya Uwezeshaji, Serikali inahimiza Halmashauri za Wilaya zijenge uwezo wa kuandaa na kuchanganua miradi. Aidha, Chuo cha Mipango cha Maendeleo Vijijini Dodoma kinatoa mafunzo ya uandaaji na uchambuzi wa miradi. Kwa hiyo, tunashauri, Halmashauri na wahitaji wengine kuwapeleka watumishi kupata mafunzo katika Chuo hiki ili waweze kusaidia wananchi katika kuibua na kuchanganua miradi ya maendeleo.

Halafu suala la kuwa na *SEZ* za kilimo amelizungumzia Mheshimiwa Simbachawene na Mheshimiwa Zambi. Vile vile, Mheshimiwa Mwang'onda tunapokea ushauri huu na tunapenda kuwahamasisha Waheshimiwa Wabunge kuwa katika maeneo ya *SEZ* kuna nafasi pia kwa ajili ya kilimo, misitu na shughuli nyingine za kiuchumi *SEZ* inachukua uwigo mpana zaidi wa shughuli za kiuchumi.

Je, uvuvi unachangiwa kiasi gani katika pato la Taifa? Ameuliza Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir. Mchango wa Sekta zote katika pato la Taifa umeonyeshwa katika jedwali Na. 4 (b) katika kitabu cha hali uchumi wa mwaka 2005 ambacho Waheshimiwa Wabunge, wamepewa nakala. Aidha, Sekta Ndogo ya Uvuvi imechangia asilimia tatu katika pato la Taifa katika mwaka 2005.

Pia, kuhusu mikopo ya huduma ya Benki kwamba vielekezwe Vijijini, ambalo amechangia Mheshimiwa Juma Njwayo, Serikali itaendelea kushawishi mitandao ya Benki hadi Wilayani na Vijijini. Aidha, huduma za miundombinu ya nishati ya mawasiliano na barabara itaendelea kuboreshwa ili kuwavutia wawekezaji katika Sekta hizi Vijijini. Vile vile, natoa wito tuendelee kuanzisha Benki za Wananchi. Hivi ndio vyombo vyetu vizuri vya kutuwezesha.

Pia, kuhusu kuunganisha barabara za Vijiji ambalo limezungumzwa na Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Lwanji, Mheshimiwa Njwayo. Maelezo yatatolewa na Wizara husika.

Wafugaji wahamishwe maeneo yaliyoandaliwa, hilo limezungumzwa na Mheshimiwa Juma Nh'unga. Tunashukuru kwa ushauri huu na Serikali ndivyo inavyofanya katika kuhakikisha kwamba wafugaji wanahamia katika maeneo yaliyotengwa tayari. Vile vile, tunaendelea na *land use planning* ili kuepusha migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Pia, Reli ya Kati ijengwe upya ili iweze kuwa kitega uchumi, wamelizungumzia Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Batenga na Mheshimiwa Ezekiel Maige. Serikali imedhamiria kuikarabati Reli ya Kati ili ifikie kiwango kizuri cha kuweza kutoa huduma bora na kwa ufanisi kwa wasafiri na mizigo. Suala hili linazingatiwa kikamilifu

katika mchakato wa kukodisha uendeshaji wa reli hiyo kwa mwendeshaji binafsi. Aidha, ukodishaji wa reli hiyo utakwenda sambamba na ukarabati wa hiyo reli.

Utekelezaji wa *vision* 2025 umefikia wapi? Mheshimiwa Peter Serukamba ameuliza. Tangu kuanza utekelezaji wa dira ya mwaka 2000 mafanikio katika baadhi ya malengo yake ambayo yameainishwa katika Kitabu cha Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 yameshafikiwa na maendeleo katika viashiria vingine yana matumaini ya kufikiwa. Kwa ujumla, utekelezaji wa dira umefanyika vizuri kupitia sera, mikakati na mipango mbalimbali na mafanikio yake yameanza kuonekana katika viashiria mbalimbali kama vile vya kutengemaa kwa uchumi jumla, kupungua kwa viwango vya umasikini, kupatikana kwa huduma za jamii kama vile mafanikio yaliyofikiwa katika Elimu ya Msingi na hata katika Elimu ya Sekondari, upatikanaji wa maji safi na salama, kupungua kwa vifo vya watoto wachanga na vya wazazi.

Takwimu zinaonyesha mwenendo wa viashiria nilivyovitaja hapo juu na vingine ambavyo sijavitaja na namwomba Mheshimiwa Mbunge asome kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa cha mwaka 2005 na kile cha hali ya umasikini na maendeleo ya watu cha mwaka 2005 ambavyo kila mmoja wenu ana nakala zake.

Bajeti ya barabara ya mwaka 2006/2007 ni asilimia 40 ya mahitaji. Wameliongelea Mheshimiwa Serukamba, Mrope, Galinoma na Mheshimiwa Kigwalilo. Mahitaji ya fedha kwa Sekta ya Barabara ni makubwa, hivyo Serikali haiwezi kukidhi mahitaji yote katika mwaka mmoja wa fedha. Mikakati inaendelea kuboreshwa ili fedha inayopatikana iweze kutumika kikamilifu kufuatia vipaumbele. Aidha, katika hotuba yangu ukurasa wa 78/80 ya aya 111 mpaka 112 nimeelezea kwa kina kuhusu changamoto tulizonazo ikilinganishwa na rasilimali zetu finyu na kwamba tunahitaji kuangalia upya vipaumbele vyetu na kuamua kutoa rasilimali za kutosha kwa shughuli chache ambazo zitachochea uchumi kwa haraka zaidi na kuharakisha maendeleo yetu katika utekelezaji wa shughuli zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Kama nilivyotangaza mapema kwamba majumuisho ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, ndiyo yanatufikisha mwisho wa shughuli za asubuhi. Lakini kwa sababu jioni tunapitisha Bajeti au kutokuipitisha ni kwamba yapo matakwa ya Katiba na Kanuni zetu ambayo lazima niwasomee mjue uzito wa shughuli ya jioni.

Kwa mujibu wa Kanuni zetu Kanuni ya 79 (1) inasema hivi mjadala kuhusu hotuba juu Bajeti utaendelea kwa muda usiozidi siku tano, mara baada ya kumalizika mjadala huu juu ya hotuba ya Bajeti Spika, atalihoji Bunge litoe uamuzi wake wa kupitisha au kutokupitisha Bajeti hiyo ili kukidhi matakwa ya ibara ya 90 (2) (b) ya Katiba. Kwa sababu hiyo, kura zitapigwa kwa kuita jina la Mbunge mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapa sitawahoji kwa ujumla tu kwamba anayeafiki aseme ndiyo au hapana. Nitaita jina moja baada ya lingine hadi majina yote 320. Kwa

nini tunafanya hivyo? Tunafanya hivyo ili kukidhi matakwa ya Katiba mabayo yanampa mamlaka na madaraka Rais wa Tanzania kulivunja Bunge kwa mujibu wa Katiba kifungu cha 90 (2)(b) kama Bunge limekataa kupitisha Bajeti iliyopendekezwa na Serikali. Ndiyo maana inatubidi tufanye hivyo. Kwa hiyo, nahimiza tu kwamba Waheshimiwa Wabunge, sote tuhudhurie ili kila mtu aweze kupiga kura yake na kupata uamuzi ambao unalingana na matakwa ya Katiba na Kanuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni. *(Makofi)*

*(Saa 07.16 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*
*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mtoa Hoja ili aweze kuongea, nawaombeni muwe na subira ili tuweze kuwatambua Wageni. Kwanza, wageni wa Mheshimiwa Dr. Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe na Rais wa Bunge la Afrika ambao ni Wajumbe saba wa Mkutano Mkuu wa Taifa wa Chama cha Mapinduzi wanaotoka Wilaya ya Ukerewe, hawa waliosimama upande wa kulia. Karibuni sana. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Pamoja na hilo, kuna Wageni ambao ni Wajumbe pia wa Mkutano wa Taifa kutoka Mkoa wa Kagera, wako 11 wakiongozwa na Mwenyekiti wa UWT wa Mkoa, ni Wageni wa Mheshimiwa Elizabeth Batenga na Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, ni wale pale! *(Makofi)*

Nilikuwa na taarifa pia kwamba Mheshimiwa Peter Kisumo, Mzee wetu ambaye ni mmoja wa Waasisi wa mapambano dhidi ya Ukoloni alikuwa yumo humu, lakini simwoni, lakini nadhani baadaye atakuja.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu, hoja yetu iliyoanza asubuhi na inayoendelea na sasa inahitimishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kutoa shukrani za dhati kwako kwa kunipa nafasi jioni hii ili niweze kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Napenda kushukuru pia Manaibu Waziri wawili ambao tayari wameanza kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kutoa shukrani za dhati kwa Naibu Spika, Mheshimiwa Anne Makinda - Mbunge wa Njombe Kusini pamoja na Wenyeviti wa Bunge akiwemo Mheshimiwa Jenista Mhagama - Mbunge wa Peramiho na Mheshimiwa Job Ndugai - Mbunge wa Kongwa kwa kuongoza mjadala wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2006/2007, kwa kweli pamoja na wewe kwa umahiri mkubwa sana wa kuliongoza Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii, kutoa shukrani za dhati kabisa kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Abdallah Kigoda

- Mbunge wa Handeni kwa kuwasilisha kwa ufasaha mkubwa sana maoni ya Kamati yake. Kwa dhati kabisa, napenda kusema kwamba maoni yake pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi yametusaidia sana katika utayarishaji wa Bajeti hii. Wametoa mawazo ambayo kwa kweli tunaweza kusema ni mawazo ya kujenga na siyo mawazo ya kubomoa.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed - Mbunge wa Wawi ambaye ni Msemaji Mkuu wa Upande wa Upinzani kwa masuala ya Fedha. Pia, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto - Mbunge wa Kigoma Kaskazini, ambaye ni Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu masuala ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia ndani ya Bunge hili, waliochangia pia kwa mawazo nje ya Bunge, lakini pia waliotuandikia na kutoa mawazo yao. Naamini kabisa kwamba nitakuwa sisemi kweli nikisema kwamba hoja zote nitaweza kuzijibu. Lakini hoja zote tumezichukua ambazo za umuhimu mkubwa sana, kuna nyingine ambazo zitatumika katika utekelezaji, lakini kuna zingine pia zitatumika katika utaratibu wa mpango wa Bajeti ya mwaka ujao *inshallah*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, wamechangia kwa kuzungumza na kwa maandishi. Ningependa kuchukua nafasi hii kuwatambua kwanza kabisa wale ambao waliochangia kwa kuzungumza.

Kwanza ni Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda - Mbunge wa Handeni ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha ya Uchumi, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed - Mbunge wa Wawi na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa upande Fedha na Mheshimiwa Kabwe Zitto - Mbunge wa Kigoma Kaskazini na Msemaji Mkuu kwa upande wa Mipango. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mheshimiwa Mwang'onda, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Faustine Rwilomba, Mheshimiwa Gakeya Mabina, Mheshimiwa Joyce Hamanilo Machimu, Mheshimiwa Janeth Kahama, Mheshimiwa Suleiman Saddiq, Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mheshimiwa Dr. Omar Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Dr. Suleiman Omar Kumchaya, Mheshimiwa Dorah Herial Mushi, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Mwandoro, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Simbachawene, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Juma Kilimba, Mheshimiwa Nyami, Mheshimiwa Kaboyonga, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Galinoma na Mheshimiwa Balozi Khamis Sued Kagasheki. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mheshimiwa Juma Nh'unga, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa Rished Abdallah, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Fred Tungu,

Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Elisa Mollel, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Devota Likolola, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Aggrey Mwanri Mheshimiwa Herbet Mntangi na Mheshimiwa Mariam Kasembe. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Charles Kajege, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Kidawa Salehe, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanga, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Phares Kabuye, Mheshimiwa Dr. Raphael Masunga Chegeni, Mheshimiwa Dk. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Guido Sigonda, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mheshimiwa Mohamed Chomboni, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo na Mheshimiwa Abdul Jabiri Marombwa. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Sameer Lotto, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, Mheshimiwa Ndesamburo, Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia ambaye ni Naibu Waziri Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Mustafa Mkulo - Naibu Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib -Naibu Waziri wa Fedha pamoja na Mheshimiwa Juma Ngasongwa ambaye ni Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Wote nawashukuru sana. *(Makofi)*

Wale ambao walichangia kwa maandishi ni Waheshimiwa wafuatao:-

Kwanza ni Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, Mheshimiwa Abbas Jecha, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Richad Nyaulawa, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kanali Feteh Said Mgeni na Mheshimiwa Aloyce Kimaro. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mwaka Ramadhani, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Manju Salum, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Abdallah Salum Sumri, Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Phillemon Sarungi na Mheshimiwa Makwetta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani za dhati kwenu nyote na kama kuna wengine ambao kwa kweli sijawataja, naomba radhi, labda wanaweza kuwa walichangia kwa maandishi lakini kama sijawataja pia wanaweza kuleta vikaratasi naweza kuwataja kabla sijamaliza.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Serikali ina thamini sana michango yote ya

Waheshimiwa Wabunge na inachukua kama nyenzo muhimu ya kuboresha utekelezaji wa Bajeti hii ili malengo yake yafikiwe kwa maisha bora ya Watanzania wote siku zote.

Mheshimiwa Spika, sasa nitoe maelezo kuhusu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Napenda kwa mara nyingine nitoe shukrani za dhati kwa Kamati ya Fedha na Uchumi. Ushauri wa Kamati ya Fedha na Uchumi ambao Serikali imezingatia asilimia 100 ni haya yafuatayo:-

Kwamba Serikali itekeleze Ilani ya CCM ya mwaka 2005; Mafanikio ya uchumi mpana yawafikie na wananchi; Matumizi ya Serikali yapangwe kwa vipaumbele kwa kuwa mapato hayatoshelezi mahitaji yote; Utulivu wa bei na *exchange rates* urejeshwe; Mifuko ya Dhamana za Mikopo iimarishwe; Wananchi wapewe elimu kuhusu mikopo; Mazingira kuanzisha vyombo vya mikopo na nyumba, mikopo ya kodi, kukodi, yaani *lease* na mengine yawekwe; Michango wa Sekta ya Fedha iongezwe; Riba ya mikopo ishushwe na ile amana ipandishwe; Sheria za Kodi zisaidie kuvutia wawekezaji; Usimamizi wa fedha katika ngazi ya Halmashauri uimarishwe; Serikali Kuu ifuatilie matokeo ya matumizi ya fedha za Serikali hasa katika ngazi ya Halmashauri; *TRA* iongeze juhudi ya kukusanya mapato yafikie angalau Shilingi bilioni 200 kwa mwezi mmoja. Kamati za Bunge zipatiwe muda wa kutosha kushiriki katika uchambuzi wa Bajeti. Yote haya yatazingatiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kuelezea hoja mbali mbali ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwanza kabisa ni suala la mgawanyo wa mapato ya misaada kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, jibu nilisema kwamba, kwa mujibu wa taratibu zilizopo katika Bajeti ya mwaka 2006/07 SMZ imetengewa Shilingi bilioni 21,196 milioni kutokana na miadi ya Wahisani ya kutupatia Shilingi bilioni 471.0, kama misaada isiyokuwa na masharti kwa ajili ya kusaidia Bajeti. Kiasi hiki ni asilimia 4.5 ya misaada hiyo. Labda niseme tu, ukiangalia Bajeti hata ya Zanzibar utakuta kwamba fedha hizi ni kama karibu asilimia 10 ya Bajeti yote ya Zanzibar. Kwa hiyo, ni mchango mkubwa tu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala ya ushirikiano ya kifedha baina ya Serikali zetu yanashughulikiwa na Tume ya Fedha ya Pamoja, yaani *JFC* na *JFC* kwa maelezo yenu, ni kwamba iliajiri mtaalam mwelekezi wa *Price Water House* kutafiti na kushauri kuhusu utaratibu wa kudumu wa mgawanyo wa mapato na gharama za Muungano. Kwa sababu huu ulikuwa si utaratibu wa kudumu wa 4.5, napenda kusema kwamba taarifa ya wataalam hawa sasa hivi inachambuliwa na Sekretarieti ya *JFC* ili baadaye iweze kuwasilishwa kwenye Tume. Tume baada ya hapo itawasilisha ushauri wake kwa Waziri wa Fedha na Mamlaka nyingine husika kwa hatua zaidi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Wizara ya Fedha inangojea kwa hamu kabisa ushauri kutoka Tume ili hatua ziweze kuchukuliwa. Kwa hiyo, mnaweza kuona kwamba kwa kweli tumefika

mbali na napenda kumhakikishia Mheshimiwa Hamad ambaye amelizungumzia suala hili kwamba, suala hili linafuatiliwa kwa karibu sana.

Hoja nyingine ilikuwa ni juu ya matumizi ya Serikali yanayoongezeka kwa kasi huku Serikali ikiendelea kutoa ruzuku kwa Mashirika kama vile *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, matumizi yameongezeka kwa kasi kutokana na dharura. Kwa kweli kuna mambo ya dharura ambayo yametokea. Kuna mambo mengine ambayo huwezi kutegemea. Masuala haya ya ukame hakuna mtu ambaye aliyategemea na kutokana na ukame ndipo ambapo tukapata matatizo ya chakula na isingewezekana kwa vyovyote vile kwa Serikali kuacha kununua chakula cha njaa ikaacha wananchi wanakufa. Lakini pia suala la ukame na kwa sababu umeme wetu mkubwa unategemea maji, basi kumekuwa na suala zima la matatizo ya umeme, pamoja na bei ya mafuta ya petroli ulimwenguni imepanda. Haya ni mambo ambayo kwa kweli yalikuwa hayako katika uwezo wetu kwa wakati huu.

Kwa hiyo, ningesema kwamba kama Serikali kwa mfano isingesaidia *TANESCO* kununua umeme wa *IPTL* na *SONGAs* hali ya mgao wa umeme ingekuwa mbaya zaidi na hivyo kuathiri uzalishaji na shughuli nyingi. Kwa maana hiyo za biashara pamoja na mapato ya Serikali yangeweza kuathirika. Unaweza ku-*imagine* kwamba nchi nzima ingekuwa kwenye giza na hata Bunge la Bajeti lisingeweza kufanyika. Kwa hiyo, mambo haya yalibidi yafanyike ili kwa kweli kuongeza pia uzalishaji katika viwanda vyetu na kutokana na uzalishaji ndipo ambapo tunaweza kupata kodi.

Kwa hiyo, pamoja na Serikali kuisaidia *TANESCO* na mvua kiasi zilizonyesha, hali ya umeme tunaweza kusema bado sio nzuri. Lakini, Serikali imeamua kukodi na kununua mitambo ya kuzalisha umeme wa gesi ili kupunguza tatizo hili. Mmeona kwenye magazeti kwa wale ambao mmesoma lakini pia mmeona kwenye Bajeti fedha nyingi tumeweka katika upande wa nishati, zaidi ya Shilingi bilioni 200 na Waziri wa Nishati na Madini atatoa maelezo zaidi juu ya suala hili atakapowasilisha Bajeti yake.

Suala lingine ni juu ya uwezo mdogo wa Halmashauri kusimamia fedha za Umma. Niseme kwamba tatizo la uwezo mdogo wa Halmashauri kusimamia fedha za Umma liko wazi kwa kila mtu sasa. Ni kweli kwamba kuna tatizo la usimamizi wa fedha katika Halmashauri na tunakuta sasa hivi, kwa mfano fedha nyingi zitakwenda katika Halmashauri kwa mfano, upande wa Afya, upande wa Elimu mambo ya *TASAF*, *PEDEP* na kadhalika. Kwa hiyo, fedha nyingi sana, uwezeshaji wananchi na nafikiri kilichobaki zaidi ni kuchukua hatua za kurekebisha hali hiyo. Wizara ya Fedha inatambua umuhimu wa kufuatilia kwa karibu sana matumizi ya fedha katika Halmashauri zetu.

Kwa sababu hii, kimeundwa Kitengo Maalum cha kufuatilia suala hilo, kinaitwa *Expenditure Traking Unit* kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya Bajeti hii. *Unit* hii ndiyo itafuatilia na itakuwa hatuingii jikoni, lakini tunafuatilia jinsi gani fedha zilivyotumika. Kwa sababu fedha hizi tunapopeleka kwenye Halmashauri, Bajeti hii itakuwa haina maana kama utekelezaji wake utakuwa haupo. Kwa hiyo, suala hili ni la muhimu mkubwa na kitengo hiki kwa kweli kitaimarishwa ili kiweze kufanya kazi kwa uwezo mkubwa.

Serikali pia itaendelea kutangaza kwenye Vyombo vya Habari pamoja na tovuti za Wizara ya Fedha mgao wa Halmashauri kila robo mwaka. Jambo hili litawekwa wazi kabisa, fedha ambazo zimepelekwa kwenye Halmashauri zinapaswa kubandikwa kwenye ubao wa Halmashauri nje ili wananchi pia waweze kuona kila mwezi ni fedha kiasi gani kimepelekwa na fedha zinavyotumika. *(Makofi)*

Jambo hili napenda kulisisitiza kwamba hakuna kuficha na ninasema kwamba kwa sababu pia Waheshimiwa Wabunge ni Madiwani, tunaomba tusaidiane kuhakikisha kwamba fedha zinatumika kwa kile ambacho kimepangwa kwamba fedha hazitatumika kwa kitu ambacho hakijapangwa. Kama fedha zitatumika kwa kile ambacho hakijapangwa hatutaweza hata kidogo kufanya lolote katika Taifa hili. *(Makofi)*

Lingine, Halmashauri zinahimizwa kutoa taarifa kama nilivyosema kwenye mabao ya matangazo na pia Serikali itaendelea kuunganisha Halmashauri zilizobaki katika mtandao wa udhibiti wa matumizi ya fedha za Serikali. Programu hii inaitwa *IFMS*, yaani *Intergrated Financial Management System* na mpaka sasa ni Halmashauri zaidi ya 32 zimeingia katika mtandao na katika mwaka 2006/2007 zoezi la kuunganisha Halmashauri nyingine katika mtandao litaendelea, ambapo Halmashauri 47 zaidi zitaunganishwa.

Pamoja na hayo, kama tulivyoeleza, watumishi wataajiriwa na nafikiri kwa wale ambao mmesoma gazeti, mtaona kwamba tayari *Induction Course* zinafanywa, watumishi wataajiriwa na Serikali Kuu ili kwenda kwenye Halmashauri hizi kushughulika na masuala ya fedha.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni juu ya nani ni wamiliki wa *MEREMETA* na Mwananchi? Kwa maelezo niliyokuwayo ni kwamba *MEREMETA* ni Kampuni ya Serikali iliyoanzishwa kwa lengo la kununua dhahabu kutoka wachimbaji wadogo wadogo. Baadaye Kampuni ilianza mradi wa kuchimba dhahabu katika eneo la Buhemba Mkoani Mara. Kutokana na mwenendo wa kibiashara wa Kampuni kutokuwa mzuri, Serikali hivi sasa imeunda timu, Kamati ya Wataalam ili waweze kuishauri ni kitu gani cha kufanya kuhusu shughuli za Kampuni hii. Haya ndiyo maelezo mafupi ambayo ninayo. Kwa hiyo, Kamati ile bado inafanya kazi na inatoa ushauri kwa upande wa Serikali.

Kwa upande wa wananchi, *Gold* ni kwamba hii ni Kampuni yenye wabia kadhaa, ikiwemo Benki Kuu, yenye lengo la kuanzisha karakana ya kusafisha dhahabu hapa nchini, yaani *Gold Refinery*. Hii inatokana na ukweli kwamba Tanzania sasa inazalisha dhahabu kwa kiwango kikubwa na imeonekana ni vyema tukaangalia uwezekano wa kuisafisha hapa nchini ili kuongeza thamani. Benki Kuu ya Tanzania inashiriki katika mradi huu kwa sababu duniani kote dhahabu huhesabiwa kama fedha za kigeni na Benki Kuu inahusika katika usafishaji na utunzaji wake kama moja ya majukumu yake muhimu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni juu ya Benki ya Maendeleo ya Tanzania, yaani *TIB*. Wakati nikiwasilisha Bajeti ya mwaka 2006/2007 tarehe 15 nilielezea uamuzi wa Serikali wa kuibadili Benki ya Rasilimali Tanzania kuwa Benki ya Maendeleo hasa

kwa ajili ya Sekta mbalimbali zikiwemo Sekta ya Kilimo, Viwanda na Utalii. Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanapenda kupata ufafanuzi zaidi kuhusu mtaji wa Benki na mchakato wa kuibadili kuwa Benki ya Maendeleo. Kwa sababu kama tulivyoeleza ni kwamba fedha zinazohitajika kutosha kuifanya Benki hii iwe ya Maendeleo ni Shilingi bilioni 50.

Lakini mpaka sasa hivi kuna shilingi bilioni 24.9 kutokana na ile Shilingi bilioni 17 ambazo ni fedha zilizotokana na mradi wa biashara ya mafuta ya petroli na baada ya hapo kulikuwa na Shilingi bilioni 7.4 ambazo zilitokana na shughuli zake na faida iliyolimbikiza kulingana na mizania ya vitabu vya hesabu vilivyokaguliwa.

Kwa hiyo, kuna pengo la Shilingi bilioni 25.1. Serikali inafikiria kwamba kwa fedha hizi ambazo inazo kwa hivi sasa *TIB* inaweza ikaanza kujiimarisha katika nyanja za utaalam wa masuala ya mikopo na maendeleo kabla ya kupanua shughuli zake. Lakini Serikali nayo pia kwa sababu ya umuhimu wa Benki hii ya Maendeleo na kwa sababu ya pengo hili kwa kuwa hatukupanga, hatukuweka katika Bajeti hii, tunafikiria kwamba fedha hizi kwanza zilizokuwepo zitumike katika kujenga huo utalaam. Lakini kuanzia mwaka kesho 2007 zitapangwa fedha kwa ajili ya *TIB* kwa muda wa miaka mitatu. Kwa hiyo, tunafikiria kwamba hili nalo litasaidia sana kujenga *TIB.*

Suala lingine ni kuhusu ongezeko la ushuru wa bidhaa kwenye muda wa maongezi ya simu za mkononi. Uamuzi wa Serikali kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye Huduma ya Mawasiliano ya Simu za Mkononi au *Mobile Phone Air Time* kutoka asilimia tano ya sasa hadi asilimia saba ya mauzo, una nia ya kuongeza mapato ya kodi toka kwenye chanzo hiki, na kupanua wigo wa kodi, kwa sababu hapa tunazungumzia jinsi ya kupanua wigo wa kodi. Hii ni njia mojawapo. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha Shilingi bilioni 6,719 milioni. Hizo siyo fedha kidogo. Shilingi bilioni 6,719! Ongezeko la kodi kutoka asilimia tano ya sasa hadi asimilia saba ni sawa na Shilingi sita tu kwa dakika moja ya maongezi. Lakini bei inayotozwa na Makampuni ya simu za mikononi inayolipwa na watumiaji wa simu hizo ni kati ya Shilingi 300 hadi 360 kwa dakika.

Aidha, kiwango cha asilimia saba kinachopendekezwa, nasema kiwango kwa sababu sisi kama Tanzania kwa kweli sio Kisiwa, kwanza siyo Kisiwa, lakini ni sehemu ya Afrika ya Mashiriki. Kwa hiyo, lazima kuna mambo ambayo lazima kuangalia wenzetu wanafanya nini.

Kwa mfano, Kenya hivi sasa ni asilimia 10. Uganda ilikuwa asilimia 10, lakini juzi Waziri wa Fedha ameongeza tena na akafikisha asilimia 12. Sasa sisi tunachosema ni kwamba toka mwaka 2002 tulikuwa asilimia tano, basi tuongeze kiasilimia mbili tufike asilimia saba. Hicho ndicho ambacho kwa kweli tunakieleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, gharama za muda wa maongezi kwa simu ya mkononi hazitokani na kodi pekee. Kuna gharama nyingine kama uunganishaji wa mtandao baina ya Makampuni ya Simu, *inter connection fees* na gharama za kutumia minara ya simu na viwango sahihi vinavyojiwekea Makampuni hayo, yaani *profit margin.* Hata hivyo katika

kipindi cha miaka mitatu iliyopita gharama za uunganishaji baina ya Makampuni ya simu, yaani *inter connection fees* zimepungua kutoka senti 25 hadi senti nane za Kimarekani. Lakini cha kustaajabu, bei kwa watumiaji wa simu hizo hazijapungua. Hii ina maana Makampuni ya Simu yanajipatia faida kubwa. Waheshimiwa Wabunge, ndugu zangu, tunaomba mtukubalie kuongeza hii asilimia mbili ifike asilimia saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni juu ya ushiriki wa Wabunge katika maandalizi ya Bajeti. Kumekuwa na hoja imezungumzwa kuhusu ushiriki wa Wabunge katika kuandaa Bajeti ya Serikali. Hili ni suala la mgawanyo wa majukumu baina ya mihimili ya dola kwa mujibu wa Katiba ya nchi. Tunapotafakari hoja hii, lazima tunajiuliza kama Bunge likishiriki tunajiuliza tokea mwanzo wa kuandaa Bajeti itawezaje kuhoji Bajeti hiyo inapowasilisha Bungeni?

Mheshimiwa Spika, pengine kinachotakiwa ni kuongeza muda wa Wabunge wa kujadili Bajeti ya Serikali. Jambo hili ni zuri, lakini litaongeza gharama. Serikali kwa kuangalia haya mawili, itaangalia na kwa kuuona umuhimu, itaangalia namna ya kuboresha ushiriki wa Waheshimiwa Wabunge katika utaratibu wa *Public Expenditure Review,* yaani *PER* ili kupata maoni yao mapema zaidi. Pia, inaweka msingi wa maandalizi ya Bajeti ya kila mwaka. Kwa hiyo, tutafanya ili tuweze kupata mawazo mapema zaidi ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, suala lingine linahusu fungu la matumizi ya *Employment Allowance* kuzidi fungu la mishahara halisi ya wafanyakazi. Nianze kwa kutoa maelezo mafupi ya mfumo wa kuainisha kasma ya mapato ya matumizi ya Bajeti ya Serikali. Tangu mwaka 1999-2000 Serikali ilianza kuainisha kasma za mapato na matumizi ya Serikali kwa utaratibu wa kimataifa ambao unaitwa *Government Finance Statistic,* yaani *GFS.*

Chini ya utaratibu huu Serikali zote duniani huainisha kasma zao kwa mfumo mmoja na kuziwekea kasma hizo katika mafungu ya kiuchumi, yaani *economic lasters.* Utaratibu huu huwezesha kupima ubora na ufanisi wa utekelezaji wa Bajeti baina ya Mataifa mbalimbali. Chini ya utaratibu huo, kuna vifungu kama vile *Personal Emoluments, Employment Allowancies, Educational Materials, Supplies and Services* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nielezee kifungu cha *Employment Allowance* na niseme kwamba kifungu hiki kimegawanyika na vifungu vidogo vifuatavyo:- Kwanza, katika hii *Employment Allowance* kuna *Leave Travel*, kuna *Ration Allowance*, kuna *Per Diem* ya hapa nchini, kuna *Per Diem* ya nchi za nje, kuna *Sitting Allowance*, kuna *Consitituency Allowance*, kuna *Risk Allowance* na kadhalika.

Katika Kitabu cha Pili cha Matumizi ya Fedha za Serikali, Fungu No. 42, Kifungu 2001, kiasi cha Shilingi bilioni 12 kimetengwa kama *Employment Allowance.* Kiasi hiki cha fedha ambacho ni pamoja na *Consitituency Allowance, Sitting Allowance na Per*

*Diem Domestic* hulipwa ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kutekeleza majukumu yao ya Uwakilishi. Hiyo ndiyo *Employment Allowance* ambayo ina maeneo hayo yote.

Mfano mwingine ni Maafisa wa Serikali wanaotembelea miradi au walioko hapa Dodoma, sasa hivi wako kwa Shughuli za Bunge. Hapa pia wanalipwa fedha zile za *Per Diem* ambayo ni sehemu nayo ya *Employment Allowance.*

Kifungu kingine ambacho mlitaka maelezo ni kile cha *Hospitality*. Kifungu hiki labda nieleze kwamba siyo cha takrima hasa, kama vile tafrija au na sherehe. Bali hutumika kulipia *Catering Expenses*, chakula na *refreshments* kwa Vikao halali vya Serikali. Nilitaka kuonyesha tofauti ya hiyo *Hospitality*.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni Bajeti ya Maendeleo ya Mkoa wa Mwanza kwamba imepungua mwaka 2006/2007 ikilinganishwa na mwaka 2005/2006. Ni kweli kabisa kuwa Bajeti ya Maendeleo ya Mkoa wa Mwanza imepungua kutoka Shilingi bilioni 6.0 mwaka 2005/006 hadi Shilingi 2.0 kwa mwaka 2006/07. Sasa upungufu huo umesababishwa na nini?

Upungufu huo ni matokeo ya kupungua kwa fedha za Wahisani baada ya miradi waliyokuwa wanasaidia kukamilika. Kwa hiyo, Wahisani walikuwepo na baada ya mradi kukamilika wakawa wameondoka, kwa hiyo fedha zikawa zimepungua. Katika mwaka 2005/2006 Mkoa wa Mwanza ulikuwa na miradi ya Wahisani kama ifuatavyo:-

Msaada wa Programu ya Maendeleo ya Wilaya kutoka *(SIDA)* Sweden, Shilingi milioni 700; msaada wa Halmashauri za Wilaya kutoka *UNDP* ni Shilingi bilioni 4.3 na Mradi wa Mama na Mtoto Shilingi milioni 378.7 kutoka *UNICEF*. Aidha, kutokana na *UNDP* Marekani, *New York*, kupunguza Bajeti yake kwa nchi inazozisaidia, Mkoa wa Mwanza hauna tena msaada kutoka Shirika hilo kwa mwaka 2006/2007.

Hali hiyo ndiyo inayosababisha kupungua kwa Bajeti ya Maendeleo ya Mkoa wa Mwanza kwa mwaka 2006/2007. Hata hivyo, kwa upande wa fedha zetu wenyewe, yaani fedha za ndani, Serikali imeongeza Bajeti ya Mkoa wa Mwanza kutoka Shilingi milioni 691 mwaka 2005/2006 kama ilivyokuwa hadi Shilingi bilioni 1.0 mwaka huu 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa juu ya Wizara ya Fedha kwamba haioni ni gharama kwa Watumishi wa Mikoa au Halmashauri kufuata *Payrolls* Hazina kila mwezi?

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ni gharama kwa Watumishi wa Mkoa au Halmashauri kufuata *payrolls* Hazina kila mwezi. Huko nyuma Wizara ya Fedha iliwahi kutuma *payrolls* za mishahara za Mikoa pamoja na Halmashauri zake kwa Makatibu Tawala wa Mikoa au *RAS*, kwa kutumia Kampuni ya Kusafirishia Mizigo ya *DAHACO*. Lakini kulikuwa na ucheleweshaji wa *payrolls* na kwa maana hiyo *payroll* ikichelewa basi na mishahara nayo inachelewa.

Kwa maana hiyo, Hazina ilifikia uamuzi wa kutaka kila Mkoa uteue Afisa mmoja, siyo kila Wilaya, ni kwamba kila Mkoa kwa maana ya Wilaya zote inateua mtu mmoja,

Afisa mmoja ambaye anafuatia *payroll* ya Mkoa kutoka Hazina. Sasa labda nieleze kwamba utaratibu huu wa kufuata *payroll* Hazina ni mzuri kwa sasa hivi kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza sababu za usalama. Kwa vile *payroll* ni nyaraka ya siri, na ni vizuri Mwakilishi wa Afisa Mhasibu aje Wizarani kuchukua mwenyewe kuliko kutuma kwa njia ya Posta au kwa njia ya *bus* au kwa njia nyingine, kutokana na usiri wake na usalama wake. Pili, ni kuwahi kulipa mishahara. Wizara ya Fedha imedhamiria kuhakikisha kwamba mishahara inalipwa kuanzia tarehe 25 ya kila mwezi. Tukituma *payroll* kwa njia ya Posta tutachelewesha mishahara hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba, kwa kweli hali sasa hivi ni nzuri na Waheshimiwa Wabunge watatueleza na sisi kwa sababu na mimi pia nimepata ujumbe kutoka sehemu mbalimbali za mbali kabisa ambapo mishahara walikuwa wanapata tarehe 10, 12, 15, lakini sasa angalau wanapata tarehe 25 na hii imesaidia sana. *(Makofi)*

Lingine ni juu ya uwajibikaji. Mkoa au Halmashauri zinavyotuma Maafisa wao huchukua nyaraka za mishahara, ni rahisi kuwawajibisha kuliko Kampuni za Usafirishaji kama Posta au kama endapo kutatokea na tatizo lolote. Hata hivyo, tunasema kwamba hili linafanyika sasa. Tunajua kwamba bado kuna matatizo. Kwa hiyo, tufanye nini kama utatuzi wa muda mrefu na Serikali imefikiria hili na kutafakari. Serikali imefikiria kwamba inaweza kutekeleza mpango wa kuweza kuunganisha nchi nzima kwa mtandao wa matumizi ya kompyuta hii *Government*, teknolojia ya Serikali. Mpango huu utakapokamilika utawezesha kila Afisa Mhasibu, kupata kwa njia ya mtandao nyaraka za mishahara, yaani *payroll* za fungu lake katika Kituo chake cha kazi badala ya kutumia watu kufuata *payroll* Hazina. Huu ndio mpango ambao Serikali inataka kuufanya ili kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni juu ya Kampuni ya *Tisca* inachukua muda mrefu kuthamini shehena. Kampuni ya *Tisca* ni Kampuni tanzu ya *KOTEKNA Inspection* iliyoingia Mkataba na Mamlaka ya Mapato ili kuweza kukagua mizigo, shehena zinazoingia kutoka nje, yaani *destination inspection.* Utaratibu huu unahusu ukaguzi wa shehena kwa kutumia vyombo, mtambo wa mionzi na pia husaidia kujenga hazina ya bei za bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ya nchi.

Ni kweli kabisa kwamba kuna baadhi ya kadhia ambazo zinapitishwa *Tisca* zinazochelewa kutoka na niseme kwamba kwa sababu ya hili *TRA* ilifanya kama tathmini kwa sababu watu wengi walikuwa wanalalamika. Ilifanya tathmini ambayo iliangalia muda gani ambao unatumika kwa kuondoa mzigo. Hii ilionyesha tathmini yenyewe kwamba kuna tatizo. Lakini ni kweli pia kwamba baadhi ya waagizaji wa bidhaa hawawasilishi kadhia zao mapema, bali ni baada ya shehena hasa magari kufika nchini. Kwa sababu unaweza kuwasilisha kadhia yako kabla ya gari kwa mfano kufika nchini. Ukingoja mpaka inafika nchini, basi unaweza kuchelewa. Aidha, mara nyingine bei zao zilizotumika ni batili. Kwani wengine wanatoa ankara za kughushi na kupotosha maelezo ya shehena.

Serikali kwa kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania, imeanzisha *database* ya thamani au ya bei ambayo kwa kuanzia imesambazwa Dar es Salaam, Tanga, Holili, Kilimanjaro na hivi karibuni Zanzibar na mwezi huu tunategemea itasambazwa Namanga, Sirari, Mwanza na Tunduma. Hii itapunguza sana haja ya kufanya marejeo ya bei kwenye nchi zinazotoka bidhaa na hivyo ucheleweshaji wa kutoa mizigo Bandarini utapungua sana. Kwa sababu kutakuwa na *database* katika maeneo hayo yote ambayo nimeyataja na nafikiri mizigo pia itakuwa inatolewa kwa haraka zaidi.

Pili ni kuongeza kiwango cha hiari cha ulipaji kodi, yaani *compliance* ambacho tutaanzisha mwezi Julai mwaka huu 2006 na utaratibu huu wa *compliance trader* ni kwamba yule mtu ambaye anaonekana kwamba hana matatizo ya kulipa kodi, kwa hivyo, kampuni zile ambazo zinaonyesha kiwango cha juu cha uaminifu zitaruhusiwa kuondosha shehena zao maeneo ya Forodha halafu baadaye ziweze kukaguliwa na hii itasaidia pia kuharakisha kuondoa mizigo kwenye Bandari.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni juu ya mapato ya Serikali yatakayopotea kwa kusamehe kodi ya *VAT* kwenye mafuta ya petroli na hapa kumekuwa na wasiwasi kwamba itakuwaje kwamba mmeondoa *VAT* halafu hapo hapo mmesema kwamba hampotezi mapato? Nisema kwamba kwa kweli Serikali imefanya mahesabu na kuona kwamba hili litawezekana. Niseme kwamba msamaha wa *VAT* kwenye mafuta ya petroli unakadiriwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha Shilingi bilioni 207,813.6 milioni katika mwaka 2006/2007. Hata hivyo, sambamba na hatua ya kufuta *VAT* Serikali imefanya marekebisho katika ushuru wa bidhaa *Excise Duty* kwa mafuta. Hatua hii inatazamiwa kuiongezea Serikali mapato kwa kiasi hicho hicho cha Shilingi bilioni 207,813.6 milioni na kwa maana hiyo kuziba pengo hilo.

Mheshimiwa Spika, bidhaa zinazohusika na hatua hii ya kufuta *VAT* ni petroli, dizeli na mafuta ya taa. *Heavy Finance Oil*, liliulizwa swali kuhusu dizeli ya kuendeshea mitambo viwandani, gesi ya kupikia na mafuta ya Ndege *Jet 1* na *Afrigas*. Kwa maana hiyo ni kwamba Serikali inatarajia Makampuni ya Mafuta hapa nyumbani hayatakuwa na sababu ya kuongeza bei ya mafuta kwa kuwa kiwango cha kodi kitakuwa kile kile kwa lita ya mafuta hata kama bei ya mafuta hayo ikipanda kwenye Soko la Dunia. Sisi tunaona kwamba ni hivyo, kwa sababu *VAT* ni *volume* lakini *Excise Duty* unalipa fedha ile ile kwa lita.

Hata hivyo, labda niseme kwamba marekebisho haya pengine hayatoi hakikisho kwamba bei ya petroli nchini haitaendelea kupanda. Lakini nafikiri haitapanda sana kutegemea na huku itakakopanda. Kwa sababu zitawekwa *static* na kwa maana hiyo tunatarajia Makampuni ya Mafuta nayo yatachukua hatua za kupunguza makali ya bei ikiwa ni pamoja na kupunguza viwango vya faida na gharama nyingine kwenye bei ya mafuta. Hapa niseme kwamba *VAT* ni asilimia 20. Kwa maana hiyo kama *VAT* asilimia 20 ikiwa lita 1,000 na halafu ukachukua kwamba *Excise Duty* labda Sh. 315/= kwa lita moja, kwa vyovyote vile ukiwa unatumia *VAT*, bei itapanda kwa sababu ya *volume*. Lakini kama utatumia *Excise Duty* ni kwamba bei itakuwa *static*.

Sisi tunategemea kwamba kama wenye biashara hawatataka kutengeneza faida kubwa sana, basi hatutegemei kwamba bei ya petroli itaendelea kupanda kama

ilivyokuwa hivi sasa. Lakini nieleze pia kwamba wenye biashara hii ya petroli wao wenyewe walifanya Mkutano na Mheshimiwa Waziri Mkuu na mapendekezo hayo pia waliyatoa na ndipo Serikali ikatekeleza. Hayo naweza kusema kwamba hatutegemei kwa kweli kwamba itaendelea kupanda.

Mheshimiwa Spika, lingine ni juu ya Bajeti inayozungumzia juu ya upanuzi wa wigo wa kodi, lakini bidhaa zinazoongezwa kodi ni zile zile yaani vinywaji baridi, vinywaji vikali na sigara. Ni kweli kwamba ipo haja ya kupanua wigo wa kodi. Hii ndiyo njia pekee itakayotuondoa kwenye adha ya utegemezi. Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuweza kupanua wigo wa kodi mwaka hadi mwaka na itaendelea kufanya hivyo kwa awamu, yaani *phase approached*. Baadhi ya hatua zilizochukuliwa katika miaka ya hivi karibuni ni pamoja na kuanzishwa kwa kodi ya ongezeko la thamani, yaani *VAT* mwaka 1998, kuanzishwa kwa utaratibu wa Kodi ya Makisio, yaani *Presumtive Tax* mwaka 2000, kwa walipa kodi wasiotengeneza mahesabu, kuanzishwa kwa utaratibu wa Namba ya Utambulisho ya Mlipa Kodi, yaani *TIN* mwaka 2001 ili kuwa na orodha sahihi ya walipa kodi na pia vivutio mbalimbali vya uwekezaji ili kukuza uchumi na kupanua wigo wa kodi.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia ilianzisha kodi ya Muda wa Maongezi kwenye simu ya mkono *Air Time* na pia imechukua hatua mbalimbali za kudhibiti ukwepaji wa kodi hasa kupitia katika misamaha ya kodi. Kwa mfano kutumia hati ya malipo ya Hazina, yaani *Treasury Vouchers* kulipia misamaha ya kodi kwa makusudi maalum. Kwa hiyo, *Treasury Voucher*s vinatumika na kwa maana hiyo Serikali inakuwa inalipia kodi. Serikali kwa hivi sasa imeunda Tume Maalum ya kuweza kutathimini Mikataba ya Madini ili kuweza kubaini ni jinsi gani Tanzania inatanufaika na uwekezaji katika Sekta ya Madini kwa njia ya kodi na pia njia nyingine. *(Makofi)*

Aidha, kama nilivyoeleza katika hotuba ya Bajeti, Serikali imepanga kuangalia upya ufanisi wa ukusanyaji mapato kutokana na vianzio visivyo vya kodi kwa lengo la kuboresha makusanyo kutoka kwenye vianzio hivyo. Lazima tupate kodi na kama nilivyosema, kwa kweli inabidi tupate kodi angalau Shilingi bilioni mia mbili kwa mwezi mmoja.

Mheshimiwa Spika, mengi ni juu ya *VAT* kwamba iondolewe kwenye saruji na mabati ili wananchi wawezesha kujenga nyumba bora. Kuondoa *VAT* kwenye saruji na mabati kutaipunguzia Serikali kwanza uwezo wa kuwahudumia wananchi, kwa sababu Serikali inategemea kodi. Licha ya kupunguza mapato ya Serikali, hatua hiyo itaongeza gharama za uzalishaji wa bidhaa hiyo, kwani wazalishaji hawataweza kujirudishia *VAT* watakayokuwa wamelipa katika malighafi ya uzalishaji kwa sababu watafutwa kutoka kwenye usajili wa *VAT* na hivyo bei ya Wizara hizo haitapungua. Aidha, kama nilivyoeleza, mafuta mazito ambayo ni muhimu sana katika mitambo ya kuzalisha saruji yamefutiwa *VAT* kama nilivyotangaza katika hotuba yangu ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni juu ya Serikali inachukua hatua zipi kuondoa tatizo la baadhi ya wafanyabiashara kutotoa ankara ya kodi au risiti kwa mauzo yao. Mamlaka ya Mapato Tanzania imechukua hatua zifuatazo kuondoa tatizo hilo. Kwanza

maeneo yote ya biashara na sehemu za makazi ambapo shughuli za biashara zinaendeshwa, yamegawanywa katika vitalu vidogo vidogo, yaani imegawanywa katika *blocks*, katika maeneo yote ambayo yanafanya biashara, kama katika maeneo ya Kariakoo maeneo ya Ilala, maeneo ya Temeke kote kule ambapo kuna biashara ndogo ndogo imegawanywa katika *blocks* au katika vitalu. Kwa hiyo, inajulikana ni watu gani ambao wanafanya biashara na kwa maana hiyo watu gani wanapaswa kulipa kodi. Moja ya kazi ambayo inafanywa na Maafisa wa Mamlaka katika Vitalu ni kufuatilia kwa karibu sana ili kuhakikisha kwamba wafanyabiashara katika vitalu wanatoa ankara za kodi na stakabadhi kwa mauzo yao.

Katika kipindi cha Julai, 2005 hadi Mei, 2006 jumla ya wafanyabiashara 3,236 walikamatwa kwa kosa hilo na jumla ya Shilingi billioni 1,139 zilikusanywa kutokana na kodi na adhabu. Aidha, Mamlaka ya Mapato ilifanya ukaguzi wa mahesabu ya wafanyabiashara kwa lengo la kupunguza tatizo la kutotoa ankara za kodi na risiti hadi kufikia mwezi Mei 2006 mwaka huu. Jumla ya kaguzi zilizofanywa ni 2,966 na zilikuwa zimefanywa na fedha ambazo ziliweza kukusanywa ni Shilingi bilioni 15,346. Kwa hiyo, tunaweza kuona kwamba kwa kazi hii ya kuweka katika maeneo ya *blocks* katika kila eneo tumeweza kupata fedha hizi, natumaini fedha zaidi zitaweza kupatikana.

Pia, kuanzia mwezi Julai mwaka huu 2006, Mamlaka ya Mapato itaanzisha utaratibu maalum wa kuingiza kila mwezi katika mifumo yake ya kompyuta orodha ya wafanyabiashara wote waliofanya biashara na walipa kodi waliosajiliwa na *VAT*.

Hatua hii ambayo inaitwa *intelligence information dissemination system for VAT returns* inalenga kudhibiti tatizo hilo na pia kuweka kumbukumbu sahihi za manunuzi ya bidhaa au huduma za walipa kodi waliosajiliwa.

Aidha, mamlaka ya mapato inakamilisha mpango wa kuwagawa wafanyabiashara, kuwapanga katika makundi ya kati na madogo ili kuyasimamia, kuwaelimisha walipe kodi kwa hiari, yaani *tax payer* kwa *voluntary complies.* Tungependa watu wengi zaidi waweze kulipa kodi wao wenyewe bila matatizo yoyote.

Serikali pia katika Bajeti hii ya mwaka 2006/2007 kama mnavyoelewa Waheshimiwa Wabunge, imefanya marekebisho ya viwango vya faini kwa kosa la kutoa risiti kutoka 200,000 hadi Sh.500,000/=. Matatizo katika Sekta ya Mafuta kwamba haina mratibu, haina udhibiti wa bei na *flow meters* ina *pressure* ndogo.

Mheshimiwa Spika, masharti ya biashara katika Sekta ya Mafuta nchini yamejazwa au *liberalize* mwaka 1999, wakati huo ni kweli hatukuwa na chombo cha uratibu wa Sekta hiyo. Lakini sasa Serikali imeanzisha chombo cha kusimamia masuala yote ya nishati na maji, yaani *Energy and Water Utility Regulatory Authority* au kwa kifupi *EURA.*

Chombo hiki kinasimamia na pia kuratibu masuala yote yanayohusu nishati ikiwemo nishati ya mafuta. Inategemewa kwamba pia chombo kitaweza kusimamia na kuweza kuratibu pia masuala ya bei haya ambayo niliyazungumza muda sio mrefu.

Aidha, shirika la viwango, yaani *TBS* ikishirikiana na *EURA* vitasimamia pia suala la ubora wa bidhaa za mafuta ya petroli nchini. *(Makofi)*

Hapa Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika alizungumzia juu ya suala zima la *adulteration* na tunategemea kwamba tutafuatilia kwa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari imefunga *flow meters* katika Bandari ya Dar es Salaam ili kudhibiti udanganyifu wa kiasi cha mafuta yanayoingizwa kwa lengo la kukwepa kodi.

Serikali kwa kupitia Mamlaka ya Bandari, pia ipo mbioni kufunga *meter* katika Bandari yaTanga. Zoezi hilo linatarajia kukamilika mwisho wa mwezi Julai mwaka huu 2006. Tatizo la kuchanganya mafuta kama ulivyoeleza la *adulteration* linatafutiwa pia ufumbuzi. Maoni ya Waheshimiwa Wabunge, waliyoyatoa kuhusu njia ya kudhibiti vitendo hivyo viovu yatazingatiwa pia.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni juu ya *Jet A* 1 na I, K, yote ni mafuta ya taa na kuwa wanaoagiza *Jet A* 1 walipe ushuru baadaye warejeshewe fedha zao. Serikali inaanda utaratibu wa kiutawala wa kuingiza mafuta haya *Jet A* 1 nchini ili kudhibiti uwezekano wa kutumika kwa mafuta haya kama mafuta ya taa. Kama tulivyosema kwamba wanaweza kuingiza mafuta ya ndege, lakini wakati huohuo yakachanganywa pia mafuta ya taa pamoja na dizeli pamoja na mafuta haya ya ndege.

Sasa katika utaratibu huo Serikali itasajili Kampuni moja au mbili za mafuta ambazo zitaruhusiwa kuingiza nchini mafuta ya *Jet A* 1 baada ya kuridhika kuwa zinajihusisha na uuzaji wa mafuta hayo kwa Kampuni za Ndege. Badala ya kuwa na utitiri wa Makampuni ambayo mengine ni Makampuni danganyifu. Kwa hiyo, tunakuwa na Kampuni moja au Kampuni mbili basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu Mamlaka ya Mapato kwamba iunde Kitengo cha kushughulia kodi ya pango kwani bado kuna upotevu wa mapato kwenye sekta hii. Mamlaka ya Mapato imeunganisha huduma zake, yaani *integrated oppression* ili kuhudumia walipa kodi kwa ufanisi zaidi na kuwapunguzia gharama kwa kutoa huduma zote mahali pamoja. Mlipa kodi anatumia muda mfupi, kwa kuwa analipa kodi zote anazostahili kulipa katika sehemu moja. Aidha, ili kudhibiti ukwepaji wa kodi ya pango Mamlaka ya Mapato imeimarisha mfumo wake wa usimamizi wa kodi kwa njia zifuatazo:-

Kwanza kuanzisha utaratibu wa vitalu, yaani *Block Management System* kama nilivyoeleza ambapo Maafisa wa kodi wanasajili kila mlipa kodi na kupata taarifa sahihi kwa ajili ya makadirio ya kodi ya pango na nyinginezo.

Pili, kuweza kuimarisha mawasiliano na Taasisi nyingine za Serikali kama Wizara ya Ardhi, Halmashauri za Miji na Wilaya, Kituo cha Uwekezaji Tanzania *Investment Centre* na Taasisi nyinginezo ili kupata taarifa sahihi za majengo.

Tatu, kuweza kutumia taarifa za walipa kodi wengine pamoja na wapangaji wa majengo ili kupata taarifa sahihi za kodi ya pango.

Nne, kuendelea kutoa elimu ya kodi ili kuweza kuhamasisha walipa kodi walipe kwa ridhaa bila ya kusubiri kubughudhiwa. Kwa kweli matarajio ya Serikali ni kuwa hatua hizi zinazochukuliwa na ushiriki wa wananchi kwa ujumla katika kufichua wale wanaokwepa kodi, kwa sababu wananchi wanajua pia wanaokwepa kodi waweze kuwafichua zitaweza kupunguza sana tatizo la ukwepaji wa kodi ya pango.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilikuwa ni juu ya marekebisho ya ushuru wa bidhaa kwa vinywaji baridi. Katika hotuba ya Bajeti nilipendekeza mabadiliko ya viwango vya ushuru ya vinywaji baridi kutoka Sh.41.5 kwa lita hadi Sh. 45/= kwa lita.

Ningependa kufanya marekebisho kidogo kwa sababu tulisema kwamba kodi hizi zinapandishwa kutegemeana na mfumko wa bei ambapo tumeweka mfumko wa bei kwa asilimia saba. Kwa hiyo, upande wa soda nao itakuwa Sh.44.50.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni juu ya Bajeti iliyotengwa kwa MMEM na MMES kwa mwaka 2006/2007 kwamba haitoshi. Niseme kabisa kwamba Bajeti iliyotengwa kwa ajili MMEM na MMES haitoshi na hali hii kwa kweli imesababishwa na ufinyu wa mapato ukilinganisha na mahitaji tuliyokuwanayo.

Wizara yangu inashughulikia tatizo hili kwa kuweza kuongeza juhudi zaidi katika kukusanya mapato ya ndani. Juhudi zinaelekezwa pia kwa Wahisani kuweza kuwashawishi watuchangie zaidi kwa kupitia mkakati wetu wa *JAS,* yaani *Joint Assistance Strategy for Tanzania* kama wenyewe walivyoahidi kwamba hakuna mtoto atakayekosa Elimu ya Msingi kwa ukosefu wa fedha.

Kwa hiyo, tunajitahidi, lakini kama nilivyosema ni kwamba bado haitoshi na tunazidi kujitahidi pale ambapo tunapata mapato zaidi, basi tuweze kuwasukuma huko pia. Lakini pia kuweza kujitahidi kwamba Wahisani pia waweze kutusaidia katika Sekta hii.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilikuwa juu ya malalamiko mbalimbali kuhusu huduma za Benki. Nafikiri hili kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri alilizugusia, kwa hiyo nafikiri kwa sababu ya muda pengine sitakuwa na haja ya kuligusia, lakini niseme kwamba tulifanya Kikao na wenye Benki zote 27 pale Dar es Salaam na wameunda Kamati *(Task Force)* ambayo inaanza kazi yake mwezi huu wa Julai na watamaliza mwezi wa Oktoba, ambapo Serikali imejipanga kufanya kazi kwa maeneo yale yanaoonekana kwamba yanawasumbua sana wananchi, *you know* masuala ya kukosa mikopo kwa wananchi walio wengi hasa Vijijini, ukosefu wa mikopo kwa muda mrefu na kwamba huduma za Benki zaidi hujikita Mijini na kadhalika. Hii ni kwa sababu imeshagusiwa, nafikiri sitoligusia.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu Ushuru wa Forodha wa asilimia kumi kwenye mafuta ghafi ya mawese, yaani *Glub Palm Oil*.

Kikao cha Mawaziri wa Fedha wa nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambacho kiliketi tarehe 8/6/2005 kiliafiki na kuamua kwamba Tanzania itoze ushuru wa asilimia 10, kwenye mafuta ghafi ya mawese yanayoingizwa nchini kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia 2006/2007. Katika kipindi hicho, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zitafanya utafiti wa kubaini njia nzuri ya kuzuia udanganyifu katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zimechukuliwa ili kuweza kuwalinda wakulima wetu wanaozalisha mbegu za mafuta, hususan wakulima wa mawese na alizeti hapa nchini dhidi ya mafuta mengi yanayoingizwa kutoka Malaysia, Indonesia na nchi zingine zinazozalisha zao hilo.

Serikali kwa kweli ilibaini kwamba uko udanganyifu kwa baadhi ya waagizaji wa mafuta hayo kudai kuwa mafuta waliyoagiza ni ghafi wakati ni mafuta yaliyokwishapitia hatua za usafishaji na usindikaji. Eneo hili limekuwa sugu kwa muda mrefu.

Hatua hii ya kuongeza ushuru itakuwa kwa mwaka mmoja wakati Kamati Maalum ya Wataalam wa Nchi Wanachama wa jumuiya ya Afrika Mashariki ikiangalia ni jinsi gani viwanda vyetu vya Afrika Mashariki na Wakulima wetu wanavyokatishwa tamaa ya kuzalisha mbegu za mafuta na kupendekezwa kwa Baraza la Mawaziri la Jumuiya marekebisho yanayohitajika.

Aidha, Viwanda vya Mafuta ya Kula hapa nchini vimegawanyika katika makundi mawili. Kundi moja, linaelewa msimamo wa Serikali, kundi lingine halielewi na ndilo linalotaka ushuru ubaki sifuri ili Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla iendelee kutegemea Malaysia na Indonesia.

Jambo hili kwa kweli tumepata taarifa hata wakulima wa Tanzania wamefurahi sana na kuna maeneo mengine ambayo tayari wameshaanza kupandisha bei ya alizeti kutoka Sh. 170/= mpaka Sh.220/= kule Arusha. Kwa sababu ya muda, kama nilivyosema, kwa kweli Waheshimiwa Wabunge sitaweza kujibu hoja zote. Mnaona wenyewe hata hizi ambazo nimezipanga muda ni mdogo.

Napenda kurudia tena kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia na napenda kurudia kusema tena kwamba yale yote mliyoyachangia tutayafanyia kazi, yale ambayo yanawezekana katika kipindi hiki kama *implementation* tutayafanyia kazi, lakini yale ambayo hatuna uwezo nayo, tutaweza kuyafanyia kazi mwaka kesho wa 2007/2008, *inshallah*.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kutoa shukrani zangu za dhati na kusema kwamba naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijatoa maelezo ya hatua zinazofuata, naomba kwa heshima na taadhima tumtambue pale *Speakers Gallery*, Mzee wetu Mzee Petro Kisumo, mmoja wa wapigania uhuru wa nchi yetu, amefanya kazi kubwa tangu akiwa Kiongozi wa Vyama vya mwanzo kabisa vya Wafanyakazi na ameendelea kuwa mwaminifu kwa nchi yetu hadi leo. Tunakushuru sana Mzee Petro. *(Makofi)*

Pamoja naye yupo Mwanasheria Hassan Mapande, ambaye pia alikuwa Mshauri wa Kampeni ya Chama cha Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu uliopita. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyopo mbele yetu na inayohitaji uamuzi ni kwamba Bunge hili likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Sasa kama nilivyotangaza, tulivyokaribia kusitisha shughuli za Bunge hapo asubuhi utaratibu wa upigaji kura ni wa jina la Mbunge mmoja mmoja na hii inalazimika kufanyika hivyo kwa sababu Katiba imezingatia kwamba upo uwezekano wa Bunge kuikataa Bajeti ya Serikali, jambo ambalo likitokea lina athari nyingine ambazo zinagusa mhimili wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ikitokea hivyo, Mheshimiwa Rais anayo mamlaka ya kulivunja Bunge, turudi kwa wananchi na kufanya uchaguzi mwingine.

Kwa hiyo, tunapiga kura jina moja moja, kwa kuanzia na kwa kuzingatia uzito huo, nitamwomba *Sergeant At Arms* agonge kengele hivi sasa ili kama kuna wenzetu wapo nje waweze kuingia Ukumbini na baada ya hapo nitamwomba Katibu wa Bunge aite majina ya Waheshimiwa Wabunge mmoja baada ya mwingine hadi kura zote 319 au zote zilizopo humu ndani zitakapokuwa zimepigwa.

Nitoe taarifa tu kwamba katika hatua hii Mheshimiwa Spika, hatakiwi kupiga kura, kwa sababu kwa mujibu wa Kanuni zetu yeye ana kura za turufu, kama mambo yakija kwamba mmefungana, basi Mheshimiwa Spika, atapiga kura yake ili kukwamua jambo.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge msishangae kwamba jina la Spika halitaitwa. Tutaanza na jina la Mheshimiwa Waziri Mkuu, tutakwenda kwa mtiririko huo mpaka tumalize. Ahsante sana, kengele ipigwe sasa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuwaita Waheshimiwa Wabunge wote walio nje kuingia Ukumbini)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, inaelekea wote tumo humu. Kwa taarifa yenu, Waheshimiwa Wabunge ambao hamjauzoe Ukumbi huu, kwenye Ukumbi huu kengele haisikiki ndani, inasikika nje, sio kama tulivyozoea Ukumbi ule mwingine.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, muda nilioutoa unatosha. Namwita Katibu sasa, tuanze kushughulikia kupiga kura. Katibu. *(Makofi)*

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba sasa kusoma majina ya Waheshimiwa Wabunge.

| | |
|---|---|
| Mhe. Edward N. Lowassa | - Ndiyo |
| Mhe. Juma J. Akukweti | - Ndiyo |
| Mhe. Muhammed Seif Khatib | - Ndiyo |
| Mhe. Zakia Hamdani Meghji | - Ndiyo |
| Mhe. Harith Bakari Mwapachu | - Ndiyo |
| Mhe. Prof. Juma Athuman Kapuya | - Ndiyo |
| Mhe. Dr. Mary Michael Nagu | - Ndiyo |
| Mhe. John Pombe Joseph Magufuli | - Hakuwepo |
| Mhe. Basil Pesambili Mramba | - Ndiyo |
| Mhe. Prof. Mark James Mwandosya | - Ndiyo |
| Mhe. Dr. Asha-Rose Mtengeti Migiro | - Hakuwepo |
| Mhe. Dr. Juma Alifa Ngasongwa | - Ndiyo |
| Mhe. Andrew John Chenge | - Ndiyo |
| Mhe. Kingunge Ngombale-Mwiru | - Ndiyo |
| Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda | - Ndiyo |
| Mhe. Capt. John Zefania Chiligati | - Ndiyo |
| Mhe. Dr. Ibrahim Said Msabaha | - Ndiyo |
| Mhe. Dr. Hussein Ali Mwinyi | - Ndiyo |
| Mhe. Anthony Mwandu Diallo | - Ndiyo |
| Mhe. Philip Sang'ka Marmo | - Ndiyo |
| Mhe. Margaret Simwanza Sitta | - Ndiyo |
| Mhe. Prof. Peter Mahamudu Msolla | - Ndiyo |
| Mhe. Nazir Mustafa Karamagi | - Ndiyo |
| Mhe. Stephen Masatu Wasira | - Ndiyo |
| Mhe. Prof. David Homeli Mwakyusa | - Ndiyo |
| Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe | - Ndiyo |
| Mhe. Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa | - Ndiyo |
| Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia | - Ndiyo |
| Mhe. Sophia M. Simba | - Ndiyo |
| Mhe. Johnson Paulo Mathias Mwanyika | - Ndiyo |
| Mhe. Anne S. Makinda | - Ndiyo |
| Mhe. Dr. Maua Abeid Daftari | - Ndiyo |
| Mhe. Abdisalaam Issa Khatib | - Ndiyo |
| Mhe. Zabein Muhaji Mhita | -Ndiyo |
| Mhe. Hezekiah Ndahani Chibulunje | - Ndiyo |
| Mhe. Rita Louise Mlaki | - Ndiyo |
| Mhe. Dr. Emmanuel John Nchimbi | - Ndiyo |
| Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | - Ndiyo |
| Mhe. Mathias Meinrad Chikawe | - Ndiyo |

| | |
|---|---|
| Mhe. Mwantumu Bakari Mahiza | - Ndiyo |
| Mhe. Dr. Cyril August Chami | - Ndiyo |
| Mhe. Dr. Luka Jelas Siyame | - Ndiyo |
| Mhe. Salome Joseph Mbatia | - Ndiyo |
| Mhe. Dr. Diodorus Buberwa Kamala | - Ndiyo |
| Mhe. Dr. Milton Makongoro Mahanga | - Ndiyo |
| Mhe. Shamsa Selengia Mwangunga | - Ndiyo |
| Mhe. Dr. Aisha Omar Kigoda | - Ndiyo |
| Mhe. Ludovick John Mwananzila | - Ndiyo |
| Mhe. Dr. Batilda Salha Burian | - Ndiyo |
| Mhe. Bernard Kamillius Membe | - Ndiyo |
| Mhe. Joel Nkaya Bendera | - Ndiyo |
| Mhe. Daniel Nicodem Nsanzugwanko | - Ndiyo |
| Mhe. Dr. David Mathayo David | - Ndiyo |
| Mhe. Celina Ompeshi Kombani | - Ndiyo |
| Mhe. Mustafa Haidi Mkulo | - Ndiyo |
| Mhe. Christopher Kajoro Chiza | - Ndiyo |
| Mhe. Lawrence Kego Masha | - Ndiyo |
| Mhe. Gaudentia Mugosi Kabaka | - Ndiyo |
| Mhe. Jeremiah Solomon Sumari | - Ndiyo |
| Mhe. Mohamed Aboud Mohamed | - Ndiyo |
| Mhe. Dr. Charles Ogesa Mlingwa | - Ndiyo |
| Mhe. Omar Yussuf Mzee | - Ndiyo |
| Mhe. Dr. Abdallah Omar Kigoda | - Ndiyo |
| Mhe. John Momose Cheyo | - Ndiyo |
| Mhe. Mgana Izumbe Msindai | - Ndiyo |
| Mhe. George Malima Lubeleje | - Ndiyo |
| Mhe. William Hezekia Shellukindo | - Ndiyo |
| Mhe. Anna Margareth Abdallah | - Ndiyo |
| Mhe. William Jonathan Kusila | - Ndiyo |
| Mhe. Gideon Asimulike Cheyo | - Ndiyo |
| Mhe. Omar Shabani Kwaangw’ | - Ndiyo |
| Mhe. Juma Suleiman Nh’unga | - Ndiyo |
| Mhe. Mohamed Hamisi Missanga | - Ndiyo |
| Mhe. Hamad Rashid Mohamed | -Ndiyo |
| Mhe. Fatma Mussa Maghimbi | - Ndiyo |
| Mhe. Khalifa Suleiman Khalifa | - Ndiyo |
| Mhe. Magdalena Hamis Sakaya | - Ndiyo |
| Mhe. Masoud Abdallah Salim | - Ndiyo |
| Mhe. Ania Said Chaurembo | - Ndiyo |
| Mhe. Ibrahim Mohamed Sanya | - Ndiyo |
| Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | - Hakuwepo |
| Mhe. Abubakar Khamis Bakary | - Ndiyo |
| Mhe. Mohamed Habib Juma Mnyaa | - Ndiyo |
| Mhe. Dr. Ali Tarab Ali | - Ndiyo |
| Mhe. Salim Abdallah Khalfan | - Ndiyo |

| | |
|---|---|
| Mhe. Salim Yussuf Mohamed | - Ndiyo |
| Mhe. Mwadini Abbas Jecha | - Ndiyo |
| Mhe. Shoka Khamis Juma | - Ndiyo |
| Mhe. Bakari Shamis Faki | - Ndiyo |
| Mhe. Salim Hemed Khamis | - Ndiyo |
| Mhe. Mkiwa Adam Kimwanga | - Ndiyo |
| Mhe. Nuru Awadhi Bafadhili | - Ndiyo |
| Mhe. Riziki Omar Juma | - Ndiyo |
| Mhe. Mwanawetu Said Zarafi | - Hakuwepo |
| Mhe. Ali Said Salim | - Ndiyo |
| Mhe. Savelina Silvanus Mwijage | - Ndiyo |
| Mhe. Ali Khamis Seif | - Ndiyo |
| Mhe. Maida Hamad Abdallah | - Ndiyo |
| Mhe. Mohamed Rished Abdallah | - Ndiyo |
| Mhe. Mohammed Abdi Abdulaziz | - Ndiyo |
| Mhe. Bahati Ali Abeid | - Ndiyo |
| Mhe. Ali Haji Ali | - Ndiyo |
| Mhe. Fatma Othman Ali | - Ndiyo |
| Mhe. Aziza Sleyum Ally | - Ndiyo |
| Mhe. Ame Pandu Ame | - Ndiyo |
| Mhe. Kheri Khatib Ameir | - Ndiyo |
| Mhe. Ameir Ali Ameir | - Ndiyo |
| Mhe. Khadija Salum Ally Al-Qassmy | - Ndiyo |
| Mhe. Said Amour Arfi | - Ndiyo |
| Mhe. Idd Mohamed Azzan | - Hakuwepo |
| Mhe. Rostam Abdulrasul Azizi | - Ndiyo |
| Mhe. Faida Mohamed Bakar | - Ndiyo |
| Mhe. Prof. Feethan Filipo Banyikwa | - Ndiyo |
| Mhe. Elizabeth Nkunda Batenga | - Ndiyo |
| Mhe. Gosbert Begumisa Blandes | - Ndiyo |
| Mhe. Felister Aloyce Bura | - Ndiyo |
| Mhe. Pindi Hazara Chana | - Ndiyo |
| Mhe. Dr. Raphael Masunga Chegeni | - Ndiyo |
| Mhe. Diana Mkumbo Chilolo | - Ndiyo |
| Mhe. Samuel Mchele Chitalilo | - Ndiyo |
| Mhe. Muhammad Amour Chomboh | - Ndiyo |
| Mhe. Paschal Constantine Degera | - Ndiyo |
| Mhe. Hasnain Gulamabbas Dewji | - Ndiyo |
| Mhe. Mohammed Gulam Dewji | - Ndiyo |
| Mhe. Meryce Mussa Emmanuel | - Ndiyo |
| Mhe. Col. Saleh Ali Farrah | - Ndiyo |
| Mhe. Stephen Jones Galinoma | - Ndiyo |
| Mhe. Dr. Zainab Amir Gama | - Ndiyo |
| Mhe. Josephine Johnson Genzabuke | - Ndiyo |
| Mhe. Ali Juma Haji | - Hakuwepo |

| | |
|---|---|
| Mhe. Dr. Haji Mwita Haji | - Ndiyo |
| Mhe. Zuleikha Yunus Haji | - Ndiyo |
| Mhe. Hemed Mohammed Hemed | - Ndiyo |
| Mhe. Maria Ibeshi Hewa | - Ndiyo |
| Mhe. Parmukh Singh Hoogan | - Ndiyo |
| Mhe. Issa Kassim Issa | - Ndiyo |
| Mhe. Yahya Kassim Issa | - Ndiyo |
| Mhe. Athumani Said Janguo | - Ndiyo |
| Mhe. Asha Mshimba Jecha | - Ndiyo |
| Mhe. Rajab Ahmad Juma | - Ndiyo |
| Mhe. Siraju Juma Kaboyonga | - Hakuwepo |
| Mhe. Phares Kashemeza Kabuye | - Ndiyo |
| Mhe. Mgeni Jadi Kadika | - Ndiyo |
| Mhe. Balozi Hamis Suedi Kagasheki | - Ndiyo |
| Mhe. Janet Bina Kahama | - Ndiyo |
| Mhe. Charles Muguta Kajege | - Ndiyo |
| Mhe. Teddy Louise Kasella-Bantu | - Ndiyo |
| Mhe. Mariam Reuben Kasembe | - Ndiyo |
| Mhe. Eustace Osler Katagira | - Ndiyo |
| Mhe. Vita Rashid Kawawa | - Ndiyo |
| Mhe. Gaudence Cassian Kayombo | - Ndiyo |
| Mhe. Charles N. Keenja | - Ndiyo |
| Mhe. Yono Stanley Kevela | - Ndiyo |
| Mhe. Vuai Abdallah Khamis | - Ndiyo |
| Mhe. Mwajuma Hassan Khamis | - Ndiyo |
| Mhe. Hassan Rajab Khatib | - Ndiyo |
| Mhe. Hassan Chande Kigwalilo | - Ndiyo |
| Mhe. Felix Ntibenda Kijiko | - Ndiyo |
| Mhe. Estherina Julio Kilasi | - Ndiyo |
| Mhe. Juma Hassan Killimbah | - Ndiyo |
| Mhe. Aloyce Bent Kimaro | - Ndiyo |
| Mhe. Halima Omar Kimbau | - Ndiyo |
| Mhe. Fuya Godwin Kimbita | - Hakuwepo |
| Mhe. Paul Peter Kimiti | - Ndiyo |
| Mhe. Rosemary Kasimbi Kirigini | - Ndiyo |
| Mhe. Grace Sindato Kiwelu | - Ndiyo |
| Mhe. Capt. John Damiano Komba | - Ndiyo |
| Mhe. Anna Maulidah Komu | - Hakuwepo |
| Mhe. Suleiman Omar Kumchaya | - Ndiyo |
| Mhe. Michael Lekule Laizer | - Ndiyo |
| Mhe. James Daudi Lembeli | - Ndiyo |
| Mhe. Castor Raphael Ligallama | - Ndiyo |
| Mhe. Devota Mkuwa Likokola | - Ndiyo |
| Mhe. Dr. Festus Bulugu Limbu | - Ndiyo |
| Mhe. Benedict Kiroya Losurutia | - Ndiyo |

| | |
|---|---|
| Mhe. Sameer Ismail Lotto | - Ndiyo |
| Mhe. Emmanuel Jumanne Luhahula | - Hakuwepo |
| Mhe. William Vangimembe Lukuvi | - Ndiyo |
| Mhe. Riziki Said Lulida | -Ndiyo |
| Mhe. Anna Richard Lupembe | -Ndiyo |
| Mhe. John Paul Lwanji | -Ndiyo |
| Mhe. Clemence Beatus Lyamba | -Ndiyo |
| Mhe. Susan Anselm Jerome Lyimo | -Ndiyo |
| Mhe. Ernest Gakeya Mabina | -Ndiyo |
| Mhe. Joyce Nhamanilo Machimu | -Ndiyo |
| Mhe. Ephraim Nehemia Madeje | -Ndiyo |
| Mhe. Dr. Binilith Satano Mahenge | -Ndiyo |
| Mhe. Ezekiel Magolyo Maige | -Ndiyo |
| Mhe. Yusuf Rajab Makamba | -Ndiyo |
| Mhe. Jackson Muvangila Makwetta | -Ndiyo |
| Mhe. Benito William Malangalila | -Ndiyo |
| Mhe. Anne Kilango Malecela | -Ndiyo |
| Mhe. John Samwel Malecela | -Ndiyo |
| Mhe. Adam Kighoma Ali Malima | -Ndiyo |
| Mhe. Halima Mohammed Mamuya | -Ndiyo |
| Mhe. Ramadhani Athumani Maneno | -Hakuwepo |
| Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya | -Ndiyo |
| Mhe. Vedastusi Mathayo Manyinyi | -Ndiyo |
| Mhe. Abdul Jabiri Marombwa | -Ndiyo |
| Mhe. Wilson Mutagaywa Masilingi | -Ndiyo |
| Mhe. Masolwa Cosmas Masolwa | -Ndiyo |
| Mhe. Haroub Said Masoud | -Ndiyo |
| Mhe. Janeth Mourice Massaburi | -Ndiyo |
| Mhe. Joyce Martin Masunga | -Ndiyo |
| Mhe. Zubeir Ali Maulid | -Ndiyo |
| Mhe. Lucy Thomas Mayenga | -Ndiyo |
| Mhe. Kiumbwa Makame Mbaraka | -Ndiyo |
| Mhe. Monica Ngezi Mbega | -Ndiyo |
| Mhe. Mwanne Ismaily Mchemba | -Ndiyo |
| Mhe. Halima James Mdee | -Ndiyo |
| Mhe. Mariam Salum Mfaki | -Ndiyo |
| Mhe. Feteh Saad Mgeni | -Ndiyo |
| Mhe. Laus Omar Mhina | -Ndiyo |
| Mhe. Fatma Abdallah Mikidadi | -Ndiyo |
| Mhe. Margreth Agness Mkanga | -Ndiyo |
| Mhe. Dunstan Daniel Mkapa | -Ndiyo |
| Mhe. Nimrod Elirehema Mkono | -Hakuwepo |
| Mhe. Capt. George Huruma Mkuchika | -Ndiyo |
| Mhe. Martha Mosses Mlata | -Ndiyo |
| Mhe. Lediana Mafuru Mng’ong’o | -Ndiyo |
| Mhe. Herbert James Mntangi | -Ndiyo |

| | |
|---|---|
| Mhe. Ali Ameir Mohamed | -Ndiyo |
| Mhe. Elisa David Mollel | -Ndiyo |
| Mhe. Balozi Getrude Ibengwe Mongella | -Ndiyo |
| Mhe. Dr. Samson Ferdinand Mpanda | -Ndiyo |
| Mhe. Amina Chifupa Mpakanjia | -Ndiyo |
| Mhe. Benson Mwailugula Mpesya | -Ndiyo |
| Mhe. Luhaga Joelson Mpina | -Ndiyo |
| Mhe. Kilontsi Muhama Mporogomyi | -Ndiyo |
| Mhe. Felix Christopher Mrema | -Ndiyo |
| Mhe. Raynald Alfons Mrope | -Ndiyo |
| Mhe. Ruth Blasio Msafiri | -Ndiyo |
| Mhe. Manju Salum Omar Msambya | -Ndiyo |
| Mhe. Dr. James Alex Msekela | -Ndiyo |
| Mhe. Balozi Abdi Hassan Mshangama | -Ndiyo |
| Mhe. Mwinchoum Abdulrahman Msomi | -Ndiyo |
| Mhe. Abbas Zuberi Mtemvu | -Ndiyo |
| Mhe. Prof. Idris Ali Mtulia | -Ndiyo |
| Mhe. Mudhihir Mohamed Mudhihir | -Ndiyo |
| Mhe. James Philipo Musalika | -Ndiyo |
| Mhe. Omar Sheha Mussa | -Ndiyo |
| Mhe. Mossy Suleiman Mussa | -Ndiyo |
| Mhe. Bernadeta Kasabago Mushashu | -Ndiyo |
| Mhe. Dorah Herial Mushi | -Ndiyo |
| Mhe. Dr. Harrison George Mwakyembe | -Ndiyo |
| Mhe. Prof. Raphael Benedict Mwalyosi | -Ndiyo |
| Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa | -Ndiyo |
| Mhe. Mbaruk Kassim Mwandoro | -Ndiyo |
| Mhe.Thomas Abson Mwang'onda | -Ndiyo |
| Mhe. Aggrey Deaisile Joshua Mwanri | -Ndiyo |
| Mhe. Hamza Abdallah Mwenegoha | -Ndiyo |
| Mhe. Omar Ali Mzee | -Ndiyo |
| Mhe. Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya | -Ndiyo |
| Mhe. Damas Pascal Nakei | -Ndiyo |
| Mhe. Richard Mganga Ndassa | -Ndiyo |
| Mhe. Philemon Ndesamburo | -Ndiyo |
| Mhe. Sigifrid Seleman Ng'itu | -Ndiyo |
| Mhe. William Mganga Ngeleja | -Ndiyo |
| Mhe. Cynthia Hilda Ngoye | -Ndiyo |
| Mhe. Hadija Saleh Ngozi | -Ndiyo |
| Mhe. Brg. Gen. Hassan Athumani Ngwilizi | -Ndiyo |
| Mhe. Juma Abdallah Njwayo | -Ndiyo |
| Mhe. Dr. Omari Mzeru Nibuka | -Ndiyo |
| Mhe. Sijapata Fadhili Nkayamba | -Ndiyo |
| Mhe. Said Juma Nkumba | -Ndiyo |
| Mhe. Dr. Lucy Sawere Nkya | -Ndiyo |
| Mhe. Tatu Musa Ntimizi | -Ndiyo |

| | |
|---|---|
| Mhe. Lazaro Samuel Nyalandu | -Ndiyo |
| Mhe. Ponsiano Damiano Nyami | -Ndiyo |
| Mhe. Richard Said Nyaulawa | -Ndiyo |
| Mhe. Esther Kabadi Nyawazwa | -Ndiyo |
| Mhe. Juma Said Omar | -Ndiyo |
| Mhe. Lucy Fidelis Owenya | -Ndiyo |
| Mhe. Ussi Ame Pandu | -Ndiyo |
| Mhe. Mwaka Abdulrahaman Ramadhan | -Ndiyo |
| Mhe. Shally Josepha Raymond | -Ndiyo |
| Mhe. Mhonga Said Ruhwanya | -Ndiyo |
| Mhe. Kabuzi Faustine Rwilomba | -Ndiyo |
| Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq | -Ndiyo |
| Mhe. Mohamed Ali Said | -Ndiyo |
| Mhe. Mwanakhamis Kassim Said | -Ndiyo |
| Mhe. Bujiku Philip Sakila | -Ndiyo |
| Mhe. Kidawa Hamid Salehe | -Ndiyo |
| Mhe. Ahmed Ally Salum | -Ndiyo |
| Mhe. Salum Khamis Salum | -Ndiyo |
| Mhe. Prof. Philemon Mikol Sarungi | -Ndiyo |
| Mhe. Lucas Lumambo Selelii | -Ndiyo |
| Mhe.Christopher Olonyokie Ole-Sendeka | -Ndiyo |
| Mhe. Haji Juma Sereweji | -Ndiyo |
| Mhe. Peter Joseph Serukamba | -Ndiyo |
| Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby | -Ndiyo |
| Mhe. Abdulkarim Esmail Hassan Shah | -Ndiyo |
| Mhe. Beatrice Matumbo Shellukindo | -Ndiyo |
| Mhe. Jacob Dalali Shibiliti | -Ndiyo |
| Mhe. John Magale Shibuda | -Ndiyo |
| Mhe- Dr. Guido Gorogolio Sigonda | -Ndiyo |
| Mhe. George Boniface Simbachawene | -Ndiyo |
| Mhe. Dr. Wilbrod Peter Slaa | -Ndiyo |
| Mhe. Mohammed Rajab Soud | -Ndiyo |
| Mhe. Ali Haroon Suleiman | -Ndiyo |
| Mhe. Abdallah Salum Sumry | -Ndiyo |
| Mhe. Eliatta Namdumpe Switi | -Ndiyo |
| Mhe. Hafidh Ali Tahir | -Ndiyo |
| Mhe. Fatma Abdalla Tamim | -Ndiyo |
| Mhe. Kaika Saning'o Telele | -Ndiyo |
| Mhe. Fred Mpendazoe Tungu | -Ndiyo |
| Mhe. Martha Jachi Umbulla | -Ndiyo |
| Mhe. Zaynab Matitu Vulu | -Ndiyo |
| Mhe. Anastazia James Wambura | -Ndiyo |
| Mhe. Chacha Zakayo Wangwe | -Ndiyo |
| Mhe. Dr. James Mnanka Wanyancha | -Ndiyo |
| Mhe. Godfrey Weston Zambi | -Ndiyo |
| Mhe. Kabwe Zuberi Zitto | -Ndiyo |

| | |
|---|---|
| Mhe. Mzee Ngwali Zubeir | -Ndiyo |
| Mhe. Mussa Azan Zungu | -Ndiyo |
| Mhe. Mohamed Said Sinani | -Ndiyo |
| Mhe. Jenista J. Mhagama | -Ndiyo |
| Mhe. Job Y. Ndugai | -Ndiyo |
| Mhe. Joseph James Mungai | -Ndiyo |

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo orodha ya Waheshimiwa Wabunge na jinsi walivyopiga kura.

**SPIKA:** Tafadhali subiri. Waheshimiwa Wabunge, kuna yeyote ambaye hajaitikia au hajapiga kura? Ambaye hajapiga kura naomba anyooshe kidole ili tumwone au asimame ili aweze kupewa fursa ya kupiga kura. Inaelekea wote waliokuwa Ukumbini wamepiga kura.

Sasa Katibu naomba uhesabu hizo kura.

Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima na taadhima naomba nitangaze sasa matokeo ya kura ambazo Bunge letu limepiga hivi punde.

Jumla ya Waheshimiwa Wabunge wote Kikatiba hadi leo ni 320. Jumla ya wale waliotazamiwa wapige kura kwa awamu hii ni 319, ukimwondoa Spika ambaye yupo kwenye Kiti.

Waheshimiwa Wabunge 12 hawapo, kwa hiyo jumla ya Wapigakura, yaani Waheshimiwa Wabunge waliomo Ukumbini ni 307.

**MATOKEO YA KURA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nawasomea matokeo ya kura tulizopiga.

Wale ambao hawakuamua yaani *abstain* Hakuna. Waliosema Hapana, hakuna; Kura za Ndiyo 307 ambazo zinalingana na wapiga kura wote. Kwa hiyo, ninavyofahamishwa ni kwamba ni tukio la kihistoria tangu Siasa ya Vyama Vingi kuanza tangu mwaka 1992. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa matokeo hayo, Hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha imekubaliwa na Bunge hili. Kwa hiyo, Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2006/2007 sasa imepitishwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, katika kura hizi ninapenda kwa furaha kuwashukuru Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani kwa sababu wao hawakufungwa kuiunga mkono hoja hii. Lakini kwa sababu nchi yetu imebahatika kuwa na Upinzani wenye Uzalendo wameona ni vyema waunge mkono hoja ambayo imekaa vizuri na Bajeti ambayo imewekwa vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, Orodha ya shughuli zetu kwa leo imekomea hapo na kwa hiyo, naliahirisha Bunge hadi Siku ya Jumatatu ijayo tarehe 26/06/2006 Saa 03:00 Asubuhi.

*(Saa 12:38 jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatatu,*
*Tarehe 26 Juni, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*